Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 29 Juni, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 139

**Uhitaji wa Hospitali ya Wilaya ya Tanga**

**MHE. AMINA M. MWIDAU** aliuliza:

Hospitali ya Mkoa wa Tanga (Bombo Hospital) inakabiliwa na ongezeko kubwa la wagonjwa kushinda uwezo wake wa kuwahudumia na hakuna hospitali ya Wilaya:-

(a) Je, Serikali inaweza kusema kwanini hadi sasa hakuna Hospitali ya Wilaya?

(b) Je, ni lini sasa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya utaanza, ili kupunguza msongomano mkubwa wa wagonjwa katika Hospitali ya Mkoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina M. Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Jiji la Tanga haina Hospitali ya Wilaya. Mpango wa Serikali uliopo ni kujenga Hospitali ya Wilaya ili kupunguza mlundikano mkubwa wa wagonjwa katika Hospitali ya Mkoa ya Bombo.

Katika mwaka 2010/2011 Hospitali ilipatiwa ruzuku ya maendeleo ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hiyo. Kazi zinazoendelea ni upimaji wa eneo la ujenzi wa Hospitali hiyo baada ya wananchi kutoa eneo Masiwani Shamba kwa Halmashauri ili kutimiza azma hiyo. Ujenzi wa Hospitali hiyo utaanza mwaka 2011/2012

ambapo hHlmashauri imetuma maombi maalum Wizara ya Fedha ya shilingi bilioni 1 kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazoendelea za kujenga Hospitali ya Wilaya, wananchi wa maeneo hayo wanahudumiwa katika Hospitali ya Mkoa wa Tanga ya Bombo, vituo vitatu (3) vya Afya vinavyomilikiwa na Serikali na viwili (2) vya Mashirika binafsi zikiwemo Zahanati zaidi ya thelathini (30) zilizopo.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Hospitali hiyo ya Wilaya ilianza kuzungumzwa katika halmashauri tangu mwaka wa fedha 2008/2009 na awali ujenzi wa Hospitali hiyo ulikuwa ufanyike katika eneo la Mwakidila ambapo halmashauri ndiyo ilitoa hilo eneo na upimaji ulifanyika, fidia zimeishatolewa kwa wananchi na wananchi walifurahia sana ujenzi wa Hospitali hiyo kwao kiasi cha kulipwa fidia chini ya kiwango.

Je, Serikali haioni kuwa kwa kuanza upya upimaji katika eneo jipya la Masiwani Shamba ni ucheleweshaji wa makusudi wa ujenzi wa hospitali hiyo?

(ii) Kwa kuwa Halmashauri ya Jiji inasema kuwa eneo hilo limetolewa bure na wakazi hao wa Masiwani Shamba, na huku kuna manung’uniko kuwa wakazi wa eneo husika wanataka fidia katika eneo hilo.

Je, Serikali iko tayari kuwalipa fidia wakazi wa eneo hilo endapo zoezi la upimaji litamalizika ili kuharakisha ujenzi wa hospitali hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, aah Mheshimiwa usije ukaingia kwenye matatizo haya.

**WAZIRI WA UCHUKUZI (K.n.y. WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amina M. Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kujenga Hospitali ya Wilaya ya Tanga ulifanyika siku nyingi na vikao vyote vya Halmashauri walipoamua tangu Kamati ya Afya na Halmashauri yenyewe uamuzi ulikuwa Hospitali hiyo ijengwe Masiwani Shamba. Hapo katikati kukatokea mfarakano, kilichofanyika sasa hivi ni Halmashauri kurejea katika uamuzi wao wa awali wa kuwa Hospitali hiyo ijengwe Masiwani Shamba. Moja ya changamoto za kujenga Hospitali hiyo Masiwani Shamba ni kuwa, zile sehemu za Masiwani Shamba tangu hapo mwanzo walisema watatoa sehemu hiyo bila kuhitaji fidia.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchanganyiko uliotokea hapo katikati bila ya uamuzi wa Halmashauri kuelezwa kuwa Hospitali sasa itajengwa Mwakidila, Halmashauri ililipa fidia kwa watu wa Mwakidila. Huo uwanja wa Mwakidila upo, na uwanja huo unafikiriwa kutumika kwa shughuli nyingine. Wapo wawekezaji ambao wanataka kujenga Chuo cha Utabibu kwenye uwanja huo, lakini hadi sasa taarifa zilizopo

kwenye halmashauri ni kuwa watu wa Masiwani hawahitaji kulipwa kwa sehemu hizo ambazo Hospitali ya Wilaya ya Tanga itajengwa na wanafurahia kitendo cha hospitali kujengwa hapo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 140

**Madai ya Kufufua upya Mradi wa Maji – Nyang'hwale**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Katika ziara za kampeni za Urais (2010) Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, katika Jimbo la Nyang'hwale aliahidi kufufua upya mradi wa maji unaotoka mkondo wa Ziwa Victoria Nyamtukuza kwenda Nyang'hwale, Kharumwa na Bukwimba ambao utakidhi na kuondoa kero za maji katika vijiji vingi vya maeneo hayo.

(a) Je, mradi huo utaanza lini?

(b) Je, ni vijiji vingapi vitafaidika na mradi huo na ni vipi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein N. Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Nyamtukuza ulijengwa mwaka 1974 kwa lengo la kutoa huduma ya maji katika vijiji 9 vya Nyamtukuza, kakora, Nyarubele, Kitongo, Ikangala, Kharumwa, Izunya, Kayenze na Bukwimba. Mradi huo ulisimama kutoa huduma hiyo mwaka 1994 kutokana na uchakavu wa mtambo wa kusukuma maji na kupungua kina cha maji sehemu ya kuchukulia maji (*intake*).

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua kero ya maji wanayoipata wananchi wa jimbo la Nyang'wale wanaoishi katika eneo la mradi, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imeanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, kwa kutenga fedha kiasi cha shilingi milioni 20 katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 kama Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa *(LGCDG).* Fedha hizo zitatumika kufanya kazi ya kusanifu upya mradi ili kubaini mahitaji halisi ya kufufua mradi huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kazi ya usanifu kukamilka na kubaini gharama zinazohitajika katika kufufua mradi huu, Halmashauri ya Wilaya ya Geita itaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali na kwa wadau wengine wa maendeleo kwa ajili ya kuufufua upya mradi huu.

(b) Mheshimiwa Spika, awali Mradi wa Nyamtukuza ulijengwa kwa ajili ya kutoa huduma ya maji katika jumla ya vijiji tisa (9) ambavyo ni Nyamtukuza, Kakora, Nyarubele, Kitongo, Ikangala, Kharumwa, Izunya, Kayenze na Bukwimba. Aidha, mpango wa kuufufua mradi huu umelenga kurudisha huduma ya maji katika vijiji hivi na vingine vya karibu baada ya usanifu kukamilika na mradi kuanza kutekelezwa.

**SPIKA:** Ahsante sana, swali la nyongeza! Waheshimiwa hata kama ni swali lako unasimama.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa majibu ambayo si ya kuridhisha kutoka kwa Naibu Waziri. Kutokana na shida kubwa na ya muda mrefu tuliyonayo katika jimbo la Nyang'hwale, Mheshimiwa Naibu Waziri atawaeleza nini wananchi kwa sababu hii ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, na leo anajibu kwamba Halmashauri ndiyo inaanza kutafuta pesa kwa ajili ya kufanya usanifu? Je, hizo pesa zitapatikana lini na kutekeleza mradi huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili namwomba Mheshimiwa Waziri tufuatane na yeye ili kwenda kuona hali halisi ya akina mama wanavyopata shida ya kutafuta maji ya kunywa maji ambayo ni machafu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hussein N. Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hussein N. Amar anafahamu kwamba mimi baada ya kutoka kwenye Mkoa wa Mara nilikuwa natokea kwake, na hili analolisema Mheshimiwa Mbunge hapa ni kweli, yaani ni kweli kwamba wale wananchi wana matatizo makubwa, unawakuta wanachota maji kwenye madimbwi ni kweli kabisa. Mheshimiwa Mbunge anachonishangaza hapa ni kuniambia kwamba haridhiki na haya majibu ninayompa hapa.

Mheshimiwa Spika, ngoja nimwambie Mheshimiwa mbunge kwamba nimekuja na faili lote hapa, na ninaomba tukimaliza hapa niende na faili kwa Mheshimiwa Mbunge, nimwoneshe hapa kwamba ni kiasi gani cha fedha ambacho kinategemewa kuingizwa kwenye wilaya na katika Halmashauri yake. Hapa inaonesha kwamba ni shilingi bilioni 2.3 ambazo tutakokotoa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nataka nikiri mbele yako kwamba wananchi wa Nyang'hwale wana matatizo makubwa ya maji na sisi kama Serikali tunalijua hilo tatizo. Mimi ninamwomba tu Mheshimiwa Mbunge tukae wote kwa pamoja, tu-*brain storm* tufikirie kwamba tunawasaidiaje wananchi hawa. Mimi ninayo orodha, nina mahesabu yote hapa, nikimaliza kujibu nitakwenda kukaa naye pale ili tuzungumze tuelewane katika jambo hili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'hwale, kabla ya kwenda huko itabidi uonane na Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa, eeh yule kavaa miwani, hebu uliza swali lako la nyongeza.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, naitwa Lolesia Bukwimba.

**SPIKA:** Aah, leo umebadilisha mtindo, mimi sijakufahamu. Jamani namjua Mheshimiwa Lolesia, ahsante Mheshimiwa Lolesia. (*Kicheko*)

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali la nyongeza. Kama ilivyo katika Jimbo la Nyang'hwale, Mheshimiwa Rais pia aliahidi mradi wa maji katika jimbo la Busanda, katika kijiji cha Katoro. Kwa hiyo, na mimi ningependa kujua. Je, Mradi huu wa Maji Katoro utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, hapa Halmashauri ni hizo hizo na ni hao wote, na wote nimepita kwao tulikuwa wote. Mimi ninakuomba nasema mahesabu ninayo hapa, nimeyaandaa mahesabu yote labda nitoe ile jumla tu kwamba tunakusudia kutumia jumla ya shilingi 2, 636,769,238/= sasa kwamba tunaanza lini na kwamba nitakwenda kule, sitegemei kwamba nitakwenda kwa sababu ni juzi tu nimetoka huko na ninaelewa hilo tatizo analozungumzia.

Mheshimiwa Spika, ikubalike tu kwamba sisi kama Wizara tutakaa na wenzetu hawa ili tusaidie tuone jinsi ambavyo tutawaondoa katika tatizo hili. Ninajua Wizara ya Maji itakuja itazungumza hapa, itasema kwamba ni mkakati gani ambao upo kwa ajili ya kuondoa hili tatizo, lakini *the bottom line is* ni kweli wanachosema Waheshimiwa Wabunge hawa wana matatizo ya maji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Aah! Mnasimama baada ya kuona kwamba swali linaendelea, mbona tunaweza kuendelea wee mpaka tukashindwa kufika mwisho. Sasa tunaenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Na. 141

**Ujenzi wa Chuo cha Ufundi – Ileje**

**MHE. KIBONA N. ALIKO** aliuliza:-

Wilaya ya Ileje imetekeleza agizo la ujenzi wa Sekondari za Kata na imefanya hivyo kabla ya mwaka 2010, ambapo idadi ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha Nne imekuwa ikiongezeka kila mwaka na vijana hao wako mitaani bila kazi.

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuwasaidia vijana hao wa Ileje kwa kujenga chuo cha Serikali ili waweze kujiunga kwenye vyuo hivyo wapate ufundi na kujiajiri wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kibona N. Aliko, Mbunge wa Ileje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kuupongeza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, kwa kutekeleza agizo la Serikali ya Chama cha Mapinduzi la kujenga shule za Sekondari ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa ujenzi wa chuo cha ufundi stadi hutanguliwa na zoezi la kutambua stadi zinazohitajika kufundishwa kwa kushirikisha uongozi wa wilaya na jamii husika.

Hatua nyingine ni pamoja na wilaya husika kutenga eneo la ujenzi wa chuo lenye ukubwa usiopungua hekta 30 na kuwa na Hati Miliki. Aidha, miundombinu muhimu kama vile maji, umeme na barabara inatakiwa kuwa karibu na eneo hilo. Zoezi la utambuzi wa stadi za kufundishwa katika Wilaya ya Ileje halijakamilika na halikufanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumwahidi Mheshimiwa Kibona Aliko, Mbunge wa Ileje kuwa mara fedha zitakapopatikana, zoezi la kutambua stadi litafanyika katika wilaya ya Ileje, ikiwa ni hatua za awali za mchakato wa ujenzi wa chuo cha ufundi stadi. Kwa sasa nawashauri wananchi wa wilaya ya Ileje kutumia chuo cha ufundi stadi Mbeya kupata mafunzo ya ufundi stadi.

**MHE. KIBONA N. ALIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa ajili ya majibu mazuri ya Naibu Waziri. Lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni vigezo gani vilitumika katika kuzipata wilaya 28 ili ziweze kujengewa vyuo vya *VETA*, wakati wilaya ya Ileje haina fursa yoyote na haimo katika zile wilaya 28 za awali?

(c) Mheshimiwa Spika, katika mji wa Itumba ambapo ni makao makuu ya Wilaya siku za nyuma kulikuwa na chuo cha ufundi kikimilikiwa na Jumuiya ya Wazazi

ya Chama cha Mapinduzi, chuo hicho kimekufa. Eneo lipo, jengo lipo, liko jirani na barabara na umeme upo jirani.

Je, Serikali sasa iko tayari kutumia eneo hilo kuanzishia chuo cha *VETA* kama inavyofanya katika sehemu nyingine ambapo inatumia vyuo vya *FTCs?*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kibona N. Aliko, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge angependa kujua vigezo vinavyotumika katika kuchagua hizi wilaya za awali kabisa.

Kwanza ningependa kusema kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema kwamba, tutajenga Vyuo vya Ufundi Stadi kila wilaya, sasa namna tu ya kupata wilaya za awali ni mchakato tu ambao utaendelea ili wilaya zote ziweze kujenga. Lakini baadhi ya vigezo ni kama vifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza lazima kuwe na miundombinu kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, kama vile maji, umeme na barabara viwe karibu. Lakini wilaya hiyo isiwe na chuo chochote cha ufundi binafsi au cha Serikali.

Vile vile wilaya itenge eneo lililomilikiwa lisilozidi hekta 30. zoezi litakalofuata vilevile ni kutambua zile stadi katika eneo husika, stadi za useremala, ufuaji wa umeme na mambo mengine na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vilevile wilaya isiwe na chuo chochote cha FTC kwa sababu baadaye katika hivi vyuo tutaanza vilevile kutoa mafunzo hayo. Hivyo ndivyo vigezo ambavyo angalau naona Ileje walipofika maafisa wetu pale, nadhani kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, waliona hicho chuo cha wazazi, sasa kama Mheshimiwa Mbunge anasema kimekufa basi labda kwa wakati huo kilikuwa kinatumika.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba itabidi Wizara ya Elimu tushirikiane na Jumuiya ya Wazazi na kwa sababu hiyo ni Jumuiya ya Chama cha Mapinduzi na najua hakutakuwa na tatizo, tuangalie kama hilo jengo lipo, linakidhi vigezo na hilo eneo lina hekta 30 na maji yapo, umeme upo, ili angalau wilaya ya Ileje sasa tutume maafisa waweze kufanya utafiti kwa ajili ya zile stadi. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo limekuwa ni upatikanaji wa fedha na kwa kuwa aliyekuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi wakati huo Mama Margaret Sitta ndiye aliyetangaza mpango wa ujenzi wa vyuo vya ufundi kwa zile Wilaya 28.

Hadi leo ni mwaka wa nne hakuna kitu chochote ambacho kinaonekana. Waziri anawaeleza nini Watanzania hata pale ambapo Serikali iliahidi kwamba vyuo vya *VETA 28* vitaanza kujengwa katika Wilaya 28, lakini hadi leo hakuna kinachoonekana?

Ahsante Mheshimiwa Spika.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inaposema kwamba tutafanya jambo fulani haliwezi kufanyika kwa wakati huo huo. Kwa sababu Serikali huwa inapanga Bajeti na sisi wenyewe Wabunge tumeshuhudia Serikali ikiweka Mpango wa Maendeleo wa miaka 5 katika nchi yetu.

Mheshimiwa Margaret Sitta alipokuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi aliahidi kwamba tutatumia majengo ya *FDC's* kwa ajili ya kuweka mafunzo ya *VETA.* Mpaka sasa matamko hayo yapo na ndiyo maana nimesema kwenye jibu langu la msingi kwamba Serikali itaweka mpango huo na baadhi ya vyuo tayari tumeshaanza kuingiza mafunzo hayo. Tuna *FDC's* katika nchi yetu vyuo 55, lakini mpaka sasa vyuo 25 tayari tumeshaanza kutumia mafunzo ya *VETA.*

Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hali hii inakwenda, lakini vile vile sasa hivi Serikali ilikuwa ina fedha inajenga vyuo vya VETA vya mikoa, mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na mkoa mwingine wa nne.

Kwa hiyo, baada ya hapo tutaanza sasa kwenye Wilaya ambazo tayari Wilaya ya Makete tumeshaanza na mwaka kesho kitakamilika kuanza kutoa mafunzo ya *VETA.*

Na. 142

**Ubadilishaji wa Umiliki wa Biashara**

**MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. MHE. CHIKU A. ABWAO)** aliuliza:-

Kumekuwa na mchezo wa wawekezaji toka nje kubadilisha umiliki kwa biashara ile ile kama ilivyofanyika kwa Hoteli ya Sheraton - *Royal Palm*, kwenda *Movenpick,* Kampuni ya Simu *CELTEL* kwenda *ZAIN* na sasa hivi inaitwa *AIRTEL:-*

Je, katika ubadilishaji huu wa kibiashara nchi yetu imepata stahiki yake ya kweli kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chiku Alfan Abwao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la Kampuni moja kuuzwa kwa Kampuni nyingine ni la kibiashara na la kawaida katika ulimwengu sasa wa utandawazi. Uuzwaji huo hufuatana

na wenye hisa kubadilika, mikataba ya mauzo na uendeshaji (*Shareholders Agreements, Management Agreements*) kubadilika au kubakia kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, stahiki ya Serikali kisheria inategemea mfumo wa wanahisa na uandikishwaji. Serikali haikupata stahiki yoyote kwenye mauzo yaliyotajwa. Sheria ya Kodi ya sasa ya Mapato SURA 332, hairuhusu kutoza mapato ya ongezeko la thamani la mtaji unaotokana na hisa za Kampuni ambazo hazikuandikishwa Tanzania *(offshore transaction)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuzingatia uzoefu uliopo, sasa inaliangalia suala hili kwa makini na kupata uzoefu wa nchi nyingine (*best practice*) katika kushughulikia suala la mauzo ya hisa katika masoko ya mtaji nje ya nchi kwa kuangalia namna ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya sasa ili kudhibiti mfumo huu wa Kimataifa wa kuepuka kodi. Hili litafanywa bila kuathiri mazingira ya kufanya biashara nchini.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la uwekezaji nchini linaambatana na misamaha ya kodi kama moja ya sehemu ya kuvutia kwa uwekezaji. Je, sasa Serikali inaweza kuwaeleza Watanzania ni kwa nini hoteli ya Sheraton ambayo ilianzishwa nyakati sawa na Uganda, Uganda bado jina ni lilelile mpaka leo wanatumia Sheraton na Tanzania imebadilika katika majina 3 kwenda *Movenpick* mpaka sasa *Royal Palm* tena *Movenpick* wakati huu.

Suala la pili, ni kwamba je Serikali inaweza kutueleza kama *Sheraton* ambayo baadaye ikaja kuwa *Movenpick* na *Royal Palm* kama ziliweza kulipa kodi katika hili Taifa? Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI):** Mheshimiwa Spika, kama jibu la msingi lilivyoeleza awali kwamba ni kawaida katika uchumi wa soko au soko huru biashara kubadilishana na watu kuuza Makampuni na yule aliyenunua Kampuni hana hiari ya kuendelea jina hilo au akawa na jina lingine.

Kama Uganda haijauza hoteli sisi Tanzania mwenye hoteli kauza kwa mfanyabiashara mwingine hayo mambo ni tofauti, Uganda wanafanya wanavyotaka na Tanzania inafanya biashara yake kama inavyotaka. Ila naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba vivutio vinatolewa pale biashara inapoendelea kwa mujibu wa mkataba ulivyo vivutio haviwezi kutolewa tena upya. Ahsante Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika eneo ambalo tunakosa kodi nyingi ni hili la kuuza hisa zetu katika Makampuni na Makampuni yakauza hisa hizo zao bila kushirikisha Serikali. Kwa mfano *Williamson Diamond* wameuza hisa zao asilimia 75 kwa Patra, hatujui kiasi gani wameuza na mkataba uliokuwepo wa *Williamson Diamond* na Serikali ni tofauti na ambao Patra wameingia. Huoni kwamba Serikali kwa utaratibu huu inakosa kodi zake.

Kwa hiyo wakati umefika sasa kwa Serikali kuwaeleza wananchi zile Kampuni ambazo zinamaliza muda wake miaka 5 wa *Tax Holidays* ziorodheshwe na zijulikane ili wanapohamisha kwa mtu mwingine tujue kama mkataba huo huo hauendelei kwa mtu mwingine ili ukwepaji wa kodi usitokee?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI):** Mheshimiwa Spika, kwanza mimi ni mmoja wa wale wanaoamini kwamba lazima tuangalie mapato yoyote ya Serikali hayapotei kwa njia yoyote ile. Kwa hivyo mkataba wowote lazima uone kwamba mapato ya Serikali yanaangaliwa ipasavyo.

Sasa pale ambapo Kampuni inauzwa kwa mtu mwingine wabia wanapaswa kukaa kwa pamoja. Mikataba huwa inasema kwamba *first priority* ni mbia ambayo uko nayo katika mkataba. Sasa Serikali inapaswa kuona kwamba mbia mwenzake anapouza lazima idai haki yake ya kwanza kuulizwa kabla Kampuni haijauzwa kwa mtu mwingine na tunafanya hivyo.

Na. 143

**Fedha Zilizokusanywa Kwa Njia aya Upatu - DECI**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Mapema mwaka juzi Serikali ilizikamata fedha za wananchi zilizotokana na mchezo wa upatu maarufu kama *DECI,* lakini ukimya mkubwa umekuwepo baada ya fedha husika kuchukuliwa na Serikali:-

Je, ni nini hatima ya fedha hizo za wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** (**MHE. GREGORY G. TEU**) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Jimbo la Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haijachukua fedha za *DECI* bali fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 14.81 zimezuiliwa katika akaunti zinazomilikiwa na Wakurugenzi wa *DECI* katika Mabenki mbalimbali nchini. Fedha hizo ni asilimia 37.77 ya fedha ambazo zinazodaiwa na wanachama wa DECI ambazo ni takriban shilingi bilioni 39.27.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuzizuia fedha hizo uliotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni hatua mojawapo ya uchunguzi dhidi ya *DECI* ambayo ilikuwa inaendesha mchezo wa upatu (*Pyramid Scheme*).

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu na kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa, kesi ya *DECI* Nambari 109/2009 iliyofunguliwa tarehe 12 Juni, 2009 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu bado inaendelea kusikilizwa. Hivyo basi, hatima ya fedha hizo za wananchi itategemea hatma ya kesi hiyo kwani *DECI* ilikuwa na matawi 40 katika mikoa 18 ya Tanzania Bara. Usikilizwaji wa mashahidi wa Dar es Salaam umekwishakamilika na hatua za kuwapata mashahidi kutoka mikoa mingine zimekwishaanza. DECI ilikuwa na jumla ya wanachama wapatao 649,859 na sehemu ya wanachama hawa watahitajika kuja kutoa ushahidi Mahakamani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee swali la nyongeza, lakini mmesema hiyo kesi iko Mahakamani? Tusikilize swali lako.

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Kwa kuwa imethibitika kwamba fedha husika ni za wanachama. Na kwa kuwa waliofanya uhalifu huu ni kile kikundi cha watu 5. Je, Serikali haioni kwamba hasa ukizingatia thamani ya shilingi inashuka, Serikali haioni ni jambo la busara kuandaa utaratibu wa kuwawezesha wale ambao hawajavuna hata mara moja waweze kuzingatiwa katika mgao wa asilimia hii ambayo imeshikiliwa?

Suala la pili, kwa kuwa sheria za nchi kama ambavyo umeeleza zinakataza masuala ya upatu. Lakini kwa kipindi cha miaka 3 DECI ilikuwa inaendelea wakati kuna vyombo vya Serikali vipo kwa ajili ya kusimamia hilo. Je, Serikali imechukua hatua gani kwa maofisa ambao wana majukumu ya kusimamia masuala ya fedha ambao hawakutekeleza wajibu wao hali iliyopelekea Watanzania maskini kuingia hasara kiasi hicho?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Spika, ningeomba sana nieleweke kwa Wabunge wote masuala ambayo yako Mahakamani majibu yake inakuwa vigumu sana kuyatoa hapa. Kwa vile nimesema kwamba suala hili liko Mahakamani kwa hiyo undani wake sana sana itakuwa sio vizuri kulisemea. *(Makofi)*

Lakini naomba ieleweke kwamba hawa Wakurugenzi wa *DECI* kiasi ambacho Serikali imekizuia ni kidogo sana na wanachama wanaodai wanadai hela nyingi sana. Kwa sasa nafikiri ni kwamba….

**SPIKA:** Sehemu ya pili kwamba maafisa wenu ambao hawakuzuia hii kitu kuanza.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** (**MHE. GREGORY G. TEU**): Sehemu ya pili ya maafisa ambao wanahusika na mambo haya ni vile vile kama nilivyosema kwenye

jibu la msingi kwamba suala hili liko Mahakamani inabidi tusubiri tu hapo Mahakama itakapotoa uamuzi wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri labda hukumwelewa mwuliza swali, anasema Maafisa wa Wizara ya Fedha ambao walitakiwa kuzuia kwamba upatu ni kinyume cha kisheria wamefanyiwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** (**MHE. GREGORY G. TEU**): Nafikiri walikuwa bado hawajajiandikisha wakati hii inafanyika.

**SPIKA:** Ni kwamba *DECI* yenyewe iliingia kinyemela ndio anachokisema.

Na. 144

**Shamba la Mpira la Kihuhwi Rubber Plantation**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Shamba la Mpira la Kihuhwi *Rubber Plantation* linakodishwa kwa wawekezaji tofauti:-

(a) Je, wawekezaji hao ni nani na mikataba yao ni ya muda gani?

(b) Je, kumbukumbu zinaonyesha wamevuna na kuuza kiasi gani cha Mpira na kiasi gani cha kodi kimelipwa Serikalini na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza mwaka 2005 - 2010?

(c) Je, ni lini Serikali itachukua jukumu la kulipa madai ya wafanyakazi walioshinda kesi Mahakamani kwa kuwa mkodishaji kutoka Kenya amewatoroka?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mashamba ya Mpira ya Kihuhwi, Muheza na Kalunga Kilombero yalianzishwa na Serikali kupitia Kampuni ya *General Tyre East African Limited (GTEA)* mwaka 1978 kwa ajili ya kuzalisha malighafi ya Kiwanda hicho.

Kwa kuzingatia kuwa shughuli za kilimo hazikuwa za msingi za Kampuni ya *General Tyre*, mwaka 1994 ilirudisha mashamba hayo Serikalini na mwaka 1995 yalikodishwa kwa Kampuni ya *Merchantile Freighters Ltd*. ya Kenya. Hata hivyo, Kampuni ya *Merchantile Freighters Ltd.* Ilishindwa kuendeleza mashamba hayo na

mwaka 2005 Serikali iliwanyang'anya mashamba hayo na hii ilikuwa ni miaka 5 ilishapita.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 mashamba hayo yalikodishwa tena upya kwa Kampuni ya *Jumaan Muhsin El-Ardh Ltd.* ya Tanzania ambayo pia baada ya miaka 4 ilishindwa kuyaendeleza.

Mwaka 2005 Serikali iliyachukua na kuyaweka katika mchakato wa ubinafsishaji kuanzia mwaka 2006 hadi 2008 ambapo mwishoni wa mwaka 2008 Serikali iliamua kusimamisha zoezi hili la ubinafsishaji wa mashamba hayo na kuyarudisha moja kwa moja Serikalini na kukabidhi Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC).*

Mwaka 2009, *NDC* iliingia mkataba na Kampuni ya *Coast Water Project* Ltd. Hadi Desemba 2011 kwa lengo la kutunza na kuendeleza mashamba hayo wakati mkakati wa kuwavutia wawekezaji wakubwa kwa ajili ya upanuzi wa mashamba na kuanzisha mapya ukiandaliwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai, 2009 hadi Desemba, 2010 mpira wa tani 120 ulivunwa katika shamba la Kihuhwi na kodi mbalimbali zililipwa za jumla shilingi milioni 31.5 kati ya hizo shilingi milioni 27.0 zililipwa Serikali Kuu na shilingi milioni 4.5 Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kama kodi ya mazao.

(c) Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa mashamba ya Kihuhwi na Kalunga walishinda kesi dhidi ya waliokuwa waajiri wao Makampuni ya *Merchantile Freighters* ya Kenya na Jumaan Muhsin *El-Ardhi* ya Tanzania ambayo yalikuwa hayajalipa baadhi ya mishahara ya wafanyakazi hao walikuwa wakidai.

Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Juni, 2010 Wizara yangu ilijibu swali Na. 6 la Mheshimiwa Herbert Mntangi na kukubaliana naye kwamba wananchi wa Muheza waliofanyakazi katika shamba Kihuhwi sambamba na wale wa Kilombero wanapaswa walipwe haki zao na jukumu hilo ni la wawekezaji wa Kampuni ya *Merchantile Freighters Ltd.* ya Kenya na *Jumaan Muhsin El-Ardhi* ya Tanzania.

Wawekezaji hawa kwa ufupi ni wezi waliwaibia wananchi kwa kutokuwalipa mishahara yao kwa muda mrefu na wawekezaji hawa ni Wajumbe wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tarehe 14 Juni, 2010 gazeti la Uhuru na Tanzania Daima waliliripoti wakisema wawekezaji wawaliza wafanyakazi na wanasakwa. Kwa maana hiyo ningependa kuchukua nafasi hii kwanza kuwaagiza tena Katibu Mkuu wa Wizara yangu na wataalam katika Wizara yetu washirikiane upya na Wizara ya Mambo ya Ndani washirikiane vile vile na Jeshi la *Interpol* kwanza kuhakikisha kwamba wawekezaji hawa waliowaibia wananchi wa Tanzania wakamatwe.

Nimeangalia upande wa Kenya Kampuni ya *Merchantile Freighters Limited* wameripoti kwamba wamefilisika na utaratibu wetu wa Kimataifa unaruhusu Wakurugenzi wa Makampuni hayo wao wenyewe *in person* wakamatwe.

Tatu, Mahakama ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilishatoa haki kwa wafanyakazi wa mashamba haya yote baada ya kesi hiyo kuendeshwa muda mrefu na ikaagiza kwamba makampuni haya yawalipe wafanyakazi. Ni wajibu sasa hawa watu wasakwe kwa nguvu mpya tuhakikishe wanaletwa hapa nchini wanashitakiwa tena kwanza kwa kukaidi amri ya Mahakama lakini kwa kuwaibia wafanyakazi ambao walipaswa kuwalipa.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jitihada ambazo ameonyesha dhamira. Naomba tu kumkumbasha kwamba hii ni mara ya nne swali hili linaulizwa na wakati wote Serikali imekuwa inakiri kwamba itawasaidia wananchi watalipwa haki zao. Naomba aendeleze jitihada hizo hasa kwa kuzingatia yafuatayo:-

Ni nani aliyeingia mkataba kati ya Serikali na wananchi wale ambao walifanya kazi. Bila shaka aliyeingia mkataba ni Serikali na Mwekezaji. Wananchi wanakosa gani? Kwa sababu tumeahidi kwamba tutawalipa. La pili, kwa sababu tulikwishatoa ahadi kwamba tutawalipa, la pili ni kwamba kwa sababu tulikwishatoa sababu kwamba tutawalipa na inaonekana jitihada za kuwapata hao wawekezaji zitakuwa ngumu je, Waziri haoni kwamba kwa sababu walishapata hela nyingi zaidia ya shillingi milioni 31 ya malipo ya uvunaji, kwamba sasa wawalipe wakati jitihada zikiendelea kuwatafuta wale wezi waliowadhulumu wananchi wa Muheza. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**: Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Juni, 2010, Serikali kupitia aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Cyril Chami, alilijibu hili swali ambalo nimelijibu leo kama lilivyo. Lakini Mheshimiwa Chami alilisitiza kwamba katika juhudi hizi ambazo Serikali inazifanya ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na Wizara ya Mambo ya Nje, Ubalozi wa Tanzania nchini Kenya na leo nimeongeza *Interpol*, *Police system* ya Afrika Mashariki, hawa watu wasakwe. Kwa sababu haiwezekani tukaendelea kuvutia wawekezaji ambao mwisho wa siku baada ya miaka mitano wanawaibia wafanyakazi wa Tanzania. Serikali hiko tayari kuona hilo linafanyika.

Jambo la pili, katika sehemu ya ahadi ya Mheshimiwa Chami mwaka 2010 alisema Serikali itaendelea kuangalia uwezekano wa kuweza kulirejesha hili jambo Bungeni ili mwisho wa yote na kama itakuwa imeshindikana kabisa wananchi hawa bado watastahili kupatiwa haki zao.

Na. 145

**Ujenzi wa Barabara ya Namanyere - Kipili**

**MHE. ALLY K. MOHAMED** aliuliza:-

Bandari ya Kipili itakuwa na shughuli nyingi za kibiashara na nchi jirani za *Congo DRC* na Burundi:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara toka Namanyere - Kipili kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mbunge wa Jimbo la Nkasi, Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Namanyere-Katongoro - Kipili (km 57) ni moja ya barabara zilizo katika mpango maalum wa majaribio ya matengenezo ya barabara *(PMMR)* katika Mkoa wa Rukwa. Chini ya utaratibu huu barabara hufanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe na kutunzwa kwa kufanyiwa matengenezo kwa kipindi cha miaka mitano. Tayari ukarabati kwa kiwango cha changarawe umekamilika na inaendelea kufanyiwa matengenezo. Kwa sasa ipo katika hali nzuri na inapitika majira yote ya mwaka. Serikali kwa sasa haina fedha ya kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Bandari ya Kipili nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri haifahamu sana hii barabara. Hii barabara haijafika kwenye Bandari ya Kipili, bado Km 7.5 haipitiki shahidi Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Mfutakamba tulikwenda naye. Je, Naibu Waziri analithibitishia Bunge barabara inapitika na Serikali imewekeza shilingi bilioni 1.2 kujenga bandari hii lakini hakuna gari linaloingia? Je, Waziri atahakikisha kumaliza kile kipande cha Km 7.5 ili magari yafikie Bandari ya Kipili kwa urahisi?

Je, anathibitisha kwamba muda wa miaka hii mitano baada ya wakandarasi wote waliotia sahihi hizi barabara mpya za lami hakuna barabara yoyote itajengwa kwa kiwango cha lami kama Serikali haina pesa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi nimetembelea Mkoa wa Rukwa na nazifahamu hizo barabara, barabara ya Namanyere, Katongoro, Kipili kama nilivyosema inajengwa chini ya *PMMR* na chini ya mpango huu Mkandarasi anaingia mkataba na *TANROADS* wa miaka mitano kuitengeneza hii barabara na kuifanyia matunzo kwa miaka mitano na mpango huu unakwisha kwa upande wa barabara hii unakwisha kwaka kesho mwezi Novemba na baada ya hapo Mheshimiwa Mbunge tutakaa naye tujadili namna ya kuitunza hii barabara.

Kuhusu swali lake la pili, sio kwamba barabara za lami hatuwezi kujenga tena. *PMMR* ilinza Mkoa wa Rukwa mwaka 2007 ni Mkataba wa miaka mitano na lazima tuuheshimu na lazima aelewe Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Mkoa wa Rukwa Serikali inajenga barabara nyingi sana.

Sasa hivi tuna wakandarasi wa kimataifa sita, wakijenga barabara katika Mkoa huo kutoka Tunduma kwenda Ikana, kwenda Laela, kwenda Sumbawanga kutoka Sumbawanga kwenda Matai, kwenda Kasanga Port kwenda Kanazi mpaka Kibaoni. Sasa mimi nadhani awe na subira tu, Serikali hii haiishi mwaka huu kuwa na Bajeti hata mwaka kesho kuna Bajeti.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, hajanijibu kipande cha kilomita 7.5.

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy ukae chini. (*Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge ukishauliza swali la nyongeza huulizi tena. Mheshimiwa Tizeba.

**MHE. DKT. CHARLES TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa barabara ya Sengerema, Nyehunge, Nzera hadi Geita iko chini ya Mpango huohuo wa *PMMR* na utekelezaji wake si mzuri kama ulivyo katika mkataba wa utekelezaji wa kazi hiyo. Je, Mheshimiwa Waziri ana maoni gani kuhusu mpango huu ambao kiukweli hautekelezwi kama ilivyoazimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, mimi ningemwomba Mheshimiwa Mbunge afuate mfano wa Wabunge wa Mkoa wa Tanga ambapo pia kuna Mradi wa *PMMR* lakini wao hawajasubiri kuja Bungeni kuuliza wao walichokifanya ni kuja Wizarani na kujenga hoja na mimi nimekwenda Tanga kukagua barabara ya Amani, Muheza nikiwa nimefuatana na Mheshimiwa Mbunge Mntangi nikabaini kwamba kweli Mkandarasi kiwango cha kazi ni cha chini. Tumependekeza mkandarasi huyo mkataba wake uhitimishwe. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge afanye hivyohivyo ajenge hoja aje Wizarani tuweze kulipatia ufumbuzi tatizo hilo. *(Makofi)*

Na. 146

**Ahadi ya Kuweka Lami Barabara ya Kidatu –Ifakara**

**MHE. ABDUL R. MTEKETA** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais aliahidi kuwa barabara ya Kidatu - Ifakara yenye urefu wa Km 20 itawekwa lami. Je, Serikali itaanza lini utekelezaji wa ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Mteketa, Mbunge wa Jimbo la Kilombero, kama ifuatavyo:-

Barabara ya Kidatu –Ifakara yenye urefu wa Km. 73.26 ni sehemu ya Barabara Kuu ya Mikumi –Ifakara –Mahenge yenye jumla ya km 178. Azma ya Serikali ni

kuijenga sehemu yote ya barabara ya Kidatu –Ifakara kwa kiwango cha lami na kazi hiyo imekuwa ikitekelezwa kwa awamu kutokana na ufinyu wa Bajeti. Mpaka sasa sehemu yenye urefu wa Km 17 kutoka Kiberenge (Magereza) hadi Signali (Km 10) na kutoka kibaoni (Ifakara) hadi Ifakara Mjini (Km 7) imekwisha kukamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 tumepanga kukamilisha utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Barabara hiyo ilikuwa imeahidiwa miaka mingi na imekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wa Kilombero. Naomba Serikali itueleze wananchi wa Kilombero hasahasa ni lini itaanza kujengwa?

Swali la pili, Barabara ya Kidatu mpaka Ifakara itakapojengwa kwa lami kuelekea daraja la Kilombero itakuwa inapita nje ya Mji wa Ifakara sasa naiomba Serikali waeleze mapema ni sehemu gani barabara hii itapita ili kuondoa usumbufu wa bomoa bomoa kwa wananchi?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza nilisema kwenye jibu langu la msingi kwamba tumeshaanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais. Lakini azma yetu vilevile sio tu kujenga Km 20 ila kujenga barabara yote kutoka Kidatu kwenda Ifakara yenye urefu wa Km 73.26 kwa lami na baadaye tutajenga mpaka Mahenge maana hii yote ni *trunk road* kama nilivyosema. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge naomba awe na uvumilivu.

Kuhusu suala la barabara itapita wapi kuepuka bomoabomoa hili suala ni la kiufundi lakini kwa kweli napenda kumweleweshа Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii itakapopita Ifakara tutatoa *notice* mapema na tutaweka alama kama tulivyozoea. Lakini kama wananchi watapenda isipite mjini ni hiari yao tutapitisha nje ya mji lakini tena baadaye isije ikaanza malalamiko kwamba hatujaipitisha mjini.

Na. 147

**Deni Kubwa la Maji kwa JWTZ**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Mamlaka ya Maji Mtwara (MTUWASA) imeshindwa kulipa deni la umeme kwa *TANESCO* kutokana na deni kubwa la maji ambalo MTUWASA analidai JWTZ kwa takribani miaka miwili sasa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa deni hilo la JWTZ?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mtwara (MTUWASA) inadai vikosi vya JWTZ shilingi 99,166,86.00 ikiwa ni gharama za matumizi ya maji. Deni hilo ni malimbikizo ya Ankara za maji kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili hadi mwezi Mei, 2011.

Jitihada mbalimbali zimechukuliwa na MTUWASA kufuatilia deni hilo liweze kulipwa. Katika kushinikiza kulipwa kwa deni hilo, mwezi Aprili, 2011 MTUWASA ilisitisha huduma ya maji kwenye vikosi vya JWTZ. Baada ya kukatiwa maji, JWTZ iliomba kurudishiwa huduma na kuahidi kulipa nusu ya deni kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2011.

Mheshimiwa Spika, katika kuisaidia Mamlaka ya Majisafi Mtwara pamoja na Mamlaka nyingine zinazotoa huduma ya majisafi nchini, mwezi Februari, 2011 Wizara yangu iliwasilisha Hazina malimbikizo ya madeni ya jumla ya shilingi 3,030,736,000/- ambayo Mamlaka za Majisafi na Majitaka zinadai Taasisi mbalimbali za Serikali. Katika madeni ya jumla ya shilingi mbalimbali za Serikali. Katika madeni hayo Vikosi vya JWTZ vilikuwa vinadaiwa shilingi 1,561,562,263.00 ambapo MTUWASA pekee ilikuwa inadai shilingi 84,541263,00. Lengo likiwa ni kuomba Hazina ilipe madeni hayo moja kwa moja kutoka katika fedha zinazotengwa kulipia umeme na maji zinazotolewa na Hazina.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa ushawishi wa Taasisi za Serikali kutumia fedha zinazotengwa kulipia umeme na maji kwa shughuli nyingine, Wizara yangu inapendekeza Wizara ya Fedha kuweka utaratibu wa kutuma fedha hizi moja kwa moja kwa Taasisi zinazotoa huduma husika.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kabla sijauliza maswali yangu naomba ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Bodi ya Maji ya MTUWASA lakini vilevile ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali yafuatayo:-

Mpaka sasa MTUWASA imejitahidi kulipa takribani robo ya deni la TANESCO, lakini hata hivyo *TANESCO* imetoa tahadhari kwamba kufikia tarehe 29 Juni, kama deni lote itakuwa halijalipwa basi itaikatia MTUWASA umeme na kukatwa kwa umeme inamaana kwamba Manispaa ya Mtwara itakuwa haina maji.

Je Serikali iko tayari sasa kuchukua hatua za haraka ili kuzuia umeme usikatwe?

Swali la pili, kutokana na deni la JWTZ, MTUWASA imeshindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yake ya msingi na hali hii inatishia sana uhai wa MTUWASA Je, Serikali itakuwa tayari kuiwezesha MTUWASA, kifedha ili kusudi iweze kutekeleza majukumu yake ya msingi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Wambura kwa namna anavyosaidia MTUWASA iweze kufanya kazi na naomba nimwahidi kwamba Serikali inachukua hatua kwa sababu hizi fedha zinazotolewa kwa *other charges* mara nyingi zinakuwa hazitoshi lakini ninafikiri katika Bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amewasilisha fedha hizo zimeongezwa na tutaweza kuboresha na kulipa madeni ambayo yanadaiwa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba niongezee majibu mazuri ya Naibu Waziri kama ifuatavyo: Naomba ieleweke kwamba sio kwamba JWTZ inapewa hizo fedha halafu wanashindwa kulipa. Bali ni kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya *utilities* ikiwemo maji na umeme ni kidogo kuliko mahitaji halisi ya Jeshi na kwa sababu hiyo Wizara ya Fedha imefanya uhakiki wa madeni hayo na wameahidi kwamba fedha hizo za maji pamoja na umeme zitalipwa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha. Hivyo naomba Waheshimiwa Wabunge hili tatizo siyo Mtwara peke yake liko, Mtwara, Tabora na Mmalaka nyingine za maji na Umeme na madeni hayo yameshahakikiwa na yatalipwa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

**SPIKA:** Ahsante, mwisho wa mwaka wa fedha ni kesho. Tunaendelea na Swali linalofuata kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Stephen Masele atauliza swali hilo.

Na. 148

**Migogoro ya Mipaka –Shinyanga**

**MHE. STEPHEN J. MASELE** aliuliza:-

Kumekuwa na Migogoro mingi ya mipaka kati ya wananchi na Jeshi la Wananchi katika Kata za Kizumbi eneo la Busongo na Lyandu na Kambi ya Jeshi *Old Shinyanga* na wananchi wa Kata ya Mwawaza eneo la Nyegezi na Itogwang’olo na ile ya Ndembezi, Kitangili na Ibinzamata.

(a) Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi wa Ibadakuli, Kolandoto na Mwanubi waliotii amri ya Serikali kupisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege?

(b) Je, Serikali itafika lini shinyanga ili kutoa uamuzi wa haki na kutatua mgogoro huo wa ardhi?

(c) Endapo itabainika kuwa hati zilizotolewa katika maeneo ya Ndembezi Kijiji na Kitanili zilizotolewa kinyume cha Sheria na Utaratibu. Je, Serikali itakuwa tayari kuzifuta hati zote ili haki itendeke kwa wale walioonewa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Masele, Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini kwa jitihada anazofanya kushughulikia maslahi ya wananchi wa Jimbo lake. Baada ya pongezi napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu, kuwa Serikali imefanya uthamini wa mali (Ikiwemo ardhi, majengo na mazao) katika eneo la kiwanja ya cha ndege cha Ibadakuli na kuthibitisha kuwa zinahitajika zaidi ya shilingi milioni 323,030,000/- kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi 241. Maeneo yaliyofanyiwa uthamini ni vijiji vya Ibadakuli, Kolandoto, Uzogore na Mwamagunguli. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inashughulikia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kulipa fidia wananchi wanaohusika.

(b)Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa tumepokea wito wa ke wa kutaka Uongozi wa Wizara kufika Shinyanga kushughulikia mgogoro wa ardhi na bila kusita nathibitisha tutatembelea Jimbo la Shinyanga Mjini baada ya Mkutano wa Bunge, ili kushirikiana naye na uongozi wa Mkoa wa Wilaya kutatua kero hiyo.

Vilevile napenda kumjulisha kuwa Serikali ilikwishaanza kushughulikia mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania Vikosi vya Kizumbi na *Old Shinyanga* na wananchi wa Kata za Kizumbi na Mwawaza kama ifuatavyo:-

(i) Mgogoro kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania Kikosi cha Kizumbi na wananchi wa Kata za Kizumbi ulihusu haki ya njia ya wananchi hao. Mgogoro huo ulianza kushughulikiwa kwa kuzikutanisha pande zinazohusika na kufikia mwafaka mwaka 2006. Kwa kuwa moja ya pande zinazohusika haukuridhika, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwemo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI, uongozi wa Mkoa, Wilaya na wananchi wenyewe tutakaa pamoja kwa mara nyingine ili kupata suluhu ya kudumu.

(ii) Kuhusu mgogoro kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania Kikosi cha *Old Shinyanga* na wananchi wa Kata ya Mwawanza, Serikali ilishughulikia tangu mwaka 2006 kwa kufanya uthamini wa mali za wananchi 153 na kubaini kuwa jumla ya shilingi milioni 300.73 zinahitajika kwa ajili ya kulipa fidia. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa Bajeti fedha hizo hazijalipwa kwa wananchi. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 ulipaji wa fidia sharti ufanyike ndani ya miezi sita baada ya uthamini kufanyika. Baada ya muda huo kupita mlipaji atatozwa riba ya asilimia sita kila mwaka. Hivyo Serikali inatafuta fedha za kulipa fidia hiyo pamoja na riba iliyoongezeka kutokana na ucheleweshaji.

(c)Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuwa uchunguzi ufanyike endapo itabainika kuwa hati zilizotolewa katika maeneo ya Ndebezi na Kitangiri zilizotolewa kinyume cha Sheria na Kanuni za Ardhi na Mipangomiji zifutwe kwa kuzingatia utaratibu zilizoelekezwa na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999. Kwa sasa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga inafanya uhakiki wa viwanja

vilivyogawiwa kwenye maeneo hayo pamoja na maeneo mengine kubaini mapungufu hayo.

Mheshimiwa Spika, narudia kwa mara nyingine kwa niaba ya Serikali kumpongeza sana Mheshimiwa Masele kwa namna ambavyo amekuwa akitatua kero zinazowakabili wananchi wa Jimbo lake.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:**Mheshimiwa Spika ahsante, Je ni lini Serikali itawasaidia wananchi wanyonge na wa maeneo ya Ndembezi, Bushimangira na Kitangiri ambao wamenyang'anywa ardhi yao ya msingi ambazo walikuwa wakiishi kabla ya upimaji, kwa mfano Ndugu Sudi na Mzee Mwandu wamehukumiwa na Baraza la Ardhi na wameagizwa wahame katika maeneo yao.

Je, fidia ambayo inapaswa kulipwa kwa wananchi ambao wamepisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Shinyanga ni lini Serikali italipa fidia hiyo?

**WAZIRI WA UCHUKUZI (K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, uwanja wa Ibadakuli wa Shinyanga ni moja kati ya viwanja saba ambavyo vipo katika hatua za kuboreshwa sasa hivi. Malipo ya fidia ya wakazi waliokuwa wanastahili yatalipwa katika mwaka wa fedha ujao 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Spika, hajajibu swali langu.

**SPIKA**: Sehemu ya pili.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi ambao wamechukuliwa ardhi yao na bila kupewa viwanja, na wala kufidiwa, Serikali itafanya uchunguzi na tukithibisha kwamba wapo wananchi walionyang'anywa ardhi yao na kuhamishwa bila kupewa viwanja wala fidia hatua zipasazo zitachukuliwa ili kuhakikisha kwamba wananchi wale kwanza wanapata viwanja katika maeneo waliyokuwa wakiishi na kupata fidia inayohusika kwa mali pamoja na ardhi yao ambayo imechukuliwa na Serikali.

Na. 149

**Mpango wa Umeme Kupitia Chanzo cha Mto Malagarasi**

**MHE. DAVID Z. KAFULILA** aliuliza:-

Inasemekana kuwa, Serikali imeahirisha mradi wa kufua umeme kupitia maporomoko ya mto Malagarasi kutokana na kugundulika kwa konokono kwenye maporomoko ya mto huo.

(a) Je, Serikali imefanya upembuzi yakinifu kulinganisha faida na hasara za mradi huo kabla ya kufikia uamuzi uliofikiwa?

(b) Je, ni lini sasa wananchi wa mkoa wa Kigoma watapata mradi utakaozalisha umeme kwa mahitaji hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba utekelezaji wa mradi huu ulisitishwa baada ya ripoti ya upembuzi wa kina kuhusu athari za kimazingira ya Septemba 2010, kuainisha kuwepo kwa konokono adimu kwenye maporomoko ya mto huo katika eneo la mradi la Malagarasi *stage* II. Aidha, kulingana na taratibu za masuala ya mazingira kimataifa mfadhili wa mradi *MCC* alitoa uamuzi wa kusitisha utekelezaji wa mradi katika eneo la Malagarasi *stage* II *November,* 2010. Ni kweli pia kwamba Serikali haijafanya upembuzi yakinifu kulinganisha faida na hasara za kusitisha utekelezaji wa mradi kwa kuwa bado kuna upembuzi yakinifu unaofanyika katika eneo jipya la Malagarasi *stage* III. Aidha, kazi hii ya mradi huu kwa sasa bado inaendelea na imeonesha kuwepo kwa uwezo wa kuzalisha umeme mwingi zaidi kuliko chanzo cha awali (MW8) kwani kwa sasa chanzo hiki cha Malagarasi *Stage* III kinaweza kuzalisha umeme wa hadi kufikia *MW 41*.

(b) Mheshimiwa Spika, jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali kwa kushirikiana na *MCC* pamoja na washirika wengine wa maendeleo kutekeleza mradi wa *Malagarasi stage III (MW41)* ni mojawapo ya mikakati ya kuwapatia wananchi wa Mkoa wa Kigoma mradi utakaozalisha umeme kwa mahitaji yao.

Mkoa wa Kigoma pia inatarajiwa kupata umeme wa uhakiki kutoka kwenye gridi ya Taifa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme ya msongo wa *Kv 220* kutoka Nyakanazi, Kigoma, Rukwa, hadi Mbeya ambapo kampuni ya *CMEC* ya China imekubali kujenga mradi huo chini ya utaratibu wa *Engineering Procurement and construction EPC* chini ya ufadhili wa *China Export Bank*, ambao unatarajiwa kukamilika mwaka 2015. kuanzia Oktoba 2010 kampuni ya *CMEC* imekuwa ikifanya tathmini ya kuunganisha umeme wa gridi kuanzia Nyakanazi -Kigoma ni sehemu ya mradi wa kuiunganisha kwenye *grid* ya Taifa Mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa na Mbeya. Uunganishaji wa Mikoa hii kwenye *grid* ya Taifa utaanzia Kahama-Geita-Nyakanazi-Kigoma-Rukwa-Mbeya.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana.

Kwa kuwa, taarifa ya utafiti huo kuhusu ugunduzi wa konokono ni tafiti ambazo siyo za kweli na ushahid upo ambao siyo wa kweli. Lakini kwa kuwa muda umepita na mradi ule ulikuwa umelenga *generation* kwa maana ya kuzalisha umeme pamoja na uzalishaji.

(a) Je, Serikali imeelekeza pesa za *generation* wapi ambazo zilipaswa zitumike kwa ajili ya ujenzi wa mradi ule, kwamba mradi ule ulikuwa na *generation* na *distribution*, pesa za *generation* zimekwenda wapi?

(b) Kwa kuwa, miradi yote hiyo miwili kwa maana ya kuunganisha Kigoma kwenye gridii ya Taifa na kwa maana ya kuzalisha umeme kupitia Malagarasi bado inaonesha kwamba siyo ya uhakika ndani ya kipindi hiki kwa miaka minne kwenda 2015, na kwa kuwa Wabunge wa Mkoa wa Kigoma hatuko tayari kuendelea kusikia orodha ya miradi mpaka tukimaliza Bunge hili la kumi, Serikali inatueleza nini kuhusu mpango wake wa kuhakikisha Kigoma inapata pesa ya kuzalisha megawati 41 za umeme ndani ya kipindi hiki?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, niseme kwa dhati kabisa kwamba mimi Napata taabu Mheshimiwa Kafulila anaposema utafiti huu siyo wa kweli. Mimi napata taabu kidogo kwa sababu ripoti ya utafiti huo mimi nanayo, na baadaye akipenda tukionana mimi nitampatia hii ripoti. Ripoti hii imefanyika mwaka 2004 ikathibitishwa na watalaam mwaka 2006 ikathibitishwa tena na watalaam mwaka 2008 na ndiyo chanzo cha *MCC* kidogo kuwa na mashaka kusema kama ripoti hii tayari ilikuwepo kwanini hamkutupatia tukalenga dola milioni 57 humu ndani. *(Makofi)*

Ripoti hii kwa ruhusa yako ilibaini kwamba kuna viumbe vitatu ambavyo viko, ambavyo ni *rare.* Kuna kiumbe kinaitwa *Igombigobhi cyclic,* ambaye ni kisamaki hivi, halafu kuna *Igombi cycle mouth cat fish,* hawa wanapatikana katika maeneo marefu zaidi ya ule mto lakini hii *Igomba golden snail* huyu ni kiumbe ambacho kinapatikana pale tu, na kwa bahati mbaya ni pale ambapo ile *construction* ya *site* ilikuwa inakusudiwa.

Mheshimiwa Spika, wakasema hakuna namna, na maisha yake yule snail ni kwamba anataka aishi kwenye maji yanayopita kwa kasi, sasa ukishaweka *dam* pale maji yatakuja kwa utaratibu, kwa hiyo wakasema utaathiri mazingira yake.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu yeye ni mfadhili na ana pesa yake dola milioni 57 anasema anataka kuweka Malagarasi katika mazingira haya anasema atashindwa. Serikali tumesema asubiri kwanza, tuende tukaangalie Malagarasi III amebaini na yeye amekubali kwamba Malagarasi III pana uwezo mkubwa zaidi wa kuzalisha umeme kuliko hata ule.

Mheshimiwa Spika, pale pana megawati 41unasema pesa za jeneresheni za Serikali, siyo za Serikali ni za mfadhili tunayekaa pamoja kukubaliana kwamba tutengeneze pale. Tumekubalina tunakwenda na Malagarasi III. Lakini kwa wakati huo kwa kuwa pale Kigoma tayari pana upanuzi wa mradi wa umeme uliokuwepo kutoka megawati mbili hadi kumi na moja, tunasema ule uliokuwepo uwafikie wananchi kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mradi mmojawapo ni ule ulizungumza juzi kwamba utakwenda Kigoma Kaskazini Bitale, Mkongoro mpaka Kalinze ni sehemu mojawapo. Sehemu ya pili ni huku kuja chini kwa vijiji vitakavyokidhi umeme wa megawati 11.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali inalifanyia kazi na ninakuomba uamini kwamba hili jambo litawezekana wala siyo jambo la maneno maneno kwa miradi hii miwili itakuja lakini kwa sasa mradi wa haraka ni huu.(*Makofi*)

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na maneno yalikuwa mengi. Naomba nitumie muda huu kwa uangalifu ili kusudi tumalize ile orodha ya wachangiaji kwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge leo tuna bahati ya kutembelewa hapa Bungeni na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi wa Uganda Mhandisi Abraham Biandala, Waziri huyu amekuja kusaini makubaliano ya pamoja yaani *Memorandum of Understanding* kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda kuhusu utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari mpya ya Tanga Mwambani, Ujenzi wa reli ya Arusha hadi Musoma, uboreshaji wa reli ya Tanga hadi Arusha, uboreshaji wa bandari ya Musoma na Ujenzi wa Bandari mpya ya Kampala.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mgeni wetu leo ameleta habari njema, tunaomba haya yote yafanyike tuweze kufanya mambo mazuri katika nchi zetu hizi mbili. Karibu sana Waziri, tunakupongeza na karibu jisikie upo nyumbani.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge pia tunao wanafunzi tisa kutoka Chuo cha Mipango, Dodoma wasimame mahali walipo, ahsante karibuni sana. Tunawategemea msome kwa bidii na siyo vinginevyo.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge ninayo matangazo ya kazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na mkutano katika ukumbi wa Msekwa C, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Mheshimiwa Abdulkarim Shah anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tena saa saba watakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 231.

Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa John Mnyika, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kwamba leo tarehe 29 Juni saa Nane Mchana kutakuwa na kikao kwenye Ukumbi wa Msekwa, sijui ni ukumbi gani mkifika pale mtaelewana. Kaimu Katibu wa Kamati ya Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM Mheshimiwa Hussein Mzee, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM kuwa kutakuwa na kikao leo baada ya kumalizika kwa kikao cha Bunge jioni katika ukumbi wa Msekwa, wajumbe wote wa Kamati hiyo wanaombwa wahudhurie bila kukosa.

Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Katibu wa Wabunge wa maeneo yanayolima korosho kibiashara, anawatangazie Wajumbe wote wanaowakilisha maeneo yanayolima korosho kibiashara wakutane leo baada ya kuahirishwa kwa Bunge, hakusema ni muda gani nadhani ni mchana huu chumba namba 227 saa saba.

Waheshimiwa Waunge haya ndiyo matangazo niliyonayo kwa leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu kwa Kanuni ya 33(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007, mtakumbuka kwamba tarehe 23 Juni, 2011, wakati wa mjadala kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia kuongeza muda wa shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma *(Consolidated Holding Cooperation* (*CHC*), Mheshimiwa Kabwe Zitto alikuwa ni mmoja wa wachangiaji wa Azimio hilo, na katika mchango wake pamoja na mambo mengine alitoa kauli kwamba Baraza la Mawaziri lilirubuniwa katika kufikia maamuzi kuhusiana na hilo Shirika. Alieleza Bunge tena kwa kurudia rudia kuwa ana uhakika kuwa maamuzi ya Baraza la Mawaziri ni matokeo ya kurubuniwa huko.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka pia kuwa nilimwagiza alete uthibitisho wa kauli yake na awe amefanya hivyo kufikia tarehe ya leo tarehe 29 Juni, 2011. Kwa kuwa maagizo haya niliyatoa hapa Bungeni na terehe 29 imefika nimeona ni busara niliarifu Bunge mambo yaliyotokea.

Tarehe 23 Juni, 2011 Mheshimiwa Kabwe Zitto aliniandikia barua akinieleza kuwa ili aandaye utetezi wake anaomba nimwombee kwa Katibu Mkuu Kiongozi nyaraka mbili ambazo ni waraka kutoka Wizara ya Fedha na kujadiliwa na *IMTC* kuhusu *CHC,* na Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu *CHC*. Mheshimiwa Kabwe Zitto alinieleza kuwa anafanya hivyo kwa kutumia kifungu cha Kumi cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge sura ya 296 *The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, Cap* 296.

Waheshimiwa Wabunge kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo: S*ubject to this Act and to any statutory all other provision regulating the disclosure of information by public Officers, a member may on request by himself be furnished with information by the Public Officer concerned,* hiyo ndiyo *quotation* ya kifungu cha Kumi.

Waheshimiwa Wabunge, taratibu za Baraza la Mawaziri, kwa uelewa wangu ni kuwa, nyaraka alizoomba Mheshimiwa Kabwe Zitto ni za siri na haziwezi kutolewa. (*Makofi*)

Bunge pia limewahi kuarifiwa hivyo na Spika wa Bunge la Tisa, tarehe 1 Julai, 2008 wakati akitoa uamuzi kuhusu suala la Mheshimiwa Nazir Karamagi, kwa madai yake kuwa, uamuzi wa kuongeza muda wa Mkataba wa *TICS* ulifanywa na Baraza la Mawaziri. Hivyo, Ofisi yangu haiwezi kumsaidia Mheshimiwa Kabwe Zitto, kupata nyaraka alizoomba. Hata hivyo, kwa kuwa Mheshimiwa Kabwe Zitto, wakati akiongea Bungeni, siku hiyo ya tarehe 23 Juni, 2011, aliongea kwa kurudia na kusisitiza kuwa, ana

uhakika na alichokuwa anakisema. Ninaamini kuwa, anaweza kuleta uthibitisho kwa njia anazozijua yeye. (*Makofi*)

Hivyo, uamuzi wangu wa kumtaka uthibitisho, uko pale pale, isipokuwa nimemwongezea siku hadi Jumatatu tarehe 4 Julai, afanye hivyo. Maelezo haya yametolewa leo tarehe 29 na Mheshimiwa Mbunge amepewa barua inayohusika. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo. Katibu karibu kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

(*Majadiliano yanaendelea*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana mlitangaziwa kwamba, watakaoendelea kujadili ni Mheshimiwa Salome Mwambu, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba na wengine watatangazwa baadaye. Kwa sababu nina mkutano, ninamwomba Mwenyekiti aweze kuendelea na shughuli za Bunge.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mchangiaji wetu wa kwanza kwa siku yetu ya leo ni Mheshimiwa Salome Mwambu, atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, ninaomba nisahihishe jina langu; ninaitwa Salome Daudi Mwambu, kuna ‘U’ mwishoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba nitoe shukrani zangu za dhati kutoka moyoni, kwa vile hii ndiyo mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Ninatoa shukrani kwa Wananchi wa Iramba Mashariki, kwa kuniteua kuwa Mbunge wao na kukiteua Chama cha Mapinduzi kiweze kuongoza Dola. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaishukuru familia yangu, kwa kunipa *company*, maana walinitia joto katika mchakato wa kura za maoni. Vilevile ninaomba kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge, Mama Anne Makinda, kwa kuteuliwa kuwa Spika wa Kwanza Mwanamke Tanzania; hongera sana mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaona nijikite katika kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kila mahali wanasema kupanga ni kuchagua, kwa hiyo, kila mahali watu wanakuwa na vipaumbele vyao. Mimi kipaumbele cha kwanza kuchangia katika Hotuba hii ni umeme. Umeme ni kichocheo cha maendeleo, ukiwa na umeme unapata kila kitu; viwanda vitaanza, ajira zinapatikana na mambo mengine. Iramba

Mashariki, tumepewa Wilaya Mpya ya Mkalama, tuna kila sababu ya kutanguliza umeme ili tuje kusukuma maendeleo ya Wilaya yetu ya Mkalama kwani imeunganisha Mikoa miwili; Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Manyara. Tuna kila sababu tupate nishati hii ili tuweze kurahisisha mawasiliano yetu na jirani zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Wilaya ya Mkalama ni Wilaya ya Kilimo; tunalima sana alizeti, mahindi, vitunguu na mtama. Umeme ukipatikana, ina maana Wananchi wata-*invest,* wataweka viwanda vya kukamua mafuta ya alizeti, ambavyo vitawasaidia sana kuongezea pato lao, badala ya kuuza mbegu watauza mafuta. Mathalani, sasa hivi bei ya soko la alizeti shambani inakwenda kwa shilingi 30,000 kwa gunia. Gunia hilo hilo ukilikoboa utoe mafuta litauzwa kwa shilingi 56,000; siyo haba. (*Makofi*)

Vilevile umeme huu huu utatusaidia ili tuweze kuweka miundombinu katika harakati za kuanzisha Wilaya yetu. Makao Makuu, Ndukutu, yatahitaji umeme ili shughuli za ofisi ziweze kwenda vizuri. Tutachimba visima virefu, kwa sababu Wilaya ya Mkalama ipo kwenye Bonde la Ufa. Kuna miamba ambayo ni migumu, hatuwezi kuchimba visima vifupi, mfano, Kata ya Matongo, watafiti walishaangalia wakaona visima vifupi haviwezekani. Tukiwa na umeme, haya maji yatavutwa kwa kutumia pampu za umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yetu ya Mkalama, umeme haupatikani mbali, kwa hiyo, tunaomba Serikali itufanyie hilo kwa sababu unaweza ukavutwa kutoka Iguguno ukienda Kinyangiri, Ndukuti, Gumanga, Ibaga, hadi Mpambala kwenye lile Daraja la Sibiti. Ujenzi utashindikana tusipokuwa na umeme. Kwa hiyo, umeme tunauhitaji sana tuanze kujenga Makao Makuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Wilaya ya Mkalama, kuna sehemu nyingine ya kuvuta umeme kwa sababu tayari umeingia, kuna Hospitali ya Nkungi hapo kuna umeme wa uhakika, unaweza ukavutwa ukapita kwenye Vijiji vya Mwanga, Ilunda, Nkalakala, Mwanga, Kidaraswa ukarudi ukaenda Mwangeza. Hii itategemea na Wataalam wenyewe watakavyopanga, hautafuata maeneo ya mbali, *kilometres*, hapa uko mle mle lakini uko pembezoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ninaomba huu umeme tusifanye makosa tena, utakakopita na vijiji vitakavyopitiwa vipate. Tusije tukafanya makosa kama huko nyuma, umeme unapita lakini mwanakijiji anaangalia juu angani. Kwa hiyo, vijiji vyote vishirikishwe huko utakakopita ili na wao waweze kupata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, ninapenda nichangie ambacho ni kipaumbele katika Wilaya yetu ya Mkalama, kilimo. Wilaya yetu ni ya Kilimo. Jimbo zima kilimo kinastawi, tunalima mazao ya biashara na ya chakula. Sasa tunaomba tuingizwe katika ule Mpango wa Pembejeo na Vocha za Mbolea. Mwaka jana tulipata vocha 10,000, zilitumika zote hazikubaki. Tuliwekwa katika mpango wa majaribio. Ninaomba sasa tuwekwe kwa sababu matunda yameonesha na mazao watu wamevuna mengi, basi tutolewe hayo majaribio tuwekwe *permanent*. Tuongezewe hizo vocha za

mbolea na pembejeo, mbegu ziletwe za mazao yote yanayolimwa; tunalima mahindi, mtama, alizeti na vitunguu, lakini tulipata kwa ajili ya zao moja mwaka jana ambalo ni mtama. *(Makofi)*

Bonde la Iguguno, linazalisha sana mahindi na mazao ya biashara. Siyo kweli kama inavyosemekana eti Wilaya ya Iramba Mashariki inafaa kwa kilimo cha mtama tu, mazao yote yanastawi.  Kwa hiyo, sisi tunalima mazao yote kwa kuchangia; ya chakula na ya biashara na mtama ukiwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunahitaji masoko, inasikitisha sana tunalima vitunguu, ninaweza nikasema ni wa kwanza katika Mkoa wa Singida, lakini kwa vile Wananchi hatuna masoko, wanakuja watu kutoka nchi jirani wanachukua hivyo vitunguu vyetu kwa bei ndogo sana. Wakienda kwao wanavi-*process*, *cuttings* na *sizing*, wanavisafirisha na kuandika hivi vimelimwa Kenya, kumbe vitunguu vimetoka kwetu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunaomba Serikali ilisimamie hili jambo kwa sababu Wananchi wanadhulumika, wakulima hawapati faida. Sasa lini watajikomboa? Tunaposema wajenge nyumba bora watajenga lini? Serikali pia iliangalie Zao la Alizeti, sisi ni wa kwanza, Mkoa mzima wa Singida alizeti inalimwa nyingi sana kutoka Wilaya ya Mkalama. Hilo nalo ndiyo maana tunadai umeme tuka-*invest* kwenye mashine za kukoboa alizeti na kukamua mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niongelee kitu kingine ambacho ni kama kero kwetu nacho ni barabara.  Kwanza, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ameanza kutimiza ahadi zake kwa kututengea Bajeti ya Barabara inayounganisha Wilaya ya Mkalama pamoja na Mkoa wa Shinyanga. Daraja la *CBT* tunashukuru, tunaomba utekelezaji uwe wa haraka kwa sababu Daraja hilo ni ukombozi. Hii ni njia ya mkato kutoka Mkalama kwenda Bugando, huwezi ukazunguka Nzega, sijui wapi lakini hiyo itatufikisha. Tunamshukuru Rais na kumpongeza, tunaomba huo ujenzi uanze mapema. Unajua ukiumwa na nyoka hata jani likikupapasa unarusha mguu unajua ni nyoka huyo huyo. Kwa hali hiyo, kwa vile tulishaahidiwa siku nyingi, tunaomba utekelezaji ufanyike. Tunaishukuru Serikali kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya yetu ipo kwenye Bonde la Ufa, kunahitajika vivuko vingi sana kutoka Kijiji hadi Kijiji, kwa mfano, ukitoka Kijiji cha Mwanga kwenda Hospitali ya Nhungi, unatembea kilomita nane kwa kuzunguka; lakini kikiwekwa kivuko ni mwendo wa kilomita tatu. *Just imagine*, jamani wanawake wajawazito, wanateseka kweli. Kwa hiyo, hilo nalo tunaomba *network* ya ndani ya Wilaya ili tuweze kufunguka kwa sababu hiyo barabara ikitengenezwa, tutatokezea Mbulu hadi Manyara. Kwa hiyo, tayari hapo Wilaya ya Mkalama itakuwa imefunguka na Wilaya zingine; unafika Babati, Babati unaingia Arusha unakwenda Kenya. Kwa hiyo, wafanyabiashara watakuwa na hali nzuri, Wananchi wataweza kusafirisha mazao kwenda kutafuta masoko kuliko kuwangojea wanunuzi waje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi zote Serikali inazotufanyia, tunashukuru, ila ninapenda nisemee barabara moja ya kutoka Iguguno – Kitumbili – Gelembwe – Ulansoni – hadi Msingi. Barabara hiyo siyo barabara tena, ilishakwisha, madaraja hakuna, ina mashimo, mtu akitembea usiku akianguka haponi. Kuna baadhi wameshadondokea kwenye yale makorongo wamepoteza maisha yao. Halafu ndilo eneo tunalosema liko *very productive,* linazalisha chakula, shahidi majirani zetu Shinyanga tunawalisha mahindi. Kwa hiyo, ninaomba sana hiyo barabara ikarabatiwe pamoja na kuwa fedha tulizotengewa ni chache, hazitoshi, kwani uharibifu ulishakuwa mkubwa mno. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, kengle ya pili.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salome Mwambu. Sasa nitamwita Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Ninamshukuru pia Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uhai na afya njema, kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Kabla sijakwenda mbali, ninawashukuru Wanawake wa Mkoa wa Dodoma, walionichagua tena kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili. Ninawaahidi mshikamano wa dhati kabisa na tuendelee kuijenga Dodoma yetu na hasa akina mama na tuepukane na matatizo yanayowakabili wanawake katika kuendeleza shughuli mbalimbali za ujasiriamali na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijakwenda mbali, niseme neno moja ambalo linanikera kidogo katika siku za hivi karibuni kwamba; kuna watu wameamua kuwatia Watanzania vijiti kwenye macho. Mimi sikubaliani hata kidogo na Watanzania, tusikubali watu wanaotutia vijiti kwenye mboni za macho yetu. Watu wanaotaka madaraka kwa kuwashinikiza Watanzania kufanya wanavyotaka. Watu wanatolewa mashambani kwenda kwenye maandamano, wengine walifanya maandamano mwezi wa tatu, mwezi wa nne, kipindi cha kilimo. Ninashangaa Serikali walikubali watu wakaandamana wakaacha mashamba. Tabia hii ikome kabisa. *(Makofi)*

Sisi Wana-Dodoma miaka yote tumeishi kwa amani, hatujui fujo za barabarani na Serikali ikaona Dodoma ni Makao Makuu ya Nchi wakajenga Chuo Kikuu cha mfano. Watanzania tunajivunia Chuo Kikuu cha Mfano, lakini Chuo Kikuu hiki kinataka kuwa donda katika Mkoa wetu wa Dodoma na Watanzania. Wanaoleta vurugu ndani ya Dodoma kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma siyo Wakazi wa Dodoma. Mtu kaacha familia yake kule inastarehe, inalala usingizi mtamu, anakuja kufanya fujo ndani ya Mkoa wetu; hatutakubali. Mkuu wa Mkoa upo hapo kwenye *Gallery*, unisikie na uniunge mkono; wanaoleta fujo unawajua na tunawajua tusiwaachie. Watoto wamekuja kusoma, wazazi ambao vijana wenu wamekuja kusoma Mkoa wa Dodoma, waambieni watoto wasome, siasa ya nini? Wanaowadanganya wana posho, wana mishahara wana nyumba, wana magari na wao hawana kitu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakubaliana na hilo na Wana-Dodoma tuungane pamoja, tusikubali Chuo Kikuu cha Dodoma kivurugike; wanafunzi wasome, vijana wasome. Inaniuma sana ninapoona kwamba, Serikali imetumia rasilimali nyingi kwa ajili ya kujenga *UDOM*, lakini baadhi ya watu ambao wanapita pale kuwashawishi watoto. Wanakwenda wanaandika nne kwenye mabaa wanakunywa bia zao, wanakula vizuri, halafu watoto wanalala Nyerere Square pale; hawakuwa na chakula wala hakuna aliyekwenda kuwasalimia. Wale washawishi hakuna aliyekwenda kuwasalimia, matokeo yake wanatutafuta Wabunge wa Dodoma na Wabunge wa Majimbo kule walikotoka wakapate nauli; siyo haki. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma vizuri Kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na nimeona upungufu ambao Mheshimiwa Waziri ameueleza na sisi ni mashahidi kwamba, kwa sasa pesa nyingi zinapelekwa katika Halmashauri zetu kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, lakini Miradi hii haitekelezwi ipasavyo hasa katika Kata na Vijiji kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Amesema kwamba, makusanyo yameshuka, mwaka wa fedha uliopita tumekusanya asilimia 67 tu na tunatakiwa sasa Halmashauri zetu zifanye juhudi katika kukusanya makusanyo.

Mheshimiwa Waziri amesema pia kwamba, ili kuimarisha Halmashauri hizo, amewahamisha watumishi 164, suala siyo kuamisha watumishi, suala ni kuangalia utendaji wao, kusimamia utendaji wao, kuwasaidia katika elimu, kuajiri wenye uwezo na wengine wanaohamishwa ni wale ambao hawakutenda vizuri katika Halmashauri zao; uhamisho siyo suluhu. Suluhu ni kuangalia tatizo liko wapi; kama tatizo watumishi hawatoshi waajiriwe, kama tatizo ni elimu yao wakasomeshwe ili Halmashauri zitende navyotakiwa na ninaiomba Serikali iweke utaratibu, Halmashauri zipeleke Ripoti za Kazi kila mwezi kwa Mkuu wa Mkoa. Mkuu wa Mkoa apeleke Ripoti yake ya kazi kwa Wizara inayohusika, lakini tukikaa mpaka mwisho wa mwaka, mpaka *CAG* aseme kwamba, hapa utendaji siyo mzuri, hatutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya *CAG* inaonesha 2008/2009 kuna Hati Safi za Halmashauri zilikuwa 77, lakini kwa mwaka 2009/2010 zilikuwa 65. Tunaona utendaji unavyoshuka, kuna haja ya kuweka mkakati wa kufuatilia fedha za maendeleo katika Halmashauri zetu. Ninaomba sana Wakuu wa Mikoa, wajitahidi kuhakikisha kwamba, Halmashauri wanapeleka Ripoti za Kazi kila inapobidi na hasa kila mwezi ili wawe *up to-date* na kazi zinazofanyika katika Halmashauri zetu. Tunaona Rais wetu, kila siku anakwenda katika nchi za wahisani kuomba misaada kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika nchi yetu, lakini pesa zinazokuja zisiposimamiwa vizuri, maendeleo hayatakuja. Tumuunge mkono Rais wetu, kwa kufanya kazi, kufuatilia Miradi katika vijiji vyetu, katika Kata zetu na katika Halmashauri zetu; mwisho wa siku tutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu Kilimo Kwanza. Nimesoma katika Taarifa ya Waziri kwamba, kuna Mpango Kabambe wa Kilimo cha Kisasa katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, lakini Kilimo Kwanza haikutangazwa kwa Mikoa hiyo tu; Mikoa ambayo imewekewa Mpango unaoitwa Sangon, ninashauri kwamba, Mpango huu

uende katika Mikoa yote, tugawanye kwa Kanda, Kanda ya Kati tunawea tukaelekezwa kulima mazao yanayostawi katika Mikoa yetu.

Kwa mfano, mikakati ikiwekwa na tukiambiwa kwamba, Mkoa wa Dodoma tulime alizeti, mtama, ulezi na karanga, tunaweza na tukafika mbali. Mheshimiwa Lukuvi, alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma alisema, kila kaya ilime mtama heka mbili, tulilima na chakula kikawa kingi sana na bado tunaweza tukafanya hivyo na tukafanikiwa kwa kiasi kikubwa. Mimi ninadhani Kilimo Kwanza na Mpango huu wa Sagon uende kwa Kanda, tugawanywe katika Kanda. Kanda nne, sita, vyovyote Serikali itakavyoona, lakini sisi Mkoa wa Dodoma ardhi yetu bado ni nzuri sana, tunachohitaji ni mbegu tu na zana za kilimo wala hatuhitaji pembejeo. Tunaweza tukafanya vizuri sana, ninaomba Mipango hii ambayo imepelekwa katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ienezwe Tanzania nzima, kwa sababu Kilimo Kwanza ni kwa Tanzania nzima, ambayo imezungumzwa katika Hotuba ya Waziri na Mikoa mingine bado inaonekana kilimo kipo chini kwa sababu wakulima bado wanatumia majembe ya mkono, bado wana mbegu zile za miezi sita ndiyo wavune. Ninadhani kwamba, tukiletewa mbegu za kisasa tunaweza tukafanya vizuri sana katika mazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze habari ya *CDA; CDA* ilianzishwa chini ya Azimio la Baraza la Mawaziri la Mwaka 1974 na ikapewa miaka kumi kuangalia Mamlaka inastawisha vippi Makao Makuu ya Dodoma. Ilipoanzishwa walijenga barabara, miundombinu, wakaweka bustani, wakajenga majumba, lakini tangu hapo kazi ya *CDA* haionekani kuridhisha sana kwa sababu ya pesa kidogo wanazopewa. *CDA* ina *engineers, architects*, ina fani nyingi kiasi kwamba, Serikali ikiwatumia vizuri, wanaweza wakafanya kazi nzuri ya kueleweka. Kinachonishangaza ni kwamba, *CDA* wana hati miliki ya miaka 99 kwa Mji wa Dodoma, lakini pamoja na hilo wana Vijiji, Vijiji vina hati. Ninaisihi Serikali yangu ione namna ya kufanya, *CDA* inamiliki hati ya miaka 99 na Vijiji vina hati miliki, inapotokea wanavijiji wamepata mwekezaji; wanafanyaje wakati miliki ipo kwa *CDA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kwamba, Serikali ikiamua kuhamia Dodoma inaweza. Iliamua kujenga *UDOM* kwa miaka mitano, baada ya miaka mitatu *UDOM* ilikamilika. Miaka ya nyuma waliamua kujenga nyumba mia tatu Kisasa, walijenga ndani ya miaka miwili nyumba mia tatu Kisasa ilitimia. Sioni sababu ya Serikali kutohamia Dodoma, wanaweza wakaamua Mifuko ya Pensheni kujenga nyumba za Serikali, Nyumba za Watumishi, Ofisi za Serikali na ikawezekana; kwa nini Mifuko isitumike kujenga nyumba za Watumishi wa Serikali na Wizara na Serikali ikahamia Dodoma? Ninaomba Serikali ifanye maamuzi mazito kuhamia Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo ya hospitali; kuna mgao wa shilingi milioni mbili na laki moja kwa kila Kituo cha Afya. Kituo cha Afya Dodoma, Makole, kina wagonjwa mia moja na hamsini na zaidi kwa siku, shilingi milioni 2.1 hazitoshi. Tuna upungufu na matatizo katika Hospitali yetu ya Bahi. Bahi ni Wilaya mpya, haina hata Kituo cha Afya, kuna zahanati iliyogeuzwa kuwa Kituo cha Afya, ninaomba Serikali iiangalie Wilaya ya Bahi kwa jicho la huruma. Tumeomba shilingi milioni nane kwa ajili ya ujenzi ya nyumba za watumishi na wanatakiwa kuhamia kule kesho na hakuna

nyumba za watumishi; ninaomba Serikali iwafikirie na itufikirie Wilaya ya Bahi kupata zile shilingi milioni mia nane tulizoomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yetu ya Mpwapwa kuna milima ya ajabu na pesa zinazotengwa kwa ajili ya barabara zinazopita milimani ni kidogo mno. Ninaisihi Serikali iongeze pesa kwa ajili ya barabara zinazopita milimani.

Barabara ya Wota – Lufu – Mangaliza – Mbuga, ukimpa mkandarasi ajenge, pesa unayopanga kwa ajili ya ujenzi; ni kazi kumpata mkandarasi kwa sababu milima ni mikali mno katika Wilaya yetu ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie pia kuhusu ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Tuliomba shilingi bilioni nane, tumepewa bilioni mbili na tukisema ni bilioni mbili kila mwaka, ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itachukua miaka minane au sita kabla ya kukamilika, tufikiriwe katika hilo.

Nizungumzie Barabara ya Dodoma – Babati, Serikali imetoa pesa kwa ajili ya ujenzi wa kilomita arobaini na nne tu kutoka Dodoma mpaka Mayamaya na kutoka Bonga hado Kondoa. Kilomita sitini na tisa hazijapangiwa pesa, ninaisihi Serikali yangu sikivu ione namna ya kukamilisha Barabara hiyo, ile Barabara ndiyo *Greet North Road*, lakini kuanzia Babati mpaka Iringa, barabara hiyo inatia aibu. Ninaiomba Serikali yangu sikivu itusikilize katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Felister Bura na hasa ulipozungumzia Milima ya Lufu, Mangaliza, Matonya na Mbuga kwamba, hela za Halmashauri hazitoshi. Ninakushukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa anafuatia Mheshimiwa Tizeba na Mheshimiwa Jerome Bwanausi ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIBEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Buchosa, kwa kunichagua mimi na kukichagua Chama cha Mapinduzi kusimamia maendeleo yao kwa miaka hii mitano. Ninaomba niwahakikishie kwamba, walilichagua jembe, jembe limeanza kulima, kwa hiyo, watarajie kuvuna vizuri kama walivyokuwa wamefanya uamuzi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kuushukuru sana Ubalozi wa Korea hapa nchini na Wananchi wa Korea kwa ujumla, kwa mchango mkubwa na msaada wanaotoa katika Kata mbili za Kisiwa cha Kome, kwa maana ya Kata ya Nyakasasa na Rugata. Kata hizo mbili sasa tumekaribia kuondoa maradhi yote ya minyoo na wiki hii Nchi ya Korea imegawa baiskeli kwa Viongozi wa ngazi zote za Vitongoji na Vijiji; tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri Mkuu na Timu yake, kwa mawasilisho mazuri. Nimesoma makabrasha yote, yapo maeneo machache ambayo ninaomba nitoe mchango wangu. Eneo la kwanza ni mchakato wa uchaguzi tulioupitia; takwimu zinaonesha kwamba, mahudhurio katika vituo karibu vyote nchini hayakuwa mazuri na utafiti wangu unaonesha hii inatokana na kasoro zilizojitokeza katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Ukiangalia Daftari lililotumika Mwaka 2005, lilifanyiwa mabadiliko kwa maana kwamba, wapiga kura waliorodheshwa kwa kufuata *alphabet* halafu wakawa *re-allocated* kwenye vituo vingine. Hili lilisababisha baadhi ya Wananchi kupangiwa vituo vya mbali sana kutoka maeneo yao ya makazi na kwa hiyo watu wa umri mkubwa wote walishindwa kwenda kutimiza haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi wao. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tume ya Uchaguzi irudi tena kwenye lile Daftari la Mwaka 2005, watu wapangwe katika vituo walivyojiandikisha mara ya kwanza wakati tunaanza kutengeneza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kwa sababu kwa vituo hivyo watakuwa wako karibu na vituo vya kupigia kura na siyo kama ilivyotokea mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la maendeleo; wapo wanaosema hawaoni kwa vipi uchumi unakua kwa asilimia saba, sita, ngapi, halafu katika mifuko ya wananchi hakuna pesa. Ninaomba niseme kidogo kwamba, ukuaji wa uchumi unatafsiriwa katika maeneo mengi, lakini kubwa zaidi ni huduma kwa jamii. Nchi yetu katika miaka hii kumi na saba ya mageuzi ya mfumo wa uchumi wetu, imepiga hatua kubwa sana katika kuboresha huduma za jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo shule, hospitali na barabara, sasa hawa wanaotaka uchumi u-*translate* kwa hela mifukoni tu, ninadhani wana matatizo tu warudishe kwenye nadharia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hesabu ndogo tu, tunalinganishwa na China kwamba, kwa nini Wachina mwaka 1963 tulikuwa na uchumi unaofanana, leo mwaka 2011 hatufanani; wao wamekuwa na uchumi mkubwa wa pili duniani. Sawa, mimi nina shilingi elfu kumi mfukoni, mwenzangu ana milioni kumi, hata kama ongezeko langu ni kwa asilimia saba na yeye ongezeko lake ni kwa asilimia moja, kwa uwiano huo yeye atakuwa ameongezekewa na hela maradafu kuliko mimi. Kwa hiyo, hatutarajiwi kwenda kwa *pace* inayofanana.

Marekani uchumi wake kwa *average* unakua asilimia 1.3, asilimia 2 na watajivuna sana, lakini bado *it is still the strongest world economy*, hawajatoka pale kwa miaka mingi tu. Kwa hiyo, hizi nadharia na ku-*take advantage* ya Wananchi wengi kutozijua ili kuwarubuni, kuwapeleka kwenye mawazo kwamba, hatupigi hatua ni uwongo. Ninaomba ndugu zangu Watanzania, tuwe macho sana na maneno ya namna hii, yanatufanya tusiwe na imani na Viongozi wa Serikali, jambo ambalo ni hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kelele kubwa ipo pia kwenye maliasili, Watanzania tunakaribia kuaminishwa kwamba, ukombozi wetu upo kwenye madini tu. Ninaomba niseme; kuna nchi chungu nzima duniani hazina hata gramu moja ya dhahabu, lakini

zimepiga maendeleo makubwa.  Dhahabu kitu gani kama huwezi ku-*add value* kwenye hiyo dhahabu?  Pamba kitu gani kama huwezi ku-*add value* kwenye hiyo pamba? Rwanda hapa panaposifiwa ooh! Wamewekeza kwingine kwenye akili, basi wamewekeza kwenye akili na tunaona wanavyopiga hatua, sasa wao wamediriki kusema wanafungulia milango kwa nchi yao, anayetaka kwenda kuajiriwa Rwanda aende, lakini na wao wana-*export brains.* Kwa hiyo, ninaamini madini yasitufunge kufikiri.

Jana mchangiaji mmoja alisema tupo kwenye chupa tunatafunana huko, lakini mimi ninasema mimi nipo nje ya boxi na kwenye hiyo chupa simo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuache ndugu zangu kushawishi Wananchi wa Tanzania kufikiria ndani ya boxi la madini. Nimezungumzia suala la ku-*add value* kwenye bidhaa zetu; juzi nilifadhaishwa sana na jambo lililotokea hapa Bungeni; tulikuwa tunapitisha Muswada wa Sheria ya Fedha, tukaomba *skill development levy* igawanywe kwa mgawanyo tofauti na ulivyokuwa umeletwa na Serikali, bahati mbaya sana katika mabishano yaliyotokea hapa ya utaratibu na kanuni, muda ukaisha na tulikuwa tume-*move schedule of amendment* kupitia kwa Mheshimiwa Makani, ambayo ingetaka asilimia inayobakizwa kwenye Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)* na asilimia inayopelekwa kwenye mkopo wa Vyuo Vikuu irekebishwe ili kutoa fedha zaidi kwa ajili ya ufundi stadi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote duniani zenye viwanda, hazikuanza na viwanda vikubwa, zilianza na *small and medium enterprises*, halafu zile zina *feed* kwenye viwanda vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa tunajielekeza vibaya, vijana wanakosa matumaini.  Fedha nyingi ikielekezwa kwenye kujenga ujuzi wa vijana, hata hiyo mitaji tunayosema waende wakachukue benki ndipo itakuwa na manufaa.  Leo Kijana wa Tanzania hana ujuzi wowote, ametoka Shule ya Msingi au kamaliza Kidato cha Nne, unamwambia nenda benki kakope pesa, akichukua milioni tano hizo anafanyia nini; au tunataka kujenga taifa la wachuuzi kwamba, vijana wote wa nchi hii sasa wawe wafanyabiashara wa kununua na kuuza; haiwezekani.  Nchi hii ni lazima i-*manufacture,* kuwe na *production,* ndipo tunaweza kupiga hatua ya kweli na uchumi wetu ukawa endelevu.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe utaratibu wa kupitisha Miswada baada ya muda kwisha kwa kutumia *guillotine* tuuangalie upya, kwa sababu mambo muhimu yanaweza yakaachwa kwa sababu tu ya muda.

Nizungumzie juu ya uhusiano wa maendeleo nchini.  Yapo maeneo yamepiga hatua kubwa, lakini yapo mengine hayajapiga hatua kubwa kwa sababu mbalimbali, lakini mojawapo ni Sheria Kandamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Na. 22 ya Uvuvi inanikera sana.  Sheria ile katika *regulation* zake imeweka kipengele cha wavuvi kulipia leseni za uvuvi, mwenye vyombo na nyavu analipa leseni na yule mtumishi aliyeajiriwa na yule tajiri naye

analipishwa leseni. Kibaya zaidi, leseni hiyo inalipiwa kwa dola. Dola siyo fedha halali kwa malipo ya Tanzania, lakini mvuvi wa huko Kisiwani Soswa anaambiwa alipe leseni yake kwa dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hitimisho tusikie kwamba, leseni hizo za wavuvi zimefutwa. Huu ni ukandamizaji, sijaona kibarua wa mkandarasi anaambiwa na yeye alipie leseni ya ukandarasi, lakini kibarua wa mvuvi anaambiwa alipie leseni. Nimesoma Mpango wa Maendeleo, Mwanza na hasa Buchosa, hatukuona chochote. Mheshimiwa Mwakyembe hapa kanijibu kwamba, niende Tanga kuiga Watu wa Tanga wanavyofanya kwenye *PMMR.* Sikubali. Siyo kazi ya Mbunge kuzunguka kwenye *corridors* za Wizara. Tunaomba sana na hili nipo tayari kutangaza mgogoro na Serikali kama Barabara ya Sengerema – Nyehunge – Nzera hadi Geita haitapata matengenezo makubwa na ya kukidhi kiwango cha magari kinachotumia barabara hii.

Mheshimiwa Rais, mara nyingi tu mtakumbuka kila aki-*refer* barabara mbovu, anazungumzia barabara hiyo ambako Mkuu wa Mkoa alitaka kukwepa kumpeleka kule; yeye akasema mimi ninakwenda kule. Inaonekana Serikali ipo kimya tu kama vile maneno haya ya Mkuu wa Nchi wao hawayasikii jamani. Sasa Watu wa Buchosa waje wote hapa Dodoma, hapana wamenituma mimi. Kwa hiyo, mimi ninasema kuwa hili tutatangaza mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo letu lina tabu sana, kuna visiwa zaidi ya ishirini havifikiki, watumishi wanagoma kwenda huko. Tunaomba sana ufanywe Mkakati Maalum wa kuwasomesha watu ambao wamekulia katika yale mazingira ili waweze kwenda kufanya kazi ya kuwahudumia Wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyikiti, ninaona muda unakwenda haraka; lipo suala la Mwanza. Nimesikia hapa kuna mpango wa kupunguza msongamano Dar es Salaam. Dar es Salaam ina msongamano, lakini Mwanza ina msongamano mkubwa pia. Hatua zichukuliwe haraka jamani, bora kuziba ufa kuliko kujenga ukuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, wapo watu wanadhani wapo juu ya Mamlaka ya Wananchi; Mbunge sijui nani? Wenzetu wa Arusha wamefikia mwafaka wa Madiwani, anachomoka Mheshimiwa anasema mimi simtambui. Wewe nani; wewe ni Diwani tu katika ile Halmashauri? Ninaomba sana tuheshimu viongozi wetu katika hii ngazi, wanayo *mandate* na wanazo akili timamu; kujifanya wewe bingwa haitusaidii. Kwetu kule Uzinza kuna kamsemo ndugu zangu kwamba, *wamtengelokulunga yahendela endoso hachubuau. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatafsiri kwa Kiswahili; kuna methali moja inasema: “Mgema akisifiwa sana tembo hulitia maji.” Tusijifanye tuna akili kuliko wengine. Wale Waheshimiwa pale Arusha wana kiu ya maendeleo, wameona mgogoro sasa basi; sasa wewe unatoka huku unasema hutambui! Mamlaka hayo kakupa nani? Tumesomewa wote hapa mamlaka ya Wabunge na mipaka yenu, tuwaache Wananchi wa Arusha waendelee na shughuli zao za maendeleo kama walivyojipangia wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamebezwa bezwa hapa sijui posho, sijui nini, misimamo ya vyama na kadhalika, bahati nzuri jana tukasikia kumbe posho imepewa majina mengine inaitwa Ujira wa Unyiha. Mungu awabariki sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pili, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake aliyotuwasilishia ya Makadirio na Matumizi na Mapato ya Wizara yake. Kabla sijaelekea kwenye Hotuba, ninaishukuru Serikali kwa juhudi kubwa inazozifanya hapa nchini katika sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Kwa hakika Wananchi wetu ni waelewa sana, wanajua tulichokifanya pamoja na propaganda zinazoendeshwa sasa tunapofikia miaka 50 kwamba, hakuna tulichokifanya. Kwa sisi wa Mikoa ya Kusini tuna kila sababu ya kuwapongeza Viongozi wetu wa Serikali, kwa jinsi walivyojenga Barabara ya Kusini na Daraja la Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watu wa Kusini walikuwa wanateseka sana, lakini hili siyo Kusini tu hata Mwanza, Musoma, Wananchi walikuwa wanapita Kenya kwenda Musoma. Nani anapita Kenya sasa? Kwa hiyo, yapo mambo mengi ambayo yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kwenye TAMISEMI. Kwanza, nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Mkuchika, Waziri wa TAMISEMI, anayemsaidia Waziri Mkuu. Wananchi wana uhakika na wana matumaini makubwa juu ya utendaji wake wa kazi. Nilitaka tu nianze kuelezea kuhusu ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni-*declare interest* kwamba, mimi nimeshawahi kuwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa kwa miaka mitano; mambo ya msingi ambayo kwenye ngazi ile yanatakiwa yafanyike kwanza Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema ni juu ya kuhakikisha wale Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji, wanapewa hadhi walau ya kukumbukwa kupata posho zitakazowasaidia katika utendaji wa kazi. Kazi za Wenyeviti hawa ni za mchana na usiku kwa lolote linalotokea katika eneo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, ninazipongeza juhudi zinazoendelea kufanywa na Wananchi juu ya ujenzi wa Ofisi za Vijiji na Mitaa, ningeomba Serikali iendelee kuwasaidia kuunga mkono juhudi hizi ili vijiji vyetu vya mitaa viwe na Ofisi ambayo anakaa Mwenyekiti pamoja na yule Afisa Mtendaji. Siyo hilo tu, ofisi na posho ni lazima liendane na vifaa. Sasa hivi lipo tatizo sana, ukienda kwenye Ofisi ya Serikali ya Mtaa, Mwananchi anaambiwa toa fedha ili ikanunuliwe karatasi; ni wajibu wa Serikali kupitia TAMISEMI na Halmashauri kuhakikisha kwamba, inapeleka vifaa kwenye maeneo hayo.

Suluhisho la hili ni kuhakikisha Halmashauri zinapeleka fedha kwenye ngazi ya Vijiji na Kata kama mwongozo unavyosema. Hili ni jambo muhimu sana. Niendelee

kwenye ngazi ya Kata; nako ni-*declare interest* kwamba, nilikuwa Diwani kwa miaka kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo pale kwenye Kata ukianzia Diwani ni utendaji wake, ambao uko katika mazingira magumu sana. Kweli kabisa ni wajibu wa Serikali sasa kuhakikisha kwamba, Waheshimiwa Madiwani wanapata mishahara sasa na siyo posho. *(Makofi)*

Yale yaliyoelezwa kwenye Bunge lililopita na Tume ya Lubeleje, yafanyiwe kazi. Ninajua Serikali ilianza kutekeleza kwa kupandisha kutoka elfu sitini kwenda laki moja na ishirini, pamoja na kwamba, ilikuwa ni ongezeko la asilimia 100. Lilikuwa ni asilimia 100, ambalo bado lilikuwa bado lipo chini sana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kwamba, mwaka huu basi kusiwe tena na Waheshimiwa Wabunge kupiga kelele ambazo hazina matokeo mwishoni. Kwa hiyo, Waziri Mkuu atakapojumuisha atoe mwelekeo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala la usafiri ninadhani lilikuwepo kwenye Tume ya Lubeleje, nalo ninadhani ni muhimu sana kutokana na jiografia ya Waheshimiwa Madiwani wanakofanyia kazi. Nikija kwenye ngazi ya Halmashauri, ambako nako ni-*declare interest* kwamba, nilikuwa Meya wa Temeke kwa miaka mitano pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika mfumo ulioko kwenye Halamshauri sasa hauwezi kukidhi Waheshimiwa Madiwani, kusimamia ipasavyo fedha za Serikali zinazopelekwa pale. Ninasema hili kwa sababu Mheshimiwa Diwani anahudumiwa kila kitu na Halmashauri, kwa maana Mkurugenzi na Wakuu wa Idara. Jambo hili linapelekea wakati mwingine kupata kigugumizi juu ya kuwakemea wale Wakurugenzi na Wakuu wa Idara, ambao hawafanyi kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa ninashauri, posho na maslahi ya Waheshimiwa Madiwani, zihudumiwe na Serikali Kuu, wao waende kutekeleza wajibu wao tu. Hili linaweza likawekewa Afisa mmoja kwenye ngazi ya Wilaya, ambaye fungu lile litapelekwa pale na Waheshimiwa Madiwani wakihudumiwa pale ili waingie kwenye Halmashauri kama tunavyoingia Wabunge kwenye Bunge. *(Makofi)*

Lipo lingine ambalo ni la msingi kwenye Halmashauri, nilitaka niseme kwamba, fedha nyingi sana kutoka Wizarani zinapelekwa kwenye Halmashauri, lakini Wizara hazifanyi *follow up* ya kujua fedha zao zilizopelekwa zimefanya kazi gani. Nilikuwa ninaomba Wizara ziunde Kurugenzi zitakazosimamia fedha hizi ili pamoja na Halmashauri kushughulikia, lakini wao wawe na kitengo cha ku-*monitor* fedha zinazopelekwa kule. Hii ingeweza kusaidia sana kuhakikisha kwamba, kunakuwa na usimamizi mzuri. *(Makofi)*

Kuhusu Wenyeviti na Mameya; kwa hakika hali ya utendaji kazi ya Wenyeviti wetu wa Halmashauri na Mameya bado siyo nzuri. Mameya wengi au Wenyeviti wengi ambao wanafanya vizuri, wanafanya kazi zile kama *Executive Mayor* ama *Executive*

*Chairman,* wakati sisi kwenye mfumo wetu hatuna *Executive Mayor* au *Executive Chairman.* Kwa hali hiyo basi; ni vizuri Serikali itazame huko tunakoelekea, kuwe na Mameya, Watendaji na Wenyeviti ili wawe na nguvu na Wakurugenzi wawe Wasaidizi wa kuwasaidia kazi. Kwa sababu sasa inaonekana *power* kubwa ipo kwa Wakurugenzi kuliko Mwenyekiti au Meya; jambo ambalo linaturudisha nyuma sana.

Sasa nije kwenye Jimbo langu la Lulindi. Nikianzia na afya; kwa kweli mimi ninaiomba Serikali, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa katika kujenga hizi zahanati, lakini ukienda sasa hivi, kwa mfano, kwenye Jimbo langu la Lulindi, zahanati nyingi zinafanya kazi kwa kiwango cha asilimia 20 au 30, hakuna dawa, hakuna watumishi. Malalamiko ni mengi sana. Kwa hiyo, ningeiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, ihakikishe kwamba, watumishi wanapatikana katika maeneo haya.

Kwenye Jimbo la Lulindi pia tunayo hospitali nzuri sana ya Lupaso; ni Kituo cha Afya. Kituo hiki cha Afya kilipata wafadhili kilijengwa vizuri, lakini kulikuwa na kazi ambazo Wizara ilikuwa imalizie ili kituo kile kianze; tangu mwaka 2006 hadi hivi sasa Wizara haijatekeleza. Hospitali ile au Kituo kile cha Afya, kitasaidia sana Wananchi wa Jimbo la Lulindi badala ya kwenda Hospitali ya Wilaya ya Masasi, ambapo mwendo ni mrefu sana. Ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Mponda, Waziri wa Afya, kwa kweli ni msikivu na anastahili pongezi. Ameshalichukua na ninaamini kabisa, litapata ufumbuzi katika Bajeti hii ya Mwaka 2011/2012.

Kuhusu suala la kilimo; tatizo kubwa la Wananchi wa Jimbo la Lulindi ni soko la mazao yao. Ninaishukuru Serikali, ninamshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda na Waziri wa Kilimo, kwa juhudi walizofanya kupatikana kwa soko la korosho lililo zuri kupitia stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Nilishangaa hapa kuna baadhi ya Wabunge wanasema stakabadhi ghalani siyo nzuri. Mimi ninasema waje kule Masasi na Lulindi, waige stakabadhi ghalani inavyofanya vizuri. Ninaomba mazao mengine aina ya kunde, kwa mfano, choroko, kunde, pamoja na mbaazi, yaingizwe kwenye stakabadhi ghalani. Mwaka huu bei ya choroko ilianzia shilingi 1,200, lakini sasa hivi bei ya choroko ni shilingi 400. Kwa hiyo, wafanyabiashara hawa hawana urafiki na wakulima wa hali ya chini. Ninaiomba Serikali ifanye maandalizi mapema ili msimu ujao mazao haya yaingizwe kwenye stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Kuhusu maji; bahati nzuri Jimbo la Lulindi ni tofauti na Majimbo mengine ambayo hayana vyanzo vya maji. Hapa tunavyo vyanzo vitatu vikubwa vya maji; kuna chanzo cha maji cha Chiwambo; chanzo cha maji cha Mkululu; na chanzo cha maji cha Mkwaya. Kinachohitajika hapa ni miundombinu tu ya kuyaondoa yale maji kutoka kwenye chanzo na kuyafikisha kwa Wananchi. Kwa hiyo, ninaamini Wizara ya Maji imeongezewa fedha, itaona umuhimu mkubwa wa kuhakikisha vyanzo hivi vinatumika vizuri ili kuwaondolea kero Wananchi. *(Makofi)*

Kuhusu madeni; Serikali haiwatendei vyema wafanyabiashara wadogo na wa kati, wanaofanya kazi na Serikali, kwenye kupeleka vifaa, wanacheleweshewa mno malipo yao na wengine wanafilisika. Kwa hiyo, Serikali ijitahidi sana kulipa madeni ya ndani ili wafanyabiashara wale wainuke. Kwa mtindo uliopo sasa, wengine wanaogopa hata kufanya kazi ya Serikali kwa sababu hawapati malipo yao kwa wakati. *(Makofi)*

Kuhusu elimu; ningeomba suala hili ni-*declare interest* kwamba na mimi nilikuwa mwalimu. Kwenye Serikali ya Awamu ya Pili, waliwahi kuanzisha kitu kinachoitwa *teaching allowance,* lakini baadaye ikaondolewa. Mimi ninaiomba Serikali, hata kama siyo asilimia 50, walipwe kiwango chochote kile kitakachowezekana, walimu wapewe *teaching allowance.* *(Makofi)*

Kuhusu suala la Vyuo Vikuu, pamoja na kweli kwamba upo mchezo unaoendelea kwenye vyuo vyetu; mimi nishirikiane na wenzangu waliozungumza, Serikali itoe tamko juu ya kuzuia siasa kuendeshwa vyuoni na maeneo ya taasisi zinazotoa elimu. Serikali pia iwe sikivu kwa matatizo yanayowakabili wanavyuo na wakati mwingine tunakwenda pale tunawaahidi kwamba, hili litafanyika, baada ya wiki mbili kwenye *notice board* inabandikwa jambo lile haliwezekani tena. Kwa hiyo, nilikuwa ninaiomba Serikali iwe makini kwenye kushughulikia masuala ya vijana wetu ili kuondokana na matatizo haya yanayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni wastaafu: Kwa hakika wastaafu wetu wapo katika hali mbaya sana. Kwanza, wanapata malipo madogo, lakini pia hawapati kwa wakati. Sasa wafanyakazi wengine wanawatazama, wanaona kwamba alaa kumbe ukistaafu maisha yenyewe ndiyo yale, wanakata tamaa. Kwa hiyo, tuwaongezee fedha wastaafu wetu angalau waishi vizuri na walipwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Ninakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Kwanza kabisa, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, *Allah Subhanahu Wataala*, anayeneemesha neema kubwa kubwa na neema ndogo ndogo. Ninamshukuru sana kwa kuniwezesha kusimama hapa, kuongea mbele ya Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Pili, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aliweza kuniteua mwaka 2008 nikaingia ndani ya Bunge hili la Jamhuri. Nikabebwa nikabebeka; unaambiwa ukibebwa shikilia; nimeshikilia na nimeweza kuingia awamu hii tena kwa kugombea. *(Makofi)*

Akina mama wa Chama cha Mapinduzi, ninawashukuru. Akina Mama wa Mkoa wa Tanga walinibeba, Akina Mama wa Baraza Kuu la UWT Taifa walinibeba; ninawashukuru, tutaendelea kufanya kazi pamoja kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Ninamshukuru sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mtoto wa Mkulima. Tulikuwa pamoja kwenye matatizo ya mauaji ya walemavu wa ngozi, alitusaidia akisaidiana na Mheshimiwa Rais. Rais mwenyewe ndiye aliyenituma na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, kimbizana na haya; yeye ametoa uchungu wake, kazi imefanywa na Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu, alikwenda Mikoa ya Kanda ya Ziwa, akanibeba na mimi akasema Al-Shaymaa twende tukapambane, tukaenda. Tumesimama kwenye majukwaa, tumetoa elimu kwa Watu wa Kanda ya Ziwa, kwa nini mnauwa albino; mnapata faida gani? Wanasema kiungo cha albino kinauzwa mamilioni ya pesa! Mbona mimi maskini kwetu sina uwezo wowote, ningekata hata vidole vya miguu ningeuza nipate utajiri! Wamewachinja watu.

Ninakushukuru sana Waziri Mkuu, tumezunguka Kanda ya Ziwa, tumeongea na Wananchi na nina matumaini makubwa, Wananchi wametuelewa kwa sababu hii hali imepungua. Japo nina mashaka kidogo, uwoga bado upo upo, lakini yamepungua na ikiwezekana yatakwisha kabisa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakushukuru sana na ninaomba Kanda ya Ziwa achaneni na mambo ya ushirikina, imani potofu haipo jamani; Al-Shaymaa niko Bungeni hapa mbona ninafanya kazi kama wengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tofauti gani kati ya Al-Shaymaa na mtu ambaye siyo wa rangi ya Al-Shaymaa? Wote tuko sawa. Bob Marley, aliimba wimbo jamani *Different Colours One Nation,* Rangi Tofauti lakini Wote Taifa Moja la Tanzania na wote ni Waafrika na kazi ninaifanya vizuri, sikosei wala siharibu. Kwa hiyo, wasione kwamba, albino ni kituko, ni aibu au balaa, siyo balaa! Nipo Al-Shaymaa hapa, ninafanya kazi; na Wananchi wa Lindi wamemchagua Barwany, ameingia tena humu ndani, kuna tofauti gani? Hakuna tofauti.

Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hilo na pia umechukua watoto wenye ulemavu wa ngozi unawatunza; ninakushukuru sana. Hiyo imeonesha ni jinsi gani ulivyo na imani. Mungu akubariki sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na mama watoto wako ambaye ana huruma, Mama Tunu Pinda, ana huruma sana, hiyo ninathibitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba niingie kwenye Hotuba, sifa nimeshazitoa.

Nimeisikiliza Hotuba kwa makini kabisa, nikasikiliza na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuchika, nimesikiliza nikasema hapana, ngoja nisome labda sikusikiliza vizuri; jamani nimefunua mpaka mwisho, nikasema labda kwenye masuala mtambuka tutatajwa watu wenye ulemavu, hakuna! Mpaka ninamaliza hakutajwa mlemavu jamani! Nikaenda kumsikiliza Mheshimiwa Mkuchika, nikasema nifunue kitabu, nikakuta ukurasa wa 17, walizungumzia kuna michezo ipo inafanyika Kibaha inaitwa UMITASHUMTA. Hii michezo imeshirikisha pia watu wenye ulemavu; kwa kweli hapo nimefarijika. Nikasema kumbe na wao wameshirikishwa kwenye michezo wanaweza na nikathibitisha nikaongea

na yule ambaye yuko kule kwenye michezo, akaniambia wapo watoto wenye uoni hafifu na watoto wenye mtindio wa ubongo wameshirikishwa; kwa hilo ninashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeangalia kwenye Hotuba sikuona wakitajwa watu wenye ulemavu! Jamani, watu wenye ulemavu wana hali ngumu ya maisha, wanahitaji wapewe kama wanavyopewa Watanzania wengine kiukamilifu. Huu ugumu wa maisha kwa mlemavu ni maradufu. Mlemavu ana hali ngumu jamani, nyote mnajua! Hakuna Mbunge humu ndani asiyekuwa na ndugu yake au jamaa yake mwenye ulemavu. Mnajua matatizo waliyonayo walemavu, maisha yao ni magumu.

Idadi ya walemavu sasa hivi kwa idadi ya 2002 ni milioni 3.4 na *data* hizi nilimwomba Waziri. Tuna walemavu 3,452,900; hii ni ya 2002; sasa hivi miaka mingapi imepita? Kuna idadi kubwa mno ni maradufu ya hiyo. Jamani kundi hili ni kubwa, wanapenda na wao wasikike wakitajwa humu. Kila anayesimama jamani hajamtaja mlemavu, jamani tajeni! Hamkosi hizi changamoto kwenye Majimbo yenu, wapo walemavu wanawafuateni! Tajeni, hawa wana changamoto kubwa sana. Hilo nimeona niliseme na kwa walemavu hawa nitakwenda nyanja hadi nyanja; ninaanza kwenye elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya elimu kuna fedha zinatolewa kwa ajili ya Elimu Maalum na ninafikiri TAMISEMI ndiyo inahusika. Fedha hizi zinatolewa zinapelekwa Halmashauri, zikienda Halmashauri zinapangiwa mipango, zinakaliwa vikao ndiyo zinakwenda kwenye hizo shule za elimu maalum. Mimi ninavyoona; ni kwa nini hela hizi zisiende moja kwa moja kwenye shule husika? Wapelekewe moja kwa moja kwenye wahusika, wapo wanajua wajipange vipi. Ulemavu yule mwenye ulemavu ndiyo anaujua machungu yake. Machungu ya ulemavu kama mimi hapa ni mlemavu wa ngozi, kwa sababu kuna watu wananiambia Al-Shaymaa una ulemavu gani? Mimi ni mlemavu wa ngozi, nina uoni hafifu, huo ni ulemavu! Hayo ni matatizo na ninajua ulemavu huo uko vipi kwa mimi mwenyewe; nikitembea juani; nikikaa saa mbili nikirudi humu ndani ya Bunge, hamtanitamani nitakavyokuwa nimeharibika na jua. Kwa hiyo, ninajua matatizo yaliyokuwa ndani ya ngozi yangu. Ulemavu anaujua mlemavu mwenyewe, kwa hiyo, fedha hizi zipelekwe moja kwa moja zisipite Halmashauri, zikifika Halmashauri vikao vingi, zipangiwe mipango, vikao vitatu, vinne, zinapangiwa mipango fedha hizi kwenda kwenye Elimu Maalum! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wa Elimu Maalum wana matatizo, wanafundisha kwenye mazingira magumu mno. Ufundishaji wa mtoto mwenye ulemavu siyo sawa na ufundishaji wa mtoto wa kawaida; ni tofauti. Ufundishaji wa mtoto mwenye ulemavu unatakiwa *extra*, utumie mtoto mmoja kwa mwalimu na walimu hawa wanafundisha kwenye mazingira magumu sana. Mimi nina mfano wa Walimu wa Shule ya Uhuru pale Dar es Salaam; wamenieleza matatizo yaliyopo, wanafundisha kwa sida sana. Mbali na hapo wamejisomesha wenyewe, wakaiomba Serikali basi turudishieni hela yetu tumejisomesha wenyewe tupeni hii hela, hawakulipwa! Hawa walimu ninawajua, ikiwezekana walipwe hela yao waliyojisomesha kwa faida ya nchi hii. Warudishiwe hizo hela ili wapate moyo; na mishahara yao iwe maradufu. Wana kazi ngumu jamani,

asilimia 30 zaidi ya walimu wa kawaida. Jamani, nina uchungu, inawezekana mimi nikazuwia shilingi kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wanaopata Elimu Maalum, wanapata matatizo kwenye hizi shule; kuna shule ambazo ni *inclusive*, wapo watoto wenye ulemavu na watoto wa kawaida; na kuna shule nyingine wapo watoto wenye ulemavu tupu, kama uoni hafifu wanawekwa pamoja na wenye ulemavu wa ngozi, kwa sababu *at least* uoni hafifu na kutokuona kabisa wanaendanaendana. Kuna shule Shinyanga inaitwa Ndala, kuna Shule ya Uhuru Shinyanga na kuna Buhangija Shinyanga; Mwanza kuna Misungwi, nimefika mimi mwenyewe pale, kuna Kigongo Ferry ipo huko huko Mwanza; Mbeya kuna Uyole, kuna Mwenge, kuna Hiji, kuna Pongwe Tanga; Kigoma kuna Kabanga Kigoma, nimefika mimi mwenyewe. Wazazi wanaacha shughuli za kulima, shughuli za kuendeleza maendeleo, wanaangalia watoto, wanawalinda watoto wao mwenye ulemavu wa ngozi, wanaogopa watachukuliwa na kuchinjwa. Kwa hiyo, wazazi wanaacha shughuli za maendeleo, wanakaa wanaangalia watoto wao, Kabanga nimekwenda mimi! Wallahi kengele inalia, sijamaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ajira; watu wenye ulemavu 0.7% ndiyo wenye ajira. Jamani, mbona wapo wenye elimu zao; wana *certificates* zao; kwa nini wasipewe ajira? Watu wenye ulemavu inatakiwa angalau 3% wapate ajira. Watu wana elimu zao, wapewe ajira, *disability is not inability,* kuwa na ulemavu siyo kutokuweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji; kwenye uwezeshaji jamani kupanga ni kuchagua. Makundi ya watu wenye ulemavu yakihamasishwa kujiunga pamoja, wajiunge pamoja, waelimishwe, wapewe pesa, wafanye miradi, wanaweza! Kupanga ni kuchagua, alisema Mwalimu Nyerere. Tujitahidi tuwaweke na wao, tuhakikishe wakishatoa bidhaa, tunazi-*promote* zile bidhaa, tununue sisi hata Wabunge wakituletea hapa tuzinunue tuwawezeshe; hali ngumu tuwa-*promote*. Kuna *NGOs* nyingi tu zimeanzishwa kusaidia walemavu, lakini mnapopata zile pesa msinunue viti kumi vya kuonesha mfano, hela nyingine unatia mfukoni! Toa pesa, fanya msaada hasa kwa watu wenye ulemavu. Unapata pesa za kutosha, fanya *value for money* wanasema kama sijakosea.

Unapata pesa, fanya mambo watu wapate, siyo kuweka *wheel chair* mbili, unanunua *sun screen* kumi unawapa walemavu wa ngozi kumi hizo hela nyingine unazitia mfukoni. Nunua vifaa wape wahusika, Serikali pamoja na ninyi Wadau mkisaidia tunasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaingia kwenye afya. Wizara ya Afya kuna Kitengo cha Ustawi wa Jamii. Ustawi wa Jamii, wanapewa pesa kidogo na watu wenye ulemavu kwenye Wizara ya Afya, mimi ninaona kwamba, haina nguvu sana. Tulipenda tuingie kwako Waziri Mkuu, lakini juzi nimesikia kwamba Wizara ina kazi nzito, sasa sijui tutapelekwa wapi *toba yarabi*! Tuliomba Wizara ya Afya, watununulie *sun screens* na *lotions,* kwa ajili ya walemavu wa ngozi, zikaenda zikanunuliwa *lotions* zisizotakiwa! Wangetushirikisha, tungenunua *lotions* zinazotakiwa, lakini zimenunuliwa *lotions* ambazo sizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miundombinu, nitazungumzia kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu. Kwenye masuala ya miundombinu, majengo siyo rafiki, majengo hayako rafiki, walemavu wanapata matatizo, wakifika kwenye majengo pengine wanataka kwenda ghorofa ya saba wanashindwa, kwa sababu hayako rafiki na walemavu wale. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara isikie hilo. Pia niliomba watu wenye ulemavu wawekewe alama za barabarani na nilitoa *documentation* yote, nilimkabidhi Mheshimiwa Kawambwa, alipokuwa Waziri wa Miundombinu; sijaona jibu lolote na sijui kama imeshafanyiwa kazi! Ninaomba lifanyiwe kazi suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba kusisitiza kuwa, walemavu ni wanadamu kama wanadamu wengine, wapewe kipaumbele. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakuomba, mimi nitaishikilia shilingi siku hiyo na nitasimama kuzuwia mshahara kama ikiwezekana. Kama sitakuwepo, anaweza kuwepo Mama Margareth Mkanga, akasimama hapa na yeye akapigia kelele angalau tutajwe. Tunajua Serikali yetu ni sikivu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, watatusikia walemavu, tuna kilio kikubwa mno Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naingia kwenye Halmashauri yangu; mimi nipo Halmashauri ya Muheza. Muheza kuna matatizo makubwa ya maji, kuna Mradi wa Mto Zigi unapeleka maji Tanga Mjini. Wana-Muheza wenyewe hawapati maji lakini Tanga Mjini wanapata. Tunaambiwa kwamba, kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwamba, tutapatiwa maji Wana-Muheza, tunaomba ahadi hiyo itekelezwe, lakini kwa dharura tumeambiwa tutapewa visima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana mwezi wa sita tulipewa milioni 50 kwa ajili ya visima vitatu vya maji; na huu ni mwezi wa sita, mwaka mmoja umeshapita, tunaomba vile visima vitatu vichimbwe.

Tuna matatizo ya maji, kijijini kwangu Mamboleo tuna kisima kimoja. Akina mama wanapata shida sana, wanatembea mwendo mrefu kutafuta maji na matatizo mengi yanawakuta. Akina mama ambao ni walemavu ndiyo wanapata shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesahau kuwatetea Madiwani; Madiwani waongezewe posho. Ninaunga mkono hoja, ninaomba siku ya mwisho walemavu watajwe kwa kina la sivyo nitasimama. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Timu yake, lakini niseme kwanza, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, Waheshimiwa Wabunge, wamechangia maeneo mengi vizuri sana na wametoa rai kwa Serikali, ku-*concentrate* na vipaumbele vichache vitakavyotuwezesha kutuvusha badala ya kuwa na vingi halafu vyote vikawa haviwezi kukidhi matakwa na matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianzie katika suala la elimu. Elimu ndiyo msingi wa maendeleo na mchango mzuri ni mchango mzuri tu hata kama unatoka kwa mtoto mdogo, bado utabakia kuwa ni mchango mzuri; au wazo zuri na wazo baya litakuwa baya tu hata kama linatoka kwa mtu mzima. Kuna mambo ambayo yanaendelea katika Vyuo vyetu Vyuo Vikuu, mimi mbali na kusema tu niunge mkono yanayojitokeza labda wanafunzi wamegoma, niseme haya gomeni, andamaneni, nimefanya utafiti, kwa sababu lengo langu ni kusaidia.

Mimi ni Mwakilishi wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, kwa hiyo, ninayozungumza ni yale ambayo yako sahihi. Bahati nzuri sikutaka niongelee jambo kwenye Ukumbi huu ambalo sijaziambia Wizara *inadvance.* Kwa hiyo, niliandika barua mapema ya kusudio la kutoa hoja ya kusema kwamba, Walimu wa Vyuo Vikuu, wana malimbikizo makubwa sana ya posho zao za nyumba; hapana haivumiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wale sasa hivi wanafundisha idadi kubwa kuliko ile ambayo ni ya kiwango cha Kimataifa, kinachostahili kutokana na matarajio yetu ya kutaka kuwa na wanafunzi wengi waliosoma katika kipindi hiki kifupi. Wanafanya kazi nzito sana, lakini posho zao karibu shilingi bilioni 9.5 hazijalipwa kwa muda mrefu, kwa takriban miaka mitatu. Ninayezungumza ni Mbunge kutoka CCM, ninaieleza Serikali yangu ili iweze kuondoa utata huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu anapokuwa anadai posho yake kwa muda mrefu, kwanza, anakuwa hana uhakika wa mazingira yake ya kupumzika na hata kufanya kazi za ziada za wanafunzi ambazo anazichukua. Haitoshi, mwalimu huyu akiingia darasani anakuwa yuko *frustrated,* akiwaona wanafunzi anaona kwake ni mzigo na wanafunzi wanamwamini mwalimu. Akikaa kidogo anawaambia aah, hiki chama hiki; akikaa kidogo, jamani Chama cha Mapinduzi, akikaa kidogo jamani mimi posho yangu; na wanafunzi wanamwamini nao wanaanza kujenga tabia za kugoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, kwanza, ninawashukuru sana Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, lakini pia Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, kwa sababu baada ya kuona hayo, nilifanya tafiti zangu zote kupitia Wizarani husika, nikasema nina hoja yangu inakuja na hakika nitatoa shilingi, hakuna utani; nikaambiwa kwamba, baada ya kuliona hilo, wamezingatia katika Bajeti hii; ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninalolihitaji ni moja; sina haja ya kurudia kutumia muda wa Bunge peke yangu kwamba ni lazima nilete tena hoja binafsi, sasa hivi ninaomba niyajumuishe hayo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakapojumuisha japo Wizara inayohusika bado haijafika, lakini nipewe ahadi kwamba, hawa watu angalau baada tu ya kupitishwa Bajeti, kipindi cha miezi mitatu wawe wamelipwa, kama itawezekana. Ninaomba nipewe ahadi hiyo kama kweli Bajeti hii imelenga hivyo na kama sivyo basi hoja yangu itaendelea kusimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi pia katika suala la wanafunzi, nimefanya pia utafiti nikasema shilingi 5,000 ambayo wanapewa kama mkopo wao wa posho; je, unawatosha au kuna tatizo gani? Nini kinasababisha kuwa na mgomo?

Nikasema pia kwa nini wanafunzi wamekuwa na kiu ya kuigomea Serikali badala ya kuanza kuwagomea wazazi wao kwa sababu mwenye mamlaka wa kwanza na wajibu wa kwanza ni mzazi. Niliyoyapata kutoka huko ni kwamba, zile posho zinachelewa kupelekwa na wale wanafunzi, baadhi yao, wanatumia kuwasaidia wadogo zao kutokana na hali halisi ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo maneno sijayatunga, nimefahamishwa na wanafunzi wenyewe kwamba, wao wanaona kwamba kupata zile hela ni kweli zinawatosha kula tu, lakini wakiangalia nyuma na wadogo zao wanahitaji kusoma na yeye unakuta wakati mwingine ndiyo aliyetangulia, anachukua angalau sehemu kusomesha wadogo au kusaidia wadogo zake kwenye familia na inapochelewa kutoka ile posho kama alivyojipangia sasa anajikuta hana kitu cha kula na akipita hapa yule anayewaambia haya sasa gomeni, inakuwa rahisi kwao kugoma ili waweze kusaidiwa kwa haraka. Lakini kitu kimoja katika utafiti uliofanyika inasemekana Tanzania ni nchi ya kwanza katika kusaidia wanafunzi wake kwenye mikopo, na ni jambo la kuipongeza sana Serikali yetu kwa kuona umuhimu huo hasa ikizingatiwa kwamba wanafunzi wale wasingesomeshwa sasa hivi hakika Taifa lilikuwa linaangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaumiza sana, angalia jiografia, fuata *statistics* za watu waliosoma katika nchi hii, ukabila siyo mzuri, lakini ukifuatilia utakuta kuna baadhi ya makabila yamesoma vizuri zaidi kuliko mengine kwa sababu mbalimbali. Nimefuatilia katika mkopo, mkopo ule siyo kweli unawafikia watoto wa maskini kama ambavyo inazungumzwa. Watoto wengi wa maskini ndiyo wanaosoma zile shule za Kata, ndiyo wale wako katika shule ambazo bado hazijawezeshwa vizuri, lakini wakati wa kuchagua *pass mark* ya kuendelea wao wanakuwa na *grade* za chini, matokeo yake wanakosa kabisa zile fursa. Nilikwenda Bodi ya Mikopo, nikasema wanipe jiografia ya jinsi gani mikopo hii imeweza kutawanywa katika nchi nzima ya Tanzania. Tusipoangalia kwa umakini, tutakuwa na sehemu za watu walioendelea na watwana katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo siyo kutafiti ukabila, lengo ni kutoa fursa sawa kwa wananchi wote wa Tanzania, kwanini nasema hayo? Ni hivi, siku za karibuni tu, tumepitisha Sheria ya Gharama za Uchaguzi na katika sheria ile inasema mtu haruhusiwi kwenda kuleta fujo au kuanza kujipitisha pitisha katika Jimbo la mwenzake, ni sheria tumetunga sisi wenyewe, msimamizi yuko wapi? Vyama vinapopita kwenye maeneo, badala ya kushukuru wanakwenda kuwatukana Wabunge waliopo, kwenda kumtukana Rais aliyepo, kwenda kusema wananchi wasijitolee, msimamizi wa sheria hii yuko wapi? Tuchukue hatua mkononi*? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halikubaliki hata kidogo. Mkoa wangu wa Ruvuma una deni, unawadai Chama cha Mapinduzi. Unaidai Serikali, kwa sababu hatua iliyochukuliwa kipindi cha kampeni za kuwaeleza kwamba tukifanikiwa kupita tutawafanyia hili na hili yatawezekana kama wananchi pamoja na Serikali watashirikiana.

Mtu anakwenda kuwaambia msifanye kazi, Dkt. Slaa namheshimu sana, namtaja kwa jina leo, anakwenda kwenye kijiji changu nimewahamasisha watu wafanye kazi anawaambia, msifanya kazi, anawaambia ninyi bwana mkisikia chakula kinanukia kimepikwa nyumbani kwa Manyanya, Rais gani huyo mchonganishi wa kuweza kuchaguliwa? Nani anakubali? Isitoshe anayemwita mchumba wake akaniandikia meseji chafu chafu ninazo na nina ushahidi, nikamwambia uliyeniandikia meseji hizi ni nani? Hakunijibu ikabidi nipitie kufuatilia katika mitandao nikakuta ni Josephine Emmanuel ni jina linalofanana na mchumba wake, namwambia sitaki kunichokoza, sitaki! Tupo kwa ajili ya kazi na asilete mambo yasiyofaa katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho wanazolipwa Wabunge na hizo tunazoziomba pia zipelekwe kwa Madiwani, zinaongeza demokrasia zinaongeza mtoto wa maskini na yeye kuweza kufanya kazi zake. Nani anataka kuwekwa mfukoni apitishe maamuzi yasiyo sahihi kwa sababu amegawiwa hela ya mafuta? Nani anataka kuwekwa mfukoni ili yeye kwa sababu amesaidiwa vijisenti vya kujikimu ndiyo aweze kufanya kazi yake? Hatukubali. Wanaosema hivyo wana sababu zao na hatutaziunga mkono, wote tuna haki sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi katika suala la Mahakama, huu uhuru wa Mahakama una matatizo. Uhuru wa Mahakama una matatizo nchi hii. Siku moja nilikwenda Mahakama ya Ardhi, nikakuta wanaolalamika na kulia ni maskini tu, wazee wasio na uwezo ndiyo walionyang'anywa mashamba, ndiyo wanaodai viwanja. Wale ambao wana uwezo, walionyang'anya, hawaonekani, wanatuma ma-*advocate.*

Naomba wakati wa kupitisha shughuli, Sheria hii ya Katiba Mpya, tutakapoiangalia, uhuru wa Mahakama lazima tuuangalie tuweze kuhoji Mahakama isiponitendea haki nafanya nini? Haiwezekani kesi moja idumu miaka 13 halafu tunasema kuna uhuru wa Mahakama. Sisi Wabunge na Serikali tunakutana hapa, Mahakama tunakutana nazo wapi? Lini jopo la majaji limekaa na sisi Wabunge angalau na Serikali kutueleza matatizo yaliyopo tukaelewana kwa pamoja? Hapana mhimili huu. Lazima tuangalie vizuri, ni mhimili mkuu wa dola yetu, hatuwezi kuangalia kila siku wale wakazi wako pale mji mpya Geita wako kwenye yale mahema mpaka leo kesi haiishi, halafu tunasema kuna uhuru wa Mahakama. Hapana, haiwezekani. *(Makofi)*

Wizara ya Ardhi, naomba mnifahamishe, Karatu, katika shule ya Weruweru ilikuwa inamegwa kwa ajili ya Madiwani wale wengi, wamekaa Chama cha upinzani pale wameanza tu na mambo yao, wamemega eneo la shule, shule inatakiwa ijengwe mabweni, shule iendelezwe nyumba za walimu, mnamega tena ardhi, nataka Wizara ya Ardhi inipe jibu kuhusu lile eneo limewekwa vipi sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuwa tunaifikia miaka 50 ya uhuru, huduma zisiwe mjini tu. Kijiji cha Kiagara huduma tunaipata mbali sana. Tumeamua kujenga hospitali na kuipa jina *Uhuru Gold Jubilee Health Centre*, tunaomba kwa heshima na taadhima, napiga magoti, wanawake wanaumia wanakwenda mbali, maiti zinabebwa kwenye pikipiki, Mheshimiwa Waziri Mkulo tunaomba utuangalie mtusaidie tupate Kituo cha Afya. Sisi wenyewe tuko tayari kutoa matofali 500,000, *NGOs,* taasisi zote

zinazojiusisha na mambo ya afya mtusaidie basi, iwe ni hospitali inayofanana, siyo tukiwa vijijini maana yake lazima tupewe vihospitali vya ajabu ajabu. Hebu tuonyeshe vijijini kunaweza kuwekwa vituo vya afya vyenye hadhi, kuna siku utakwenda ziara, Mheshimiwa Waziri Mkuu utaumia kule, matokeo yake utakuwa huna pa kutibiwa. Mawaziri mnazunguka kule, mtaumia, mtakuwa hamna pa kutibiwa. Tunaomba mtusaidie, tunaombeni sana. Twende mpaka Litembo, au Mbambabay, au Litui na mimi ndiye Mbunge wa kwanza kupatikana kijiji kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja tunazidi kuomba mtusaidie. *(Makofi)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji kwa siku ya leo. Awali ya yote na mimi pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na kwa mema yote ambayo ametujalia sote ambao tuko hapa pamoja na mambo mengi ambayo ameijalia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na mchango wangu, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa bajeti yake nzuri. Hotuba ni nzuri sana na imeeleweka. Kwa hiyo, nasema hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa jambo moja tu ni kuunga mkono hoja kwa nguvu zangu zote, asilimia 100. Miaka iliyopita tulikuwa miongoni mwa nchi 10 maskini zaidi duniani, lakini ni jambo moja la kujivunia kwamba sasa hatupo miongoni mwa hata zile nchi 20 maskini zaidi duniani. Ttuna haki ya kujivunia na kujipongeza kwa hatua hii ambayo tumefikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonyesha ni jinsi gani Chama cha Mapinduzi kina sera ambazo ni za kutimiza lengo la kuondoa umaskini, ujinga na maradhi na kwa sababu hii, basi na mimi nitajikita kwenye maeneo matatu tu, eneo la afya, eneo la elimu, na eneo la uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia upande wa afya, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara, napenda nichukue fursa hii kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutenga kiasi cha fedha kwa ajili ya maendeleo ya afya Mkoa wa Mtwara na hasa kwa kuanzia ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara na huu ni utekelezaji mzuri wa Ilaini ya Chama cha Mapinduzi. Lakini vilevile kuna mpango mzima wa kufanya ukarabati hospitali zetu za Mkoa wa Mtwara, Vituo vya Afya na *Dispensary*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, ni maendeleo mazuri na makubwa sana ya afya, lakini ningeomba niikumbushe Serikali jambo moja tu ambalo kidogo itakuwa imejisahau kwa upande wa hospitali ya Mkomahindu katika kutekeleza malengo ya milenia kwa upande wa afya ya mama na mtoto. Tuliwahi kufika kule na Mheshimiwa Hokororo hivi karibuni mwezi wa tano, hali inasikitisha kwenye wodi ya

akina mama. Akina mama tunadhalilika na hili lilitusikitisha sana na wananchi kwa ujumla hususan wanawake wanasikitika, wanalala watatu watatu kitandani wakati wa kujifungua na inalazimika sasa wawaache watoto peke yao pale kitandani, watatu wao walale chini. Hii inaturudisha nyuma, na sijui tutatekeleza vipi malengo haya ya afya ya mama na mtoto endapo tutasahau kupanua wodi za akina mama. Inawezekana siyo Mkomahindu peke yake, inaweza kwenda nchi nzima na ukakuta tatizo hili lipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuiomba Serikali ilitiliea mkazo suala hili, ipanue wodi ya Mkomahindu. Lakini pamoja na hili, kuna suala lingine ambalo tumelikuta kwenye wodi ili ya akina mama, hakuna *drip stand* za kutosha, hizi siyo zama za kutumia mianzi, lakini pale Mkomahindu, wanatumia *drip stand* za mianzi. Mimi nadhani tuangalie, mambo mengine siyo ya kuhitaji trilioni nane, mambo mengine ni madogo madogo yanahitaji tu usimamizi na ufuataliaji wa karibu. *(Makofi)*

Hata hivyo, kwa upande wa afya, zipo baadhi ya hospitali ambazo ukienda utakuta *operation* zinasitishwa au huduma za upasuaji zinasitishwa kwa sababu tu hakuna zile *gauze*, vile ni vitu vidogo sana lakini mtu anaweza akapoteza maisha kwa sababu tu kifaa hiki kimekosekana. Lakini baya zaidi, ukienda mawodini hospitali hiyo hiyo, unaweza kukuta hizi zinatumika kama ndiyo *handkerchief*. Inasikitisha na inatisha. Mimi nadhani hapa siyo suala la pesa, ni suala usimamizi mzuri. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Afya iwe makini kuzingatia sana kuhakikisha usimamizi mzuri unakuwepo mahospitalini na kwenye Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kidogo kuhusu elimu. Nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kujenga chuo kikubwa sana Afrika Mashariki na kati, Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefika pale nimekuta kweli Serikali ina azma ya kutimiza kutatua tatizo la upungufu au uhaba wa walimu katika nchi yetu, imejidhihirisha wazi kwamba kati ya wanafunzi takribani 20,000 wanafunzi 9,000 ni wale wanaochukua fani ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nichukue fursa hii kuwapongeza sana wanafunzi hawa 9,000 kwa fani ya elimu kwa sababu hii migomo tunayoisikia inazungumziwa hapa, hakuna mwanafunzi mmoja wa fani ya elimu ambaye aligoma. Tuwapongeze hawa kwa sababu hawa wanadhihirisha kwamba ni jinsi gani wanavyochukulia au wamelelewa katika maadili ya ualimu na tuna haki sana ya kujivunia kwamba siku chache zijazo au miaka mitatu ijayo tutakuwa na walimu 9,000 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ambao ni wazuri na waadilifu. Ninaomba tuwaunge mkono na naomba Serikali iwaenzi walimu hawa 9,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba nimetembelea pale, kuna tatizo moja ambalo nimeweza kuliona, ni uchache wa wanafunzi ambao wanachukua fani ya sayansi, na tukizingatia kwamba sasa hivi nchi yetu ina upungufu mkubwa sana wa walimu wa sayansi, mwaka wa tatu, wanafunzi wa sayansi ni chini ya 90 kati ya wale 9,000 wa mwaka wa tatu ambao sikujua idadi yake, lakini wanafunzi wa sayansi ni chini

ya 90. Lakini pamoja na hayo, tuna tatizo pia la walimu wa hesabu, lakini walimu wanaosoma hesabu pale ni wanafunzi 14 tu wa mwaka wa tatu, sasa ukichukulia tatizo kwamba wanafunzi wetu wa Kidato cha Nne anapokuwa amepata hata *division one*, lakini amefeli hesabu anapigwa *penalty* anashushwa mpaka *division three*, mwanafunzi huyu tunamsaidiaje kama hakuna walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani cha msingi hapa, tuzidi kuweka vivutio vya ziada kwa ajili ya walimu wa sayansi ili tupate wanafunzi wengi wanaosoma sayansi na tuweze kutatua tatizo la uhaba wa walimu wa sayansi. Labda kwa upande wa walimu au wanafunzi, niwaombe tu msiogope masomo ya sayansi na hesabu, siyo magumu kiasi hicho endapo mtu unajiamini. Sisi tulipokuwa katika Shule za Sekondari, tulikuwa tukifuatilia sana wenzetu wanafanya nini na waliokuwa wakishinda kwenda *Form Five.* Tulikuwa tunafurahi na tulikuwa tuna wimbo mmoja tulikuwa tunasema hivi: *"If cantie, can tie a tie, why can I tie a tie, as cantie, tie a tie?* Kwa tafsiri fupi, rahisi, kwamba kama mwenzangu anaweza, kwanini mimi nishindwe? Kwa hiyo, wanafunzi, wanangu wapendwa, kama mnanisikiliza, naomba msiogope sayansi, msiogope hesabu. Jiulizeni tu, kama wenzetu wanakwenda kusoma masomo haya, sisi kinachotushinda ni kitu gani? Kwani wao wana nini? Kwa hiyo, nawaomba acheni woga, mjiamini, mkasome sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie tu kidogo suala la uchumi. Kuna changamoto ambayo imejitokeza katika maeneo mbalimbali na hasa katika bajeti ya Serikali. Changamoto kubwa ambayo ilionekana ni kwamba uchumi wetu unakua sana, lakini kupungua kwa umaskini hakuna kasi ya kuridhisha. Kwa hiyo, nadhani hili linawezekana kutatuliwa endapo tutautekeleza vizuri ule mpango wetu wa miaka mitano ambao tumeletewa, ni mpango mzuri na nichukue nafasi hii kwa kweli kuipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao wanatutisha tisha, hapa wanasema mpango huu hauwezi kutekelezeka mpaka zipatikane trilioni nane. Hii siyo kweli kabisa kwa sababu ukirudi nyuma hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais anatuambia mpango huu hautatekelezeka endapo hakuna utawala bora. Lakini vilevile hata Tume yenyewe ya Mpango katika maelezo yake wanatuambia fedha au maliasili ni njia tu ya kutuwezesha kufikia malengo ya dira yetu, lakini cha msingi kikubwa Tume imetuambia ndani ya Mpango, kinachotakiwa ni ubunifu wa watunga sera na sekta binafsi katika kutumia fursa tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirudi tena kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na yeye anatumbia kwamba tunahitaji uwajibikaji, uadilifu, ubunifu, kufanya kazi kwa bidii, pamoja na kuwa makini. Haya ndiyo mambo ambayo ametuambia. Lakini hata ukifuatilia hotuba za Waheshimiwa Wabunge, wengi wamekuwa na wasiwasi kwamba utekelezaji unaweza ukawa mgumu kutokana na tabia zetu za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yamesemwa, lakini nilichokuwa naiomba Serikali ni kwamba sasa ihakikishe inaweka *mechanism* kuyafanya haya yawe ni ya lazima, siyo

ya hiari kwa sababu tukisema tunayaacha kuwa ya hiari tutaendelea kusema hivi hivi kila siku, lakini hakuna kitakachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunaambiwa nchi kama za Switzland, Hong Cong pamoja na Indonesia hawa hawana maliasili yoyote, lakini wao wameweza kuwa juu kiuchumi kutokana na kwamba wanatumia utawala wa kisheria. Hata hivyo, wameruhusu mazingira ya kibiashara na ndiyo maana wako juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kitu kidogo kuhusiana na kutokuwajibika. Kuna suala moja la umeme Mtwara, ilikuwa tupatiwe umeme wa Sh. 60,000/= kwa kuunganisha umeme kutoka msaada wa Holand wa fedha takribani shilingi bilioni 42. Lakini inasikitisha na wananchi wa Mtwara wanasikitika sana kwamba pesa hizi zimepotea na sasa watarudi kwenye shida ile ile ya kuunganishiwa umeme kwa bei ya juu, yaani Sh. 500,000/= kutoka *TANESCO* au zaidi na tatizo kubwa ni utendaji mbovu wa taasisi zetu za udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana hili liangaliwe ili makosa haya yasirudiwe tena siku za baadaye, shilingi bilioni 42 ni nyingi na ilikuwa ni fursa nzuri sana ya kuleta maendeleo ya kiuchumi Mkoani Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe mfano mwingine mzuri tu, kuhusiana na matumizi mazuri ya fursa tulizonazo. Ni suala la stakabadhi ghalani. Mkoa wa Mtwara umefanya vizuri sana mwaka uliopita kwa stakabadhi ghalani. Nimekuwa nikishangaa kwamba wengine wanasema huu utaratibu ufutwe. Lakini Mtwara tumepata manufaa makubwa sana kutokana na zao la korosho, tumeuza korosho kwa kilo zaidi ya Sh. 1,600/= na kutokana na ubunifu wa viongozi wetu wa Mkoa au Serikali ya Mkoa waliwaomba wananchi wachange kiasi fulani fulani kwa kilo, pesa ndogo tu lakini wakulima wote waliweza kuchanga zikapatikana shilingi bilioni tano...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anastazia James Wambura na sasa namwita Mheshimiwa Capt. Mstaafu John Chiligati na baadaye Dr. Seif Rashid ajiandae.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mkuchika kwa kutuletea hotuba ambayo ni ya utekelezaji wa mambo ambayo yanagusa maendeleo ya Watanzania moja kwa moja. Tunasema ahsante sana, tunaiunga mkono hotuba hii. *(Makofi)*

Pili, nawashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Manyoni Mashariki kwa kunichagua kwa mara ya tatu mfululizo kuwa Mbunge wao, najua ni heshima kubwa, ni deni kubwa na mimi ninaahidi kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kwa uadilifu mkubwa na unyenyekevu mkubwa. Nataka niwaeleze wananchi wa Manyoni ambao najua sasa hivi wananisikiliza kwamba uchaguzi umekwisha. Chama cha Mapinduzi kimeshinda vizuri bila mashaka yoyote. Kazi iliyobaki sasa hivi ni kutekeleza zile ahadi ambazo tulikuwa tunaahidi wakati wa kampeni. Ahadi zile nataka niwaeleze kwamba hazikuwa zangu binafsi kama Chiligati ila zilikuwa ni ahadi za Chama cha Mapinduzi kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tumeunda Serikali na ninataka niwahakikishie kwamba yale tuliyoyaahidi yatatekelezwa.

Kuna matatizo ya maji Manyoni, lakini nina hakika kabisa kwamba Serikali imejipanga vizuri kutekeleza miradi ya maji vijijini. Kule ambapo mradi umeanza, tutaendelea kuutekeleza kwenye maeneo ya Majili, Mpapa, Londoni, Lusilile, Kintinku na kote ambako kuna miradi ya maji wawe na hakika kabisa kwamba itatekelezwa. Pamoja na mradi wa maji mkubwa Manyoni Mjini, tulikuwa na tatizo kubwa sana la maji. Mradi mkubwa umeanzishwa na utaendelea. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia wananchi wa Manyoni Mjini kwamba ule mradi utaendelea, sasa hivi 80% ya wananchi wa Manyoni Mjini wanapata maji, lakini nataka iwe ni mia kwa mia ndivyo tulivyoahidi wakati wa uchaguzi na hayo yatatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna tatizo la barabara, napenda kwa niaba ya wananchi wa Manyoni kuishukuru Serikali kwamba barabara ya lami kutoka Dodoma kwenda Manyoni imekamilika na vilevile barabara ya lami kutoka Manyoni kwenda Singida imekamilika, ni lazima tushukuru. Sasa hivi ile ndoto ya kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza kwa *taxi* imekamilika, kutoka Dar es Salaam mpaka Ngara kwa *taxi* imekamilika. Ni mambo ambayo yako wazi kabisa na wale wanaosema Serikali haijafanya kitu, nasema kwamba washindwe na walegee, kwa sababu mambo yanaonekana. *(Makofi)*

Barabara ya zamani ilikuwa inapita Manyoni Mjini. Kuna kilio kwamba itengenezwe vilevile kwa kiwango cha lami, ni kama kilomita nne tu, wakati Waziri Mkuu anazindua barabara ya lami ya Dodoma - Manyoni alitoa ahadi kwamba na kale kabarabara kazamani kanakopita katikati ya mji na yenyewe itajengwa kwa lami.

Nataka niwaambie wananchi wa Manyoni kwamba ahadi ya Waziri Mkuu haikuwa ahadi hewa, ni lazima itatekelezwa na nadhani *comrade* Mwakyembe yuko hapa ananisikiliza. Ahadi ya Waziri Mkuu iko wazi lazima itatekelezwa. Wananchi wa Manyoni ahadi hizi ni za miaka mitano, maana wengine wanafikiri kwamba mwaka mmoja ahadi zote zitatekelezwa, hapana. Hizi ni ahadi za miaka mitano. Kuna mambo ya mwaka wa kwanza, mambo ya bajeti ya mwaka wa pili, mwaka wa tatu mpaka miaka mitano. Hii ni bajeti ya kwanza baadaya uchaguzi. Kwa hiyo, naomba Wananchi wa Manyoni wasiwe na wasiwasi, nasikia wengine wameanza kukata tamaa hata kabla mechi haijaanza, unakata tamaa, hapana. Hakuna kukata tamaa. Ile ni barabara ndogo, kama kilomita 1,500, Serikali ya CCM imetengenezwa kwa lami, kilomita nne haziwezi zikashindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna matatizo ya mambo ya afya. Nataka niwaeleze wananchi wa Manyoni kwamba zile ahadi ambazo tuliahidi kupitia mradi wa *MAM* zitatekelezwa, yale maeneo ambayo kuna shida ya zahanati tumeshajipanga na Madiwani tunajua mwaka wa kwanza zahanati ngapi tutazianzisha, mwaka wa pili na mwaka wa tatu. Lakini ninachoomba wananchi wa Manyoni, zile shughuli ambazo tunatakiwa tujitolee wenyewe, basi tujitolee, zile shughuli ambazo ni kubwa zinazotaka msaada wa Serikali, Serikali imetoa ahadi kwamba itatekeleza kwa kupitia mradi wa *MAM*. Vile vile Chuo cha Wauguzi cha Kilimatinde kilikuwa kinasuasua, lakini nataka niwaambie wananchi wa Manyoni kwamba kitaimarishwa ili na chenyewe kitoe mchango wa kufundisha Manesi wa kwenda kuhudumia Zahanati mpya zitakazojengwa kupitia Mpango wa *MAM*.

Namshukuru na Waziri wa Afya Dkt. Mponda kwamba *week end* hii atafika yeye mwenyewe pale Kilimatinde kuona chuo na ile hospitali ya Kilimatinde na kuona tutasaidianaje kati ya sisi wananchi wa Manyoni na Serikali yetu kuimarisha Chuo cha Manesi cha Kilimatinde. Mheshimiwa Waziri wa Afya Dkt. Mponda ahsante sana, tunakusubiri kwa hamu sana pale Kilimatinde na watu *Kilimatinde Hospital* tujiandae kumpokea Mheshimiwa Waziri ili tuweze kusaidiana kutekeleza mradi wa *MAM*.

Vile vile umeme vijijini kupitia *REA*, mradi umeanza kupeleka umeme kutoka Manyoni kupitia Solya, Kilimatinde mpaka Kintinku. Ni mradi ambao unaendelea, ninataka niwahakikishie wananchi wa Manyoni kwamba katika mwaka wa fedha ujao utakamilishwa. Tulishaomba mradi mwingine wa kwenda katika Tarafa ya Konko. Kwa hiyo, mambo haya yanakwenda vizuri wananchi wa Manyoni tunaomba tuendelee kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tuna ombi la siku nyingi la Wilaya mpya, Manyoni ni Wilaya kubwa sana, ina kilomita za mraba 28,000, jumlisha Burundi, Rwanda na kadhalika bado hawatufikii. Ni 51% ya eneo lote la Mkoa wa Singida. Tuliomba Wilaya tatu, tumeshapata mbili Mkoa wa Singida, tunaishukuru sana Serikali, basi kale kamoja kalikobaki hebu tumalizie ili Manyoni tupate Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha mambo ya Manyoni, nije kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika ukurasa wa tano wa hotuba anazungumzia habari ya maendeleo ya demokrasia ya Vyama Vingi nchini. Amesema kwamba demokrasia inakwenda vizuri, vyama vinafanya kazi vizuri na mambo yanakwenda vizuri, tunashukuru kwa hilo.

Pamoja na kwamba mambo yanakwenda vizuri, katika hii miaka 19 zimeanza kuonyesha dalili kwamba tunakiuka baadhi ya misingi ya kuendesha siasa ya vyama vingi. Tukikiuka hii misingi tutavurugana, utaratibu huu utatushinda. Moja ya msingi ambayo tumejiwekea na uko ndani ya sheria ni kwamba katika baadhi ya maeneo, tusiingize siasa za vyama vingi na sheria ipo. Jeshini hapana kuingiza habari ya siasa ya vyama vingi, maeneo ya kazi, viwandani, Mahakamani, maofisini na vyuoni, hapana kuingiza ushabiki wa vyama vingi. Tunaanza kuona dalili kwenye maeneo ambayo

tulikubaliana kwamba tusiingize ushabiki wa vyama vingi, kuna dalili za ushabiki.Kuna maeneo ambayo tulikubaliana kwamba tusiingize ushabiki wa siasa kwa sababu tutaharibu nchi. Wenzangu wamesema kwamba kwenye Vyuo Vikuu ni dhahiri kabisa sasa tumeruhusu ushabiki wa siasa kinyume cha sheria. Ni kosa la kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari za vyama kwenye vyuo imesababisha sasa kuwa na hekaheka za bendera ya Vyama vya Siasa, na watu wanavaa na *uniform* za vyama kwenye Vyuo, hapana. Wanasiasa tunakwenda kule, tunafanya Mikutano ndani ya *compass*, hapana! Kwa hiyo, tunaomba Serikali na ipo sheria, wenzangu wanasema itoe tamko, hapana! Tunasema sheria ifuatwe. Hawa wanavunja sheria na wanaharibu misingi ya mfumo wa vyama vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi mwingine ambao tunaanza kuuharibu ni vyama vingi vinataka kuvumiliana au *political tolerance,* yaani kuvumiliana na kuheshimiana na kukubali matokeo ya uchaguzi pale ambapo yameshatangazwa. Kuna baadhi ya wenzetu sasa hawataki kukubali matokeo, wanataka zile shamrashamra za wakati wa kampeni iwe ndiyo kipindi chote cha miaka mitano. Haiwezekani! Wakati wa kampeni za uchaguzi siasa huhamia mitaani, sasa ndiyo wakati wa maandamano na mikutano ya hadhara na vijembe, huo ni wakati wa kampeni. Nchi inachemka kipindi chote cha kampeni. Shughuli zinasimama wakati wa kampeni kwa sababu watu wote tuko barabarani, kwenye maandamano, mikutano ya hadhara na kadhalika. Lakini kampeni ikiisha na uchaguzi ukiisha mshindi akapatikana, mambo ya mitaani kule yanakwisha sasa, siasa zinahamia ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuendesha nchi kana kwamba kampeni zinaendelea, siyo sawa. Kampeni zimekwisha, sasa mambo yanakuwa ndani ya Bunge na siasa ndani ya Bunge, kule nje wananchi na nchi inatulia. Tulijigawa vipande vipande wakati wa kampeni za uchaguzi kila mtu na chama chake. Uchaguzi ukiisha tunaungana pamoja katika kujenga nchi na kufanya kazi. Kama tukiruhusu shughuli za kipindi cha kampeni kuendelea miaka mitano tutafanya kazi saa ngapi? Tutajenga nchi saa ngapi? Siyo sawa! Hii ni misingi ya vyama vingi, lazima tuiheshimu, vinginevyo tutapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ikiendelea kuwa ni nchi ya maandamano, tutakuwa hatufanyi kazii takuwa ni nchi ya ajabu tu, maandamano hayaishagi, tungoje miaka mitano kipindi cha uchaguzi kitakuja tena. Kwa hiyo, naomba sana haya wenzangu wanasema tushindane, Mbunge mmoja akasema sasa ninyi kama Chama hakiwezi kuingiza watu mitaani basi. Nasema hapana. Hatushindani sasa hivi kwa maandamano, bali tunashindana kufanya kazi na kujenga nchi yetu, ndiyo mashindano ya sasa, lakini siyo mashindano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo ni zuri ni kuhusu Baraza la Vyama vya Siasa. Ni chombo kizuri, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu mlitumie. Baraza hili linakusanya viongozi wa vyama vyote vya siasa, mnashauriana na kujenga undugu kama Watanzania. Chombo kile naomba sana Serikali ikitumie, ni chombo kizuri, kinatoa mashauri mbalimbali lakini sasa hivi bajeti yake ni finyu. Nimeona kwenye hotuba umesema utaliwezesha Baraza lifanye kazi, ni habari njema. Naomba mliwezeshe ili

mikutano ifanyike, na viongozi wa nchi hasa Waziri Mkuu na Rais mkutane na hilo Baraza mara kwa mara ili tuweze kulitumia lile Baraza vizuri, kwani linaleta mshikamano wa Vyama vya Siasa na ndiyo nchi yetu inaweza ikaendelea. Vipo vyama ambavyo havina wawakilishi hapa Bungeni, wanaviita vyama vidogo, lakini wenyewe wanasema hakuna chama kidogo wala kikubwa wote tumepata usajili, lakini vile vyama navyo naomba tuvitazame, vinapata taabu hata tu karatasi kuendesha shughuli zao haviwezi. Tuone jinsi gani Serikali inaweza kusaidia kwa sababu navyo vinarutubisha demokrasia ya Vyama Vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Madiwani, wenzangu wamewasema vizuri na mimi nataka niongeze kwamba hawa wanafanya kazi kubwa sana, ni vizuri tukaangalia maslahi yao, mafunzo ya Madiwani, Madiwani wakopeshwe vyombo vya usafiri ili wafanye kazi vizuri pamoja na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwasahau wastaafu kwenye *pension*, na sisi wote hapa ni wastaafu watarajiwa, wote tutastaafu. Sasa wastaafu kilio chao kikubwa kweli ni *pension* yao kwamba ni ndogo sana. Gharama za maisha zinapanda, lakini *pension* haipandi.

Naomba Serikali ya CCM kwa kuwa ni sikivu, wale wazee wamefanya kazi vizuri tuwakumbuke, tuwaongezee *pension* zao ili na wenyewe wakabiliane na hali ya maisha. Lakini vile vile na jinsi ya kuwalipa. Sasa hivi walipwa mara moja baada ya miezi sita, tuliangalie hili, wanalalamika wanadhani pengine tukiwalipa baada ya miezi mitatu tutawasaidia kwa sababu kipindi cha miezi sita ni kipindi kirefu sana, wengine hapa katikati hawana namna ya kuishi. Kwa hiyo, naomba sana hili suala la wastaafu Serikali ya CCM ni sikivu, hawa ndiyo wazee wetu wamefanya kazi kwa uaminifu, sasa wamestaafu tuwakumbuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa hotuba nzuri, lakini ni kweli kwamba wakati wa uchaguzi harakati zote mitaani, lakini baada ya uchaguzi na matokeo kutangazwa na mshindi kupatikana, mambo yote yahamie Bungeni ili mitaani watu wafanye kazi.

Sasa namwita Mheshimiwa Seif Seleman Rashid na Mheshimiwa Seleman Zedi ajiandae.

**MHE. DKT. SEIF S. RASHIDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi na pili kwa niaba ya wana Rufiji tunatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara yake kwa ujumla katika kuwasilisha hotuba ya bajeti kama tulivyoipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kushirikiana na wenzangu kwa kuunga mkono hoja. Lakini pia niipongeze Serikali katika hatua za maendeleo ambazo tayari ilishazionyesha kwa viashiria muhimu vya msingi. Kabla sijaanza kuyazungumza

yale ambayo Rufiji wanategemea niyazungumze, nitaje kwa uchache viashiria viwili ambavyo ni vya msingi vinavyoonyesha ukuaji wa maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uhuru kila watoto 1,000 waliokuwa wanazaliwa hai, watoto 167 walikuwa wanafariki. Lakini mwaka 2010 katika kila watoto 1,000 waliozaliwa hai ni watoto 81 tu ndiyo ambao wanafariki. Haya ni maendeleo ya kweli. Ukienda katika maendeleo ya msingi ambayo tulikuwa tukiambiwa vita za maadui watatu, katika kukabiliana na adui mmoja ujinga. Elimu ni kipaumbele na kwa hakika Serikali yetu imepiga hatua kubwa sana katika eneo hilo la elimu. Katika Wilaya ya Rufiji kwenye mwaka 2005 tulikuwa na Shule za Sekondari nane tu lakini mwaka 2010 tuna Shule za Sekondari 19. Kwa ujumla Tanzania tulikuwa na Shule za Sekondari zisizozidi 1,800 lakini mwaka 2010 tumekuwa na shule 4,100, hayo ni maendeleo ya kweli.

Pamoja na kupongeza jitihada za Serikali za kutuwezesha kuwa na mazingira mazuri ya kujileta maendeleo. Nianze kuzungumzia yale ambayo wenzangu Rufiji wanategemea niyaseme na hasa katika zile changamoto pamoja na kuishukuru Serikali katika kutekeleza mengi ya msingi ikiwemo ya barabara na Shule za Sekondari kama nilivyokwishazisema. Lakini hivi karibuni Serikali imetimiza azma yake ya kutupatia umeme na hasa imefikisha katika Makao Makuu ya Wilaya Utete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hili, naomba nizungumzie machache katika changamoto za uwekezaji na usambazaji wa umeme katika maeneo ya vijijini na maeneo ya Wilayani. Ya kwanza, gharama za uunganishwaji wa umeme kwa ujumla wake katika hali za maisha tulizokuwanazo na ukizingatia karibu 36% hadi 39% ya Watanzania kipato chetu hakizidi dola mbili kwa siku. Gharama zile ni kubwa na naomba Serikali itafute namna ya kuzipunguza gharama ili zimwezeshe mkulima kunufaika na usambazaji wa umeme unaondelea hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa maeneo ambayo umeme umepita katika mradi ule, Waziri Mkuu wetu alipokuwa akiuelezea unaoitwa *way river electrification project* kwamba kwa Wilaya ya Kilwa na Rufiji imeishakamilika. Mimi niseme, ukamilishaji wake ni wa hatua ya awali kwamba umeme umefika kwenye maeneo ya vijiji, lakini wengi bado hawajanufaika na uwepo wa umeme ule. Ni muhumi kuwa na mkakati wa kutosha kuweka nguzo za kusambaza umeme ili wakazi wengi katika vijiji ambavyo umeme ule umepitia uweze kuwafikia na wao waweze kuwa na nafasi ya kuunganishiwa katika majumba yao na maeneo yao ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa Wilaya ya Rufiji kuna vitu viwili ninavyoweza kuzungumzia kuhusu umeme. Kwanza ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni ambayo aliizungumzia kwamba katika vijiji vyote ambavyo umeme umepita, basi wasiwe watazamaji, isipokuwa na wenyewe wanufaike kwa kuunganishiwa umeme. Naiomba Serikali kutimiza ahadi hiyo, lakini vile vile naomba kwa vile umeme umeshapita pale Nyamwage, basi siyo mbaya ukaingia ndani kidogo kuweza kuvifikia vile vijiji vya Mbwala mpaka Nambunju.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kwa sababu umeme ule uko Ikwiriri na kwamba kuna vijiji 14 vilivyoungana pamoja vikielekea mpaka kule Mloka, naiomba Serikali kutimiza lengo la kuwafikishia umeme wakazi wengi na vijiji vingi vilivyokaa katika barabara moja iliyonyooka ya kutokea Ikwiriri hadi kufika Mloka ili vijiji hivyo viweze kunufaika na uwekezaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rufiji tuna changamoto ya barabara. Wakati wa kampeni, tulizungumza na tuliishauri Serikali kwamba, barabara ya kutokea Nyamwage kuja Utete na kutoka Utete kuja Kibiti, ni barabara mbadala ya barabara ya kutokea Kibiti kuelekea Nyamwage katika kuvuka mto Rufiji. Ni vyema Serikali ikaandaa barabara mbadala wa daraja lile la Mkapa, chochote kinaweza kutokea, basi tusije tukakosa kabisa njia ya kuvuka. Lazima tuwe na njia mbadala na njia mbadala ndiyo hiyo ya kutokea Nyamwage kuja Utete na kutoka Utete kuelekea Kibiti.

Pamoja na kuishukuru Serikali kwamba imeweza kutimiza azma ya kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe, lakini vile vile naishukuru kwamba imewezesha kuwekwa boti. Naiomba ipeleke tena macho yake katika eneo hilo la boti, eneo la ujenzi ule wa gati kwa hakika bado haujawasaidia watu wa Rufiji na watu wanaovuka pale kwa sababu boti hilo linafanya kazi kwa msimu na mara nyingine halifanyi kazi hata mwezi, miezi miwili na kwa namna nyingine tunaweza tukasema bado halijawasaidia wananchi wa Rufiji na watu ambao wanavuka kwa kutumia njia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto ya barabara kutokea Ikwiriri mpaka Mloka, barabara ambayo Mheshimiwa Rais pia aliitolea ahadi kwamba itatengenezwa kwa kiwango cha changarawe, lakini vilevile itaunganishwa kutokea Mloka kwenda Vikumburu na kuunganishwa na Kisarawe. Mimi nimeiona katika Mpango lakini kwa Mpango ambao ulikuweko kwa bajeti ambayo inakwisha mwezi huu wa sita. Barabara ile ilitajwa kwa jina, lakini hakuna hata senti tano ambayo ilitengewa. Naishauri Serikali kuweza kuharakisha ili barabara hiyo iweze kutengenezwa na iweze kuwasaidia wananchi wa Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwa haraka juu ya ufugaji ndani ya Bonde la Mto Rufiji. Kwa hakika suala la ufugaji ni zuri na Wanarufiji tunawapenda wafugaji, lakini ni suala la msingi kwa wale wote wenye kutakia mema maendeleo ya nchi hii kwamba ufugaji usifanyike ndani ya Bonde la Mto Rufiji, bali ufanyike nje ya bonde hilo na hao wafugaji waweze kuwekewa mazingira mazuri na Serikali kama ilivyokuwa imeahidi na kama vile ambavyo ilishaanza kuwatekelezea. Lakini ni wajibu wa Serikali kudhibiti ufugaji ndani ya Mto Rufiji kwa sababu ya kuhatarisha mazingira na kupoteza vyanzo vile vya maji na kuhatarisha mazao ambayo yanaweza kupatikana kwa kilimo katika Bonde hilo ambalo linaweza likaharibiwa na rutuba yake kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie namna ya kuweza kuisaidia Rufiji kukabiliana na mmomonyoko wa mto Muhoro, ambao unaelekea kula kijiji, unakula nyumba kadhaa kwa upande mmoja na kwa upande wa pili unahatarisha uwepo wa Kituo cha Afya cha Muhoro, kwani ule mmomonyoko unaendelea kula ardhi na kwa hiyo, unaweza kukifikia Kituo cha Afya nacho kikaingia mtoni. Gharama za kuudhibiti

ule mto ni kubwa sana, naiomba Serikali iangalie kwa makini namna ambavyo inaweza kusaidia kuzuia mmomonyoko ambao unaendelea kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie upesi upesi kwamba hali ya kilimo, hali ya chakula kwa Wilaya ya Rufuji, naweza nikasema ni mbaya kutokana na mambo kadhaa ambayo yalitokea na mengine yalishazungumzwa katika Bunge hili kwamba, mvua za vuli zilichelewa sana na kwa maeneo ya Rufuji hazikupatikana vizuri. Lakini vile vile hata baada ya mvua kuanza, wakulima walipata tatizo la wanyama pamoja na panya, panzi na wanyama waharibifu, wanyamapori na mvua ziliponyesha kwa wingi vile vile Bonde la Mto Rufiji lilimwaga kidogo maji likaathiri wale wote ambao walilima katika maeneo ya bonde na kwa hiyo, wakulima wengi hawakupata kipato kama walivyokuwa wamewekeza. Hivyo naiomba Serikali iangalie namna ya kuwasaidia wale wote walioathirika na majanga haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, ni Mradi wa Uendelezaji wa Bonde la Rufiji *(RUBADA)* ni mzuri na mimi nauunga mkono na Wanarufiji pia wanauunga mkono, lakini nina ushauri ufuatao: kwanza, ni kwamba wawekezaji wa *RUBADA* wahakikishe kwamba wanawaendeleza wakulima wale ambao wako pale kwa kuwawekea miundombinu na siyo kuwaondoa kuwapeleka katika vijiji vingine au mbali na pale ambapo wanaishi. Vilevile uwezo wao lazima uwe unapewa kipaumbele kwamba mkulima ambaye leo anaweza kulima ekari mbili, maanake ni kwamba akiendelea mwakani anaweza akalima ekari tno na mwaka unaofuata anaweza akalima ekari 10. Fursa hiyo iwepo na siyo kuwekewa vizingiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kwamba tuwe waangalifu katika kuwapa ardhi wawekezaji, kuwapa eneo kubwa ambalo wanaweza kumiliki kwa kipindi kirefu. Mimi nashauri uwekezaji huu uwe wa muda maalum ambao wanakijiji wale na Watanzania kwa ujumla watahakikishiwa uwepo wa maeneo yale baada ya kipindi fulani kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie mambo ya mwisho mawili. Kwanza, naiomba Serikali kwamba tuna maendeleo makubwa ya kiteknolojia, *TEKNOHAMA* imekuwa zaidi, mawasiliano yamekuwa zaidi na kwa namna hiyo inatakiwa yatumiwe kwa busara katika kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali ili iweze kuwekeza fedha za kutosha katika maeneo ya maendeleo. Kwa namna hiyo, badala ya Mkoa wa Pwani kupata shilingi bilioni 22 ambazo tumepata mwaka huu kwa ajili ya maendeleo, ingeweza kupata zaidi kama gharama za uendeshaji wa Serikali zingeweza kupunguzwa kwa upande mwingine wa shilingi katika kuhakikisha kwamba wanatumia fursa za mawasiliano zilizopo na kuweza kuzitumia kwa umakini katika usimamizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie na kuiomba Serikali kuendelea na juhudi zake za kupunguza uhaba wa watumishi katika maeneo yetu wakiwemo walimu, maafisa afya, wataalam katika ngazi hiyo ya afya, lakini pia na katika maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kusimama katika Bunge hili Tukufu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la mwezi Februari, nilisimama hapa kuelezea uwezekano mkubwa wa kutokea tatizo kubwa la njaa katika Jimbo la Bukene na Wilaya nzima ya Nzega, kutokana na hali halisi ya mavuno mabaya ambayo ilikuwa inajionyesha katika kipindi hicho. Napenda nitumie fursa hii kuipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, kwa namna ilivyoitikia kilio hiki kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, kwa maana ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa, imeidhinisha tani 3,900 za mahindi kwa ajili ya Jimbo la Bukene na Wilaya nzima ya Nzega. Sasa hivi ninavyoongea hapa, tani hizi 3,900 za mahindi zimeshaanza kubebwa kutoka maghala ya Hifadhi ya Chakula ya Shinyanga, kuelekea katika Kata mbalimbali za Jimbo la Bukene na Wilaya nzima ya Nzega, tayari kwa kusambazwa ili kukabiliana na makali ya njaa ambayo yanatukabili Jimbo la Bukene na Wilaya ya Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuitikia kwa haraka kuliko nilivyotegemea, lakini angalizo dogo katika jambo hili ni kwamba kutokana na ukubwa wa Wwilaya ya Nzega, idadi ya watu wa Wilaya ya Nzega na hali mbaya ya mavuno ambayo mwaka huu imetukabili Wilaya nzima ya Nzega, likiwemo Jimbo la Bukene, hizi tani 3,900 pamoja na kwamba zitapunguza makali ya njaa, lakini nina uhakika hazitatosha. Kwa hiyo, naitahadharisha tena Serikali kwamba kwa *spirit* hiyo hiyo iliyoionesha baada ya kilio changu cha mwezi wa pili, kuitikia na kutupatia tani 3,900 iwe tayari wakati wowote hali hii inaweza ikajitokeza tena na wananchi wa Bukene na Nzega tukahitaji tena msaada huo. Kwa hiyo, uharaka wa Serikali nauomba uwe kama ambavyo umekuwa kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Nishati ya Umeme. Jimbo la Bukene tumesubiri nishati ya umeme kwa kipindi kirefu sana. Jimbo la Bukene, kwa kipindi kirefu tumeachwa nyuma kwa maana ya kutokuwa na shughuli za uzalishaji kutokana na kukosa nishati ya umeme ambayo ni muhimu sana katika kuwezesha shughuli mbalimbali za uzalishaji zifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kwa mara nyingine tena kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Jimbo la Bukene cha kuisubiri kwa hamu nishati ya umeme, safari hii kuna kila dalili kwamba kilio hiki sasa kinafanyiwa kazi ipasavyo. Sasa hivi ninavyoongea, kuna mradi mkubwa ambao unatekelezwa na *Rural Energy Agency (REA)* kuvuta *line* ya umeme ya kilomita 42 ambayo itafikisha umeme Makao Makuu ya Jimbo katika Mji wa Bukene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ambayo ina mvua nzuri, wananchi wa Bukene tunalima mpunga kwa wingi sana, lakini miaka yote mpunga huu umekuwa ukienda kukobolewa nje ya Jimbo la Bukene na hivyo kuwafanya wananchi wa Jimbo la Bukene kuuza mpunga badala ya mchele.

Sasa kutokana na jitihada hizi za Serikali za kusikia kilio cha wananchi wa Bukene za kuleta nishati ya umeme katika Jimbo la Bukene, ambao utekelezaji umeanza na kama mpango utakwenda kama ulivyo, ni mategemeo yetu kwamba, mwezi wa Desemba au Januari, nishati ya umeme itakuwa imefika katika Makao Makuu ya Jimbo kwa maana ya Mji wa Bukene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Bukene tumeshajipanga kwa maana ya kuhakikisha kwamba nishati hiyo ya umeme tunaitumia kikamilifu kuhakikisha inatumika katika kuendesha shughuli za kuzalisha mali. Shughuli kubwa ambayo umeme huu utatumika ni kuendesha mashine kubwa za kukoboa mpunga. Kama nilivyosema, Bukene tunalima sana mpunga na sasa hivi wananchi wa Jimbo la Bukene badala ya kuuza mpunga sasa watauongezea thamani, watauza mchele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Bukene tunalima alizeti, kwa hiyo, kupatikana kwa nishati ya umeme kutawezesha wananchi wa Jimbo la Bukene kuwa na mashine za kusindika mafuta ya alizeti na hivyo, badala ya kuuza alizeti, sasa wataiongezea thamani na kuuza mafuta ya alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Bukene bado lina maeneo mengi ambayo yana miti mizuri, kwa hiyo, sasa hivi baada ya nishati ya umeme kupatikana, wananchi wa Jimbo la Bukene badala ya kuuza magogo, watayaongezea thamani na kuuza mbao nzuri zilizorandwa na mazao mengine ya mbao. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa jitihada hizi safari hii kuhakikisha sasa hadithi ya umeme kuja Bukene inafikia mwisho, umeme unapatikana, shughuli za maendeleo Bukene zinaanza kuonekana na kasi ya maendeleo inakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lingine la mabwawa ya umwagiliaji. Tumeona katika mpango, tumeona katika bajeti jitihada za Serikali za kuongeza kilimo hasa cha umwagiliaji. Jimbo la Bukene tuna matatizo ya kutokuwa na mtawanyiko mzuri wa mvua, kwa hiyo jambo ambalo litatuokoa ni kuwa na mabwawa ambayo yataweza kuvuna maji ambayo yatatumika sasa kumwagilia mashamba na mabonde mazuri ya mpunga tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa hivi tuna mabwawa matatu ambayo bado hayajafikia hatua ya mwisho ya kuanza kutumika. Kuna bwawa la Kamahalanga ambalo limechimbwa, limekamilika na ambalo Serikali ilitumia shilingi milioni 800 kulikamilisha. Lakini bwawa hili bado halijaweza kufanya kazi kwa sababu linahitaji kuwekewa mifereji na miundombinu itakayosababisha maji sasa yaanze kutumika mashambani. Kuna bwawa la Nindo ambalo linahitaji shilingi milioni 500 na kuna bwawa la Mambali ambalo linahitaji shilingi milioni 334.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kwa kupitia Wizara ya Maji ihakikishe mabwawa haya yanakamilika ili mabonde mazuri ya mpunga katika Jimbo la Bukene yaweze kutumika kuzalisha tani nyingi za kutosha za mpunga na hivyo kusaidia kuondoa umaskini katika wananchi wa Jimbo la Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mradi wa maji. Wilaya ya Nzega ina mradi wa maji unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Kuna vijiji kumi virefu ambavyo vinapaswa kuchimbiwa. Nilikuwa naiomba Serikali kwamba, hivi visima virefu kumi safari hii vifike mwisho. Vimezungumzwa muda mrefu, wananchi wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu, lakini bila miradi hii kufika mwisho. Vijiji ambavyo viko katika Mpango wa kufadhiliwa visima virefu na Benki ya Dunia ni Kijiji cha Itobo, Nawa, Sigili, Mahene, Buhondo na Ikindwa. Wananchi wa Vijiji hivi wanasubiri kwa hamu visima hivyo virefu ili viwawezeshe kuondokana na shida kubwa ya maji ambayo sasa hivi inawakabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la elimu. Kiwango cha ufaulu katika Shule za Sekondari zilizoko katika jimbo la Bukene na wilaya nzima ya Nzega hakiridhishi, kiko chini sana. Mojawapo ya sababu kubwa ni upungufu mkubwa wa walimu. Wilaya nzima ya Nzega ambayo ina shule 42 ina mahitaji ya walimu 1,058 lakini walimu waliopo sasa ni 343 tu.

Kwa hiyo, tuna upungufu mkubwa wa Walimu 715 na upungufu huu uko zaidi katika masomo ya msingi kama somo la Hisabati. Mahitaji ya Walimu wa Hisabati katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ni Walimu 119 lakini sasa hivi tuna Walimu 18 tu, kwa hiyo, tuna upungufu wa Walimu 101. Kama ilivyosemwa, Hisabati ni somo la msingi, ni somo muhimu sana ambalo ukifeli linasababisha *grade* yako kushuka, naiomba Serikali iizingatie Halmashauri ya Wilaya ya Nzega inapotoa mgao wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lingine, kuna watu wanalalamika kuhusu bajeti tegemezi kwamba bajeti ya Serikali yetu ni tegemezi lakini niseme tu kwamba njia pekee ya kuondokana na bajeti tegemezi ni kuimarisha makusanyo ya ndani, ni kuimarisha mapato makubwa ya ndani na hili ni moja kati ya eneo ambalo Serikali ya Chama cha Mapinduzi inapaswa kupongezwa. Takwimu zinatuonesha kwamba kumekuwa na ongezeko la makusanyo ya ndani, kumekuwa na *positive trend.* Ukiangalia mwaka 2008, wastani wa makusanyo ya ndani kwa mwezi ilikuwa ni shilingi bilioni 357. Mwaka 2009 kutokana na jitihada za Serikali ya Chama cha Mapinduzi wastani huo kwa mwezi ukapanda mpaka shilingi bilioni 388, miezi tisa iliyopita wastani wa makusanyo ya ndani kwa mwezi ni shilingi bilioni 470. Utaona kwamba kuna juhudi za makusudi za kuongeza makusanyo ya ndani na ambayo yakiimarika ndiyo yatafanya tusiwe na bajeti tegemezi. Kwa hiyo, wale wanaolalamika napenda kuwaambia kwamba wapongeze kwanza juhudi za Serikali za kuongeza na kukuza makusanyo ya ndani kwa sababu ndio njia pekee ya kuondokana na bajeti tegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nakushukuru wewe, namshukuru sana Mwenyezi Mungu *Subhaana Wataalah***,** kwa kupata nafasi hii kwa mara ya kwanza kabisa nizungumze katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo kwako na kwa Mwenyezi Mungu, pili, niwashukuru sana wapigakura wote wa Jimbo la Kondoa Kusini na Kondoa kwa ujumla kwa kuniamini na kunichagua kwenye uchaguzi uliopita na kuingia katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishukuru sana familia yangu, mama watoto wangu Amina na wanangu Kasi na Kimo kwa msaada mkubwa walionipa na hata nilipoacha kazi Marekani na wao walikubali kuja nyumbani kuungana na mimi kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Kondoa Kusini. Waliungana na mimi kwenye maamuzi magumu lakini lengo kubwa lilikuwa ni kuwatumikia wazee, vijana na kinamama wa Wilaya ya Kondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, niwashukuru sana Waandishi wa Habari wenzangu, Watanzania na wale ambao wanafanya kazi kwenye vyombo vingine vya habari duniani kwa msaada mkubwa walionipa wakati wa kampeni. Kwa heshima kubwa sana, nimshukuru Mkuu wa *Voice of America* Bwana Mwamoyo Hamza, kwa msaada mkubwa alionipa na hata nilipoomba kibali cha kuacha kazi, alisimamia kwa dhati na kuruhusiwa kurejea nyumbani, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi sasa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, nianze na kilimo. Wananchi wa Jimbo la Kondoa Kusini ni wakulima wazuri na mara hii kuna dalili huenda tukavuna mazao kupita kiasi. Yapo baadhi tu ya maeneo kama ya Tarafa za Farkwa na Kwamtoro yanaweza kukabiliwa na upungufu lakini naamini Serikali hii ni sikivu, tatizo hili litakwisha kama mengine yalivyomalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye kilimo tuna tatizo moja kubwa sana. Upo mgogoro wa muda mrefu kati ya Kiteto na Kondoa. Mbunge aliyemaliza muda wake amelisemea sana jambo hili na mimi itakuwa si dhambi kulisemea kwa mara nyingine. Wapo wakulima 72 walinyang’anywa mashamba yao, Mheshimiwa Waziri Mkuu anafahamu jambo hili na hata Mheshimiwa Rais alipokuja Kondoa wakati wa Kampeni alilizungumzia jambo hili kwamba tatizo la mpaka uliopo kati ya Kiteto na Kondoa sisi sote ni Watanzania, watu wa Kiteto wanaleta mifugo yao kutafuta maji Wilaya ya Kondoa na sisi tunakwenda kulima kwao dhambi ipo wapi? Kikubwa, naomba jambo hili litafutiwe ufumbuzi ili wananchi hao waishi kwa amani. Vimetokea vifo kadhaa lakini naamini sasa Serikali hii sikivu ya Chama cha Mapinduzi itatafuta suluhu ya kudumu ya jambo hili. Mimi na Mheshimiwa Ole-Nangoro tumeshazungumza kwamba tutafute suluhu na sisi tutoe mchango wetu, naamini tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo kuna suala la matrekta. Limezungumzwa hapa matrekta kutoka India tatizo lililopo hapa ni jinsi ya kuyapata matrekta hayo. Watu wa Mrijo, Kwamtoro, Sanzawa wanahitaji matrekta haya, wana pesa zao kidogo wasaidiwe ili kupitia vyama vyao vya *SACCOS* waweze kukopa

matrekta haya ili waweze kuendeleza kilimo. Tuna ardhi nzuri sana, naamini Serikali itatuangalia kwa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana Serikali kwa kutambua ukubwa wa Wilaya ya Kondoa na kuigawa vipande viwili, Wilaya ya Kondoa na Wilaya ya Chemba. Kijiografia, Wilaya ya Kondoa ni kubwa kuliko Mkoa wa Kilimanjaro. Naipongeza sana Serikali kwa kuona hili na kutupa Wilaya mpya ya Chemba ambako ndio kwenye Jimbo langu. Wananchi wako tayari, wanasubiri kwa hamu kubwa sana lini kazi hii itaanza kutekelezwa. Wameshaanza maandalizi na Makao Makuu ya Wilaya hiyo yalishapatikana mara tu baada ya kutangazwa. Tungeomba jambo hili lifanyike kwa haraka ili na sisi Wilaya ya Chemba tuanze kunawiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la elimu. Tuna Kata 20 na Shule za Kata 21. Kwa ruhusa yako, niipongeze sana Serikali na wale waliobuni wazo hili la kuwa na shule za Kata. Vijana wa Mpendo ambao walikuwa wanashindwa kwenda kusoma Kwamtoro leo wanasoma palepale Mpendo lakini wakati mwingine nikisikia mtu anakejeli Shule za Kata hapa nadhani anajikejeli mwenyewe, Serikali hii imefanya jambo kubwa kweli. Tuna upungufu wa Walimu, vitabu na vitendea kazi vingine, Kondoa inajua na Watanzania wanajua. Jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba vyote hivi vinakamilika, lakini hata Roma haikujengwa siku moja, naamini juhudi zimefanywa na tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni maji. Tuna mradi wa Ntomoko, Serikali imeahidi kuufanyia ukarabati, tuna mradi wa visima vile vya *World Bank*, mimi nilikusudia kutoa shilingi kwenye Wizara ya Maji lakini namshukuru Mungu Mhandisi wa Maji wa Wilaya jana ameniambia kwamba tayari wamepewa kibali ili kuanza kuchimba visima vya maji kule Kondoa, kwa hiyo, wazo langu la kutoa shilingi nimelifuta. Naiomba Serikali kutekeleza mradi huu wa maji wa Ntomoko kwani ungeweza kusaidia vijiji vingi sana kama Kinkima, Jangalo, Itolwa, Mlongiya, Churuku, Igunga na Goima. Hebu harakisheni basi mradi huu uweze kukarabatiwa kwa haraka, mabomba yake yameshachakaa kwani yamewekwa toka 1974 wakati wa Mwalimu, wakati ni ukuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie fursa hii kumshukuru sana Mustapha Sabodo, kwa msaada mkubwa aliotupa wa kuchimba visima virefu vya maji Wilayani Kondoa. Tumepewa visima 11, visima saba viko tayari hata katika maeneo ambayo tangu tumepata uhuru kulikuwa hakuna maji kama Ombiri lakini leo wamepata maji. Niiombe Serikali itusaidie kusambaza maji yale kuwafikia walengwa. Tumeonyesha juhudi, Mzee Sabodo ametusaidia na Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la miundombinu. Nilisimama siku moja hapa wakati Waziri anajibu swali kwamba barabara imeanza kujengwa mimi nikakataa lakini kumbe alikuwa na agenda ya siri. Nimwombe sana Mwalimu wangu Mwakyembe pamoja na kwamba nilisema ukweli, lakini sasa barabara ya kutoka hapa kwenda Kondoa, Babati vumbi limeanza kutimka. Ni Serikali hiihii ya CCM inafanya mambo haya. Naipongeza sana na sisi sasa tunaweza kutoka Kondoa kuja hapa baada ya

kipindi fulani wala sina sababu ya kulipeleka gari kuosha. Nawashukuru sana lakini nilikuwa naangalia bajeti iliyotengwa pale ni kidogo kama shilingi bilioni 10 hivi lakini naamini kutoka Mayamaya pale njia panda ya Usandawe kwenda Kondoa juhudi hizo zitaendelea ili barabara hii ikamilike kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie fedha za Kikwete wanasema Mabilioni ya Kikwete. Fedha hizi hazifiki kwa walengwa. Nilikuwa nazungumza na watu kule Kondoa nimefanya utafiti kidogo sidhani kama wanazidi watu wawili waliopata hizi fedha za Kikwete na hata waliopata sio wale wanaostahili. Naomba tuliangalie jambo hili, tutafute mbinu nzuri za kuweza kufikisha fedha kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo suala la habari, mimi ni mtaalamu wa habari kidogo. Nchi hii haina Sera ya Habari, kila chombo cha habari kinakwenda wanavyotaka, hebu Serikali itunge Sera ya Habari. Kila gazeti likiamka asubuhi wanaangalia wamwelekeze nani, ni mashambulizi tu. Nchi haiwezi kwenda, lazima tuwe na agenda ya Taifa. Mimi nina wasiwasi kama vitaendelea na hali hii baadhi ya Wahariri watakuja kuingia kwenye matatizo kama yaliyowakuta baadhi ya Wahariri wa vyombo vya habari nchini Rwanda. Tuwe makini kidogo, Serikali itunge Sera ya Habari ili tujue tunakoelekea na mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie *TBC* kidogo. *TBC* ina matatizo makubwa. *TBC* wana maeneo mawili Mikocheni na Nyerere Road. Serikali imeshindwa kutoa *guarantee* ya asilimia mia moja ili *NSSF* waweze kukarabati majengo yao yaliyopo pale Mikocheni ili wote wahame kutoka kule Nyerere Road kuja pale Mikocheni. Naomba jambo hili lifanyike kwa haraka. *TBC* imesaidia sana ukombozi wa Afrika, imeleta umoja wetu, *TBC* imechangia kwa kiwango kikubwa sana kueneza lugha ya Kiswahili. Leo Bwana Mshana mmempa kazi pale bila kumpa vitendea kazi, atashindwa. Siku moja kwenye Kamati nikasema kama *TBC* wangeweza kusaidiwa wakahamia Mikocheni kule Nyerere Road inaweza kwenda Wizara yoyote hata Wizara ya Habari wakahamia kule inasaidia zaidi kupunguza msongamano pale mjini na ni Wizara ambayo wanapanga na wana majengo karibu manne hivi, watu wanatembea na mafaili wanakatisha mjini kwenda kupeleka mahali pengine, hili jambo halikubaliki kwa kweli. Ni suala la maamuzi tu, wasaidieni wale ndugu zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie kidogo kuhusu michezo. Kwenye programu ya maendeleo michezo haikutajwa. Nchi nyingi wametumia michezo kama ajira kwa vijana wao kitu ambacho sisi hatufanyi. Tanzania tuna wataalamu wachache sana wa michezo, wanakuja makocha wa kigeni hapa tunawalipa fedha nyingi sana, lakini hata siku moja huwezi kusikia makocha hawa wanatoa semina kwa makocha wa kwetu ili wakiondoka na utaalamu wao walau tubaki na asilimia kidogo ya wataalamu wa hapa nyumbani. Amekuja Maximo, akaondoka na utaalamu wake. Amekuja Paulsen, yule mama kwenye *Netball* au yule kocha wa Cuba kwenye ngumi, watamaliza mikataba, wataondoka, tutawaita tena wageni. Hakuna nchi iliyofanikiwa kwa wageni tu, tulitazame jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nizungumzie kidogo amani na utulivu. Watu wanazungumza sana kwamba nchi yetu sijui nini, sijui nini, hawajatembea, mtu ametoka Dar es Salaam ameenda Mbozi, kutoka Mbozi ameshinda Ubunge amekuja Dodoma. Katoka Iringa pale katikati kaja Dodoma alisafiri sana kaenda Sweden, hakutembea, hajui nini maana ya amani na utulivu. Mtu anasema Tanzania ni maskini sana, si kweli. Hebu tembea uone nchi nyingine zilivyo ndio unaweza kupata kiburi cha kuzungumza maneno hayo. Mtu anasema kwa sababu mtu ana njaa hii sio amani, si kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda hapa Afrika ya Kati, *one of the poorest country in the world* lakini watu wameshikamana wanafanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yao lakini mtu mzima anasimama anasema nchi hii haina amani, ni bora tupigane, mtakapopigana wewe hutakuwepo. Wewe utaondoka, watakaoumia ni mama na watoto wetu. Machali unaniangalia, wewe una uwezo wa kuzama pale Ukerewe, lakini watu wangapi wanaweza kuzama Ukerewe wakakimbia machafuko? Nafikiri jambo la msingi, *let us think first* kabla ya kuzungumza, hili ndio jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasema kwamba uchaguzi ukiisha siasa zinahamia katika Bunge, hebu tuacheni wanafunzi wasome. Hizi safari za kila siku za watu wanatoka hapa wanakwenda *UDOM* kupiga kelele usiku kucha mnawafanya watoto wale wasisome ili wasije kuwatoa kwenye Majimbo yenu. Waacheni wasome ili na wao waweze kutekeleza wajibu wao kama Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa Hotuba ya Bajeti Ofisi ya Waziri Mkuu na mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii ni Mheshimiwa Iddi Azzan na Mheshimiwa Said Mussa Zubeir ajiandae.

**MHE. IDDI M. AZZAN**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi hii ya kwanza jioni hii ya leo na mimi nichangie hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nipongeze sana Hotuba ya Waziri Mkuu, ilikuwa nzuri, imeelekea kutekeleza kila jambo ambalo tumeahidi kwenye Ilani yetu ya uchaguzi ya mwaka huu 2010 - 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza kusimama na kuongea ndani ya Bunge hili, naomba nichukue nafasi hii pia kuwapongeza na kuwashukuru sana wanachama wa CCM wa Jimbo la Kinondoni, kwa kunichagua kuwa mgombea wao lakini nashukuru wananchi wa Jimbo la Kinondoni kwa kunipigia kura

nyingi sana za ndio na kuniwezesha kuingia hapa Bungeni, nawashukuru sanasana. Nachowaahidi ni kuwatumikia kwa uadilifu na unyenyekevu mkubwa. Deni langu kwao ni kuhakikisha yale ambayo tumeyaahidi kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi tunayatekeleza na hilo nitalisimamia kuhakikisha yote hayo tunayatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kilichopita ama miezi miwili, mitatu iliyopita, Jiji la Dar es Salaam lilikumbwa na mvua kubwa sana na bahati mbaya mvua ile imeleta madhara makubwa kwenye barabara. Bahati mbaya zaidi hata Bajeti ya Halmashauri zilikuwa zimeshapitishwa na hata zingekuwa hazijapitishwa kwa hali ambayo imejitokeza sidhani kama Halmashauri zingeweza kuzijenga barabara hizi kwa jinsi ambavyo zimeharibika kwa sababu zinahitaji pesa nyingi sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu waiangalie Dar es Salaam kwa jicho la huruma. Kwa sababu mbali ya foleni na misongamano mikubwa iliyokuwepo ya magari lakini hili la mvua kuharibu barabara limefanya barabara hizo zizidishe msongamano. Maeneo mbalimbali yameharibika, barabara ya Kinondoni kwa Manyanya kwenda *Surrender Bridge* nayo imeharibika sana na haifai na ni barabara kubwa ambayo inatumiwa na watu wengi. Kwa hiyo, niombe sana Serikali ituangalie kwa jicho huruma kwa maana ya kuhakikisha barabara hiyo inatengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu Tandare kwa Mtogole, haijawahi kutokea lakini mwaka huu imetokea, maji yaliacha kupita kwenye njia zake na yakaingia barabarani, yameharibu sana barabara na nyumba za makazi ya watu wa maeneo yale. Kwa sababu mifereji iliyokuwepo ni midogo haikidhi, matokeo yake barabara ya Sinza – Uzuri imeharibika na yenyewe tunaomba Serikali iingalie kwa sababu barabara ile ni kubwa sana na inahudumia watu wengi sana. Naomba tuone ni jinsi gani ya kuweza kuitengeneza. Kuiachia Halmashauri peke yake haitaweza kwa sababu gharama za ujenzi ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam tunazo Hospitali tatu kubwa, Temeke, Ilala pamoja na Mwananyamala. Bahati nzuri zilipandishwa hadhi kuwa za Mkoa lakini mpaka sasa hivi ninavyozungumza mgao haujapatikana. Kwa hiyo, ni hadhi ya Mkoa kwa maana ya jina lakini dawa, Madaktari Bingwa ni walewale. Niiombe sana Serikali kwa sababu tumeshakubali na tumeshapandisha hadhi Hospitali hizi basi zile stahili zake zipatikane kwa maana ya kuongezewa dawa, Madaktari na Madaktari Bingwa na Wauguzi ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu. Hospitali hizi zinahudumia watu wengi sana kwa siku. Zaidi ya watu 1200 kwa siku wanahudumiwa katika Hospitali hizi hasa Mwananyamala. Sasa niiombe Serikali ijitahidi sana kuhakikisha kwamba Hospitali hizi zinapatiwa stahili zake ili ziweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mihimili hii mitatu, Utawala, Bunge na Mahakama, tukiuliza leo mhimili huu wa Bunge Kiongozi wake anaishi wapi, wote humu ndani mtapata tabu lakini bahati nzuri Kiongozi wa Mhimili huu wa Bunge kwa maana ya Spika wa Bunge hili anaishi Kijitonyama. Mheshimiwa Spika ni mvumilivu kwa sababu badala ya kuishi pale kwenye nyumba yake labda angeamua kukaa kwenye *Hotel*. Serikali ingeingia gharama kubwa sana lakini amekubali kukaa kwenye nyumba yake lakini ukitaka kwenda kwake kama hutumii boti basi utumie *fourwheel* la ukweliukweli

unaweza usifike. Barabara ni mbovu mno, tumeiombea barabara ile kupitia Halmashauri, Halmashauri wameahidi kuitengeneza kwa mwaka huu kwa sababu lilikuwa ni ombi la tangu nimeingia Bungeni nalalamikia barabara hiyo ya Polisi Mabatini lakini Halmashauri imesema inaweza ikaitengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hiyo tu, kuna ile ya Masjid Quba ambazo zote ni mbovu hazipitiki. Niiombe sana Serikali iangalie kwa jicho la huruma barabara hizi kwa sababu kwanza zinatumiwa na wananchi wengi, zimeshakuwa ni barabara kubwa lakini tufahamu pia na kiongozi wetu yuko kule. Baya zaidi kwa sababu barabara hizi ambazo zimewekwa ili wananchi wapite zimeshakuwa mbovu, wananchi wanatumia vichochoro sasa kama ndiyo njia zao matokeo yake inaleta matatizo. Kwa hiyo, ili kuondoa tatizo hili, tuombe barabara hizi Serikali itusaidie ili ziweze kujengwa kwa kiwango kizuri cha lami kuwasaidia wananchi wetu waweze kupita vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu nilipoingia Bungeni mwaka 2005, mwaka 2006 nilizungumza kuhusu soko la Tandale na inapotokea njaa ama tatizo lolote la uhaba wa chakula Viongozi wetu Wakuu hukimbilia Tandale kuangalia vyakula kweli vimepungua ama vipo. Bahati mbaya sana, soko la Tandale nimelizungumza mara nyingi sana, halistahili, ni mabanda mabovu mno ukiachilia mbali barabara. Sasa niiombe Serikali na hili nalo tuliangalie. Kwa Halmashauri zetu hizi haziwezi, mzigo ni mkubwa sana, kipato cha Halmashauri ni kidogo. Kwa hiyo, niiombe Serikali iingalie kwa jicho la huruma pia soko la Tandale kwa maana ya kulijenga vizuri na kutengeneza barabara ili mazao yanayotoka kwenye Mikoa mbalimbali yanapokuja Dar es Salaam kusiwe na tatizo, kuwe na hifadhi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mapato ya Halmashauri. Dar es Salaam tulikuwa tunakusanya kodi za majengo lakini tukasema hapana hebu tuwape *TRA* wakusanye wao. Kwa hiyo, kazi hiyo amepewa *TRA* tangu mwaka 2008/2009. Mwenendo wa makusanyo umekuwa hauridhishi kwa sababu hakifikii kile kiwango ambacho tulikuwa tunakitarajia kama Halmashauri, lakini hata watendaji wa *TRA* hawafiki hata kule mitaani kwa sababu ni wachache. Naomba sana Serikali iliangalie upya jambo hili na ikiwezekana suala la ukusanyaji wa mapato lirudishwe kwenye Halmashauri husika ili tuweze kukusanya vizuri lakini pia kuzitumia katika miradi yetu mbalimbali ya maendeleo. *TRA* atakusanya lakini atazirudisha kwenye Halmashauri vile inavyotaka, maendeleo ya wananchi wetu yanazidi kuchelewa. Kwa hiyo, niombe sana kwa sababu Halmashauri hizi zimeshajifunza, kwa mfano, Kinondoni *database* iko tayari tumeshajipanga vizuri basi tuangalie uwezekano wa kuruhusu sasa Halmashauri hizi zikusanye mapato yake yenyewe ili yaweze kusaidia kwenye mambo mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Mawakala wa kukusanya mapato kwenye Halmashauri. Nalizungumzia hili kwa sababu nimepata uzoefu wa kutembeatembea na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Yapo matatizo makubwa sana, Serikali ijaribu kuwaelekeza ama kulisimamia vizuri. Ni kweli, tunaweza tukawapa Mawakala kukusanya hizi lodi na mapato ya Halmashauri lakini makusanyo yale hayakusanywi vile inavyotakiwa na mifano ipo. Jiji la Dar es Salaam kituo cha Ubungo

alipewa Wakala akawa anapokea shilingi milioni 1.5 kwa siku, lakini baada ya wenyewe kuchukua kazi ile tunakusanya zaidi ya milioni tano kwa siku. Kwa hiyo, unaona ni jinsi gani Mawakala hawa walivyokuwa sio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hapo tu nimeona hata Mkuranga na Mbunge wa Mkuranga atanisaidia, kwamba Mkuranga na wenyewe walimpa Wakala akawa anakusanya, kwa mwezi anawapelekea shilingi milioni tatu, siku nyingine milioni tisa anapeleka anavyotaka, ikawabidi kumwondoa. Mkurugenzi wa Mkuranga, tena ni mwanamke, nimesahau jina lake, alisimamia vizuri pamoja na kupingwa lakini aliweza kumwondoa na wamempa wakala mwingine. Hivi sasa wanakusanya shilingi milioni 24 kutoka kwenye shilingi milioni tatu hadi tisa. Kwa hiyo, tuwe tunaangalia sana na Mawakala hawa tunaowapa kazi ya kukusanya mapato ya Halmashauri kwa sababu wengi wapo kwa ajili ya kujinufaisha wao si kwa ajili ya Halmashauri zile, pamoja na kwamba wanawatumia baadhi ya viongozi wa Halmashauri kutengeneza mipango hiyo. Tukipata Wakurugenzi kama huyu wa Mkurunga, ninahakika Halmashauri zetu tutapata mapato makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza sana kuhusu Madiwani, ikiwezekana wapatiwe hata mishahara. Mimi nasema tuangalie uwezekano wa kuwasaidia Madiwani. Bunge lililopita tulipitisha misamaha ya kodi kwa vyombo vya usafiri kwa Madiwani lakini mpaka leo imekuwa ni hadithi hakuna hata kimoja kilichofanyika, misamaha ile ya kodi ya vyombo vya usafiri haijapatikana mpaka leo. Madiwani hawa wanatusaidia kwenye kazi zetu, wanajitolea sana na kufanya kazi kubwa sana kwa hiyo tuangalie ni jinsi gani tutawawezesha kupata ile misamaha ya vyombo vya usafiri lakini pia angalau sasa badala ya kuwapa posho mtu awe anapata hata mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nyumba za *National Housing.* Nimeona na hili nalo nilisemee. Nikubaliane nao tu kwamba suala lao la kupandisha kodi ni sawasawa, kodi zipandishwe ili fedha zile zitakazopatikana ziweze kwanza kuboresha hizo nyumba lakini kuweza kujenga nyumba nyingine ambazo zitawasaidia watu wengine kupanga. Watu wangu wa Jimbo la Kinondoni wanaoishi kule Mtogole, Mkunduge, Mbuyuni, Kisiwani na Suna, hawataki kuishi kule kwenye maji ni kwa sababu hakuna maeneo ya kujenga nyumba na mjini nyumba ni tabu kupata. Sasa Shirika letu la Umma lijitahidi basi kujenga nyumba nyingi ili na hawa nao waweze kwenda kupanga kwenye nyumba hizo nzuri. Mwananchi wangu anayepanga Uswahilini analipa shilingi 35,000/- kwa chumba vyumba viwili 70,000/- lakini anayekaa Upanga anakaa *flats* analipa shilingi 48,000 au 50,000/- kwa hiyo, huku si kuwatendea haki hawa wananchi wa hali ya chini. Niombe sana waongeze kodi lakini wahakikishe kwanza wanaboresha nyumba hizo na kujenga nyumba nyingine nyingi ili ziweze kuwasaidia wananchi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, ujenzi umekwenda vizuri. Tangu nimeingia Bungeni mpaka juzi nilipoleta Walimu wa Shule ya Msingi Muongozo kwenda kutembelea Chuo hicho, nimeshaleta watu zaidi ya 600 na wote waliokuja wananiambia nitoe pongezi kwa Serikali lakini nitoe pongezi sana kwa Mkuu wa Chuo pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo Profesa Idrisa Kikula kwa jinsi ambavyo ameweza kusimamia

ujenzi wa Chuo hiki na kimekuwa ni mfano katika Afrika na ninahakika wanafunzi wanaokwenda pale wanakwenda pale kwa ajili ya kusoma na si kwa ajili ya mambo mengine. Kwa hiyo, ni jambo zuri ambalo limefanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Nne, tuliahidi na tumetekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Ndugu Reginald Mengi, Mkurugenzi wa *IPP* kwa jitihada anazofanya za kuwasaidia watu mbalimbali wasiokuwa na uwezo, walemavu na hasa kupiga kampeni na kutokomeza njaa. Mzee huyu anajitolea sana, niombe na wafanyabiashara wengine waige mfano wake kwa sababu amefanya mambo mengi ya kusaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni suala la maji. Tunalo tatizo la maji Dar es Salaam, tumeshaelezwa kazi inafanyika. Niiombe Serikali iongeze jitihada kuhakikisha tatizo hili la maji linaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tatizo la umeme, mgao umekuwa ni mwingi, unakatisha tamaa Dar es Salaam. Karibu asilimia 80 ya pato la Taifa linatoka Dar es Salaam, tukiendelea kuwanyima umeme kwa kiasi kikubwa namna hii, hatuwatendei haki. Niombe suala la mgao wa umeme tuliangalie vizuri ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na msitu wa kifo. Kuna msitu ambao upo kwenye bonde la Mkwajuni. Mara nyingi maiti zinaokotwa pale, watu wanauawa na watu wanakabwa sana kwa sababu ya kimsitu ambacho kimewekwa pale. Tunataka kuundoa huo msitu lakini utasikia sijui mazingira, sijui kitu gani, wanakataa. Naomba Serikali waliangalie ili tuweze kuondoa kero ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kupata nafasi hii jioni hii ya leo.

Kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema bado ninatweta na *inshallah* kwa uwezo wake nitamaliza miaka hii na mingine ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Fuoni kwa ushindi walionipa, ushindi wa kishindo na kuweka historia katika Jimbo la Fuoni kwa mara ya kwanza Mkoa wa Mjini kuongoza kwa kura za CCM. Nawashukuru sana, nawaambia tuko pamoja na nawaahidi tutashirikiana na sitawaangusha. Nipeleke shukrani za pekee kwa Kamati yangu ya *Nuclear Family* ambayo hii ndiyo iliniwezesha kufika hapa, hii ndiyo ilikuwa *campaign team* yangu, walinisaidia sana nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za kipekee kwa familia yangu, wakati wote walikuwa karibu na mimi na kila nilipokuwa nikipata matatizo basi walikuwa wakinifariji. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Spika wetu kwa kuweka historia katika nchi yetu ya Tanzania kuwa ni mwanamke wa kwanza kushika nafasi katika mihimili mitatu ya nchi yetu, nampongeza sana na nasema kwamba kweli wanawake wakiwezeshwa wanaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisije nikasahau naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tutake tusitake tunatakiwa tujivunie amani tuliyonayo Tanzania na nitawapongeza Waasisi wa suala hili, Mheshimiwa Marehemu Rais wetu wa kwanza ambaye yeye aliasisi hii amani kwa njia alizozielewa yeye mwenyewe na Mungu alimpa nguvu ya kufanya hivyo. Kwa hiyo, sisi tuliobaki ni wajibu wetu kuilinda, tusiidharau na tuhakikishe kwamba inaendelea hivihivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie na mimi kuhusu miaka 50. Kuna watu wengi ambao wanaibeza lakini labda mimi niulize watu, hivi wanaoibeza ni akina nani? Jibu liko jepesi tu kwamba tuko kwenye Mfumo wa Vyama Vingi, kwa hiyo, wanaoibeza aghalabu watakuwa ni upande mwingine. Sasa jamani hili lisitupe taabu, tumeingia kwenye uchaguzi, tumefanya tulilofanya, wananchi wametukubali, wametuchagua kwa asilimia kubwa, kwa hiyo, kilichobaki sasa hivi kwa Wapinzani wao ni kufuja tu, hili lisitusumbue. Chochote kile tutakachosema hiki ni kizuri basi kwao wao kitakuwa kibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naamini kuna mambo mengi ambayo yamefanywa kwa miaka hii 50, kwanza wanazungumza mambo ambayo hayapo, kwa sababu wanazungumza kinyumenyume. Mtu anasema kwamba haoni chochote lakini yeye yumo kwenye Bunge hili halafu anasema haoni chochote kilichofanyika lakini yeye amemaliza Chuo Kikuu, huko nyuma mambo haya hayakuwepo. Tunaambiwa na wazee wetu kwamba watu walikuwa wakilala kwa ngoma na kuamshwa kwa ngoma yaani mpaka ngoma ipigwe na hao watu waamke na goma lipigwe hilo watu walale. Sasa tunalala kwa wakati tunaotaka tunaamka kwa wakati tunaotaka, tunafanya shughuli zetu tunavyotaka. Jamani haya mambo mengine mimi naona ni sisi wenyewe tu-*pull up our socks to make sure* kwamba Tanzania inabadilika, hili ni jukumu letu sisi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea upande wa Serikali, kama tunavyosema ni Serikali sikivu na iko makini, hili nakubaliana nalo kwamba ni Serikali makini lakini usikivu huu usifikie mahali tukasahau majukumu yetu, tunachotakiwa kuelewa ni kwamba sisi tayari tumeshatawala, ni lazima yale tuliyoyakusudia kuyafanya na hususani katika mpango huu wa miaka mitano tuyaendeleze, siyo turudi tena mezani. Haya ndiyo Wapinzani wanayataka kwamba turudi kwa kuona tumekosea, hakuna tulichokosea katika mpango wa miaka mitano, binadamu siyo mkamilifu, vipaumbele tulivyoviweka vyote vinastahili na vinafaa, kinachohitajika sasa hivi ni kuhakikisha

kwamba kila mmoja na sekta yake anakwenda kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu tulizonazo. Hili ndiyo jambo la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu siyo wakati wa kuogopa kivuli chetu, hawa Wapinzani hatuwezi tukawakimbia, wamo humu na walikuwepo tangu enzi za Mitume mpaka leo wapo. Hawa tutaendelea kuwa nao tu tusikimbie kivuli chetu wala kisitutishe kivuli chetu, kelele za mlango zisimshughulishe mwenye nyumba, ukifika wakati wa kulala lala, ukifika wakati wa kusoma wewe soma tu. Sisi tunachotakiwa ni kujipanga vizuri kuhakikisha kwamba haya mambo yetu tunayaendeleza, hawa wa kufuja wataendelea tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo vijijini, barabara ni mbovu, tukasema leo kwa kuwa Serikali labda haikuweka bajeti ikaweke angalau kifusi tutakuwa tumewasaidia wananchi, lakini hawahawa Wapinzani ambao tulishawapiga bao basi wao watatoka moja kwa moja watakwenda kijijini na kusema kwamba sasa iambieni Serikali yenu iwajengeeni na zahanati humu pembeni kwa sababu sasa wamewawekea vumbi hapa gari zikipita mbio mtatakiwa ninyi mkapimwe afya zenu baada ya miezi sita msije mkaonekana na *TB* watawaambia hivyo, wao kazi yao ni kufuja tu lakini kumbe maendeleo yameshafanyika. Serikali ikisema kwamba labda sasa twende tukaweke lami kule, ile lami ikiwekwa watarudi tena hivyohivyo watakwenda kwa wananchi walewale badala ya kwenda kuwapa elimu kwamba sasa jamani huku kulikuwa hakuna barabara ya lami sasa hivi mpate elimu ya barabara muishi nayo vipi ili mpunguze ajali, wao wataenda kuwaambia sasa jamani waambieni Serikali yenu iwatengenezeeni majeneza kwa sababu sasa hivi watu wanakufa. Wao kazi yao ni kwenda kutia chuki tu, hiki ndicho wanachokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mimi niwaulize, wana kazi gani sasa hivi? Uchaguzi umeshakwisha, nchi tumeshachukua, ridhaa tunayo, kitu gani kilichobakia kutoka kwao? Kwa hivyo, haya maneno mimi naona yasitushughulishe, sisi tufanye kazi. Hili ndiyo jambo la msingi, wananchi wametuamini na wanajua kwamba hii Serikali ni makini tangu muda huo tumeipa nafasi na bado inatuendelezea mambo yetu vizuri. Kwa hivyo, bado tuendelee kujiamini kama tulivyoaminiwa na hawa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Tanzania ni watu wenye akili zao timamu siku zote mimi nasema. Nitoe mfano tu, hivi ikija timu ya Brazil hapa kwetu tutakwenda wengi kuwalaki kwa sababu tutakuwa tunataka kuwatazama na wakifika vijijini watu wanaweza hata wakaacha kulima wakaenda kuangalia timu ya Brazil, hivi sasa ndiyo iwe sababu ya kusema kwamba kwa hivi tulivyoangaliwa na Watanzania, sasa tuwaambie Watanzania kwamba tunataka hii nchi ili tuongoze, hapo ndipo watakapojua kwamba kitunguu ni mboga ama ni urembo katika mchuzi. Kwa sababu watakapoelewa kwamba Watanzania wana akili zao timamu, wale Watanzania walitoka kwenda kuangalia timu ya Brazil kwa sababu ile ni timu ambayo hawajawahi kuiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mikutano iliyokuwa ikiwashughulisha hawa wenzetu wakajiona labda kila wakikusanya watu wanakuwa wengi, walikuwa wanaona kama *comedy*. Ni kama vile sasa hivi *the comedy* itoke huko ije hapa iseme inataka ipewe

nchi iongoze, kwa sababu *majority* wanayo, hata wale wanayo. Tukitoka hapa jioni saa kumi na mbili jioni tunaenda kuwaangalia, hivi wafikie mahali waseme kwamba na sisi tunataka nchi hii, haya mambo hayawezekani kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wana akili, wanawatazama tu, ndiyo maana wakashangaa siku ya kura, walivyoona wale watu walivyokuwa wakikusanyika, kumbe walikuwa hawajui kwamba walikuwa wanakwenda kuwasikiliza tu baadaye wanachukua wanaweka waah! Wanaelewa wenyewe watakayempigia kura, wamewapigia kura CCM. Kwa hiyo, mimi ninachowaombeni kwa hisani zenu viongozi hususani Mawaziri, mmepewa nafasi…

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kalisha vikalio.

**MWENYEKITI:** Hilo neno sijalisikia.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwambia akalishe makalio jamani, si ndiyo anakaa chini.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ndiyo lugha ya Zanzibar hiyo na ndiyo lugha ya kawaida.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba sana tutumie Bunge kama sehemu Takatifu, nilikuwa naamini kwamba hujaridhika na kauli ambayo imetolewa na msemaji aliyepita na ninajua ilikuwa hivyo, lakini sasa na wewe umeleta yaleyale, sasa unakipa Kiti wakati mgumu kwa sababu huwezi ukahukumu kesi wakati kuna kesi nyingine imezuka. Sasa mimi nikuombe tu lugha zako ziwe za kistaraabu kidogo na wewe umeanza vibaya, Kiti hiki hakina msaada hapa. Tuendelee. *(Makofi)*

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote Waswahili husema anayejishuku ndiye huyohuyo.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68 inaniruhusu kuomba utaratibu kuhusiana na kilichotokea hapa. Nadhani maelezo yako uliyoyatoa kwamba hili Bunge lina lugha zake na Mheshimiwa Spika ameshatoa maelekezo mengi sana na nadhani kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Spika, *temper* ya Wabunge ilipungua kwa kutumia maneno makali na ya kebehi na tunataka iendelee hivyo. Kilichotokea hapa, naomba unisikilize…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naamini kabisa wewe ni Mwanasheria, ukisema kuhusu utaratibu unasema Kanuni ipi imevunjwa, sasa ungenisaidia hapa, mimi

nahangaika kujua ni Kanuni ipi imevunjwa, huniambii, unaanza kuhutubia Bunge. Mzungumzaji anayechangia aendelee.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza uzilinde dakika zangu nilizokaa chini. Mimi bado kabisa na wala hajanitoa kwenye *mood.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza taratibu lakini nitaishia hivyohivyo. Wananchi wa nchi hii wanahitaji maendeleo hawahitaji kitu kingine, hawahitaji umaarufu mtu kujipatia kwenye nafasi hizi na hili liko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita hapa kuna Mheshimiwa mmoja alikuwa kila akipewa nafasi kama hiyo Mwenyekiti uliyompa huyu ajirekebishe yeye alikuwa hajirekebishi, anaendelea kung'ang'ania na kurejea neno lake lilelile. Wananchi wamemsikiliza na wanasikia. Leo hapa imetoka *solution* baada ya wiki nzima ameambiwa alete uthibitisho, matokeo yake imekuwa ni kinyume kabisa.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mbunge, hebu wewe changia mchango wako uliojiandaa, haya yaliyozuka hapa yasikuharibie hotuba yako nzuri uliyoiandaa.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tuje kwenye suala la uchumi, uchumi wetu umekua kwa asilimia saba, naipongeza sana Serikali na naiomba iendelee na utaratibu huu, lakini vilevile ni lazima tuwe na tahadhari hususani kwenye masuala ya uwekezaji, rasilimali kubwa tunayoitegemea kwenye nchi yetu sasa hivi ambayo haina gharama kubwa na bado tunayo ya kutosha ni suala la madini. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe kwamba inapoingia mikataba na hawa watu, mikataba hiyo iwe ya ufanisi zaidi, vinginevyo ni afadhali madini yaliyobakia huko chini kwa sababu yatakwisha haya na vizazi vyetu vitakuwa havina urithi. Kama hatujajipanga vizuri na hatujakuwa na elimu ya kutosha na hawa wawekezaji wanatupora sana basi tungesitisha uwekezaji huu na tutafute utaratibu mwingine kama alivyofanya Rais wetu wa Kwanza Marehemu Mwalimu Nyerere, Mungu Amrehemu, alifanya hivi kwa vile alikuwa na maana yake. Kwa hivyo na sisi naomba tuende kwa mtazamo mzuri wa kuhakikisha kwamba haya madini tuliyonayo ambayo yamebaki kwenye nchi hii, ni rasilimali tosha ya kuweza kusaida nchi hii kuondoka hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Jeshi la Wananchi, suala hili lina utata kwa upande wa Zanzibar. Tunaomba sana wastaafu wangefanyiwa utaratibu angalau ingewekwa kanda kwa upande wa Zanzibar ili wakishastaafu wasiwe na ule mpango wa wastaafu wa kuja na kurudi Dar es Salaam, wabaki Zanzibar na wakaendelea kupata huduma zile kulekule. Naomba sana hili suala lifikiriwe kwa sababu wanapokuja huku wanapoteza fedha na pengine utaratibu unakuwa haujakaa sawa, wakati mwingine unakuwa bado kwa upande wa Wastaafu wenyewe na wakati mwingine inakuwa bado kwa upande Serikali, haya mambo mawili yote yanakuwa yanakinzana, iwe kwa upande wa Serikali au wastaafu wenyewe wanakuwa hawajakamilisha taratibu zao. Kwa hiyo, naomba sana Serikali suala hili lingehamishiwa Zanzibar kwa watu wa Zanzibar ili Wastaafu hawa waweze kupata mafao yao katika hali nzuri ya kuweza kutumia zile pesa zao, kwa sababu wamekuwa ni kama wanazitumia kwa nauli tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Muungano, kwanza kabisa naunga mkono katika nafsi yangu kwamba na mimi sitaki Muungano uvunjike kama walivyoanza kusema Mwalimu wangu Mohamed Ibrahim Sanya kwa sababu yule ni Mwalimu aliyenisomesha shule somo la Jiografia, pamoja na Bi Riziki nami ninawaunga mkono kwamba Muungano usivunjike tutataka uendelee kudumu, ila ni lazima tukubali kwamba hizi kero zilizopo zishughulikiwe haraka iwezekanavyo kabla ya kuingia kwenye masuala ya Katiba. Naamini kero zikiisha siyo kwamba tutakuwa tumemaliza kero, zitakuja zingine, lakini nahisi kwamba Watanzania hawatakasirishwa tena au kuona bughudha kwa kero mpya, kwa sababu watajua kwamba zile kero za mwanzo zimeshughulikiwa na hizi zinazokuja zitashughulikiwa. Haya ni mambo ya kuendelea, tukimaliza zingine na zikiondoka hizi zitakuja zingine, lakini ni vizuri basi zile tulizo nazo tuzishughulie ili tuzipe nafasi hizo kero nyingine zije. Naomba sana hili kwa upande wa Muungano lishughulikiwe *as soon as possible* ikiwezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Said Mussa Zubeir.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7) ambayo inasema kwamba hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama…

**MWENYEKITI**: Usiisome endelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilikuwa natoa taarifa ukanikinza kidogo, Mheshimiwa Spika alitoa maelekezo ambayo naomba na wewe uyatilie msisitizo ili haya masuala yasiendelee humu ndani. Kwa sababu hatutaki kutengeneza Bunge ambalo linakuwa Bunge la vijembe, kwa sababu kijembe anakianzisha mtu na mwingine anakimalizia. Mwongeaji aliyepita katumia maneno mengi sana makali, amesema kitunguu mboga, lakini kibaya akasema uchaguzi umeshaisha sisi tunafanya nini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni ya Mfumo wa Vyama vingi uliotambuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano, sasa inawezekana Mheshimiwa hajawahi kusoma Katiba wala haijui, naomba Kiti chako kitoe Mwongozo wa hizi lugha za kebehi, dharau ambazo hazina tija, zinazoendeshwa na Wabunge ili tujadili mambo ambayo wananchi wametutuma tufanye na siyo vinginevyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wakati mwingine ni vigumu sana kuwa mwamuzi mzuri kwa sababu unapofikiria ufanye uamuzi sasa unapata tatizo zaidi ya lile lililokuwepo. Anacholalamikia Mheshimiwa Mdee ni maneno ‘kitunguu mboga,

uchaguzi umeisha mnafanya nini', wewe unasema Mheshimiwa Mbunge mzima ambaye amechaguliwa na kuingia humu Bungeni hajawahi kusoma Katiba na haijui.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Na ndiyo nilikuwa nataka na mimi nipewe nafasi. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI**: Kwa hiyo, Mwongozo wangu sasa niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, hebu tujaribu kuwa na lugha za Kibunge, tujaribu kuwa na lugha za staha, ili tusikwazane. Mimi naamini kila Mbunge anayepata muda wa kuchangia hapa ameandaa hotuba yake, hebu tusije na hotuba zingine za kuanzia hapa ndani. Tuseme yale ambayo tumejiandaa ili tuweze kuwasaidia wananchi na Taifa letu. Huo ndiyo mwongozo wangu, tuwe makini na lugha zetu ili tusikwazane pamoja na siasa za Vyama vingi lakini uvumilivu uwepo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mzungumzaji anayefuata Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi aendelee.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Waziri Mkuu iliyopo mezani kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi, Wanawake kwa wanaume, walioniwezesha mimi kufika hapa Bungeni na kuonekana mtu mbele ya watu, nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbali, naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Nachukua nafasi hii vilevile kuzungumzia mambo ambayo yamo katika hotuba ya Waziri Mkuu. Hotuba hii ina vipengele karibu 23, nimevisoma kwa umakini sana. Vipengele hivyo ni vipengele ambavyo kwa kweli vimegusa matakwa ya wananchi mbalimbali, nami nitaongelea vipengele vile ambavyo nitaweza. Nianze na ukurasa wa 10 wa kitabu hiki cha Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa kumi unazungumzia masuala ya kilimo, uchumi, hasa suala la kufufua suala kilimo nchini. Suala la kufufua kilimo nchini ni kubwa na linawagusa wananchi wengi. Waziri Mkuu amezungumza kwamba kutakuwa na Benki ya Kilimo katika dirisha la *TIB*, kutakuwa na azma ya kuanzisha ya kuanzisha ushirika, kutakuwa na kuanzisha shughuli za Kilimo Kwanza na kutakuwa na azma ya kuanzisha *SAGCOT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la SAGCOT *(Southern Agriculture Growth Corridor),* Ukanda wa Kilimo wa Kusini mwa Tanzania. *SAGCOT* imebeba jina zito sana Kusini mwa Tanzania, nikitegemea kwamba Mkoa wa Lindi na Mtwara itakuwemo katika mpango huo na wenzangu waliopita wamezungumzia suala

hilo. Naomba sana *SAGCOT* hii ya miaka 20 ambayo itaendeleza kilimo na kufufua kilimo nchini, Mkoa wa Lindi na Mtwara tuingizwe katika suala zima la kufufua kilimo nchini, kwa sababu sisi Mkoa wa Lindi tunayo mabonde ya umwagiliaji maji, tunayo maeneo ya kilimo, sasa kwa nini na sisi tusiingizwe katika mpango huu wakati jina lenyewe linabeba Mikoa ya Kusini na ukitaja Mikoa ya Kusini maana yake unataja Lindi, Mtwara, Ruvuma ipo lakini katika kijiji kimoja tu cha Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunayo mabonde 17 ya umwagiliaji maji kila Wilaya, ukianzia Wilaya ya Liwale, kuna Mtawatawa, Ngongowele na Mtowango. Ukija Wilaya ya Luangwa kuna bonde la Chikoko, Mkoe, Chinakole, Chimbila A, Chimbila B. Tunayo mabonde ya Mkunja, Chenjele hayo yapo Wilaya ya Luangwa peke yake. Ukienda Lindi Vijijini tunayo mabonde ya Kinyope, Nkwaya, Mtama, Lukuledi, Rutanda, haya ni mabonde ya Wilaya ya Lindi Vijijini. Katika Wilaya ya Kilwa tuna Bonde la Matandu na Bonde la Makangaga na Lindi Mjini tunalo bonde la Ngongo. Kwa hiyo, mabonde haya yote 17 tungeweza kuingizwa katika kilimo na sisi tungeweza kuwa na kipato fulani kwa sababu tusipoingizwa katika mpango huu maana yake ni kwamba hakuna miundombinu ya kilimo, hakuna pembejeo, hakuna wafanyakazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana mtuingize katika mpango huu wa *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania* kwa sababu Mkoa wa Lindi ni maskini. Umaskini tuliokuwa nao sisi si kwa ajili ya uvivu, wala kujitakia wala si kwa makusudi. Umaskini tuliokuwa nao sisi Mkoa wa Lindi, wenzangu waliotangulia wamezungumzia, ni kwa sababu za kimsingi kabisa za kuendeleza nchi hii. Kwa mfano, Mkoa wa Lindi, tulikuwa katika mpango wa kuendeleza suala la Ukombozi wa Afrika, Mkoa wa Lindi, kulikuwa na nchi ambazo ziko pale zinafundishwa upiganaji kwa ajili ya ukombozi wa Afrika. Kulikuwa na Kambi ya Mandela ya Afrika Kusini, kulikuwa na Kambi ya Samora Machel na Mondrane, kulikuwa na Kambi ya Zimbabwe. Kwa hiyo, kutokana na Makambi yale ya vita Mkoa wa Lindi haukuweza kuendelezwa ili suala zima lile lisifichuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mnavyotuacha katika mipango ya maendeleo kwa kweli tunapata matatizo sana. Si hilo tu, sisi tumekuwa nyuma kwa sababu sera za kikoloni za zamani ziliendeleza mikoa mingine ikaacha Mikoa ya Kusini, ili iweze kutoa manamba na wao kuwachukua kama wafanyakazi kwenda kukata mkonge katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Pangani na Zanzibar. Wakoloni walikuwa wanatuchukua kwenda kufanya kazi za Mkonge. Katika Mikoa hiyo mpaka sasa hivi wananchi wa Mkoa wa Lindi wapo kule utawakuta Wamakonde, Wayao na Wamakua, wapo kule, walikuwa wanafanya kazi ya kukata mkonge, *cheap labour*. Kwa hiyo, hawakutaka kuendeleza Mikoa ya Kusini ili wapate wafanyakazi. Kwa hiyo, hatukuwa wavivu kwa makusudi isipokuwa ni mazingira ambayo yalitukumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile milima ya Mikumbulu na Mto vile vile ilitufanya sisi tusiwe na mawasiliano na Mikoa mingine. Kwa hiyo, haya masuala mazima yametufanya sisi kuwa maskini na si kwa makusudi. Sasa mnapotuacha katika mipango mingine ya maendeleo tutazidi kuwa maskini mno na kuitwa Mikoa ya

pembezoni na kuitwa Mikoa iliyokuwa nyuma na kuitwa *cinderera*, *cinderera* ni jina la Kingereza na Kifaransa maana yake mtu aliyetengwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana mtuangalie kwa jicho la huruma ili Mkoa wa Lindi nao uingizwe katika *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa katika suala la *Mtwara Corridor*. Katika kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa mmoja naona suala la *Mtwara Corridor*. Suala la *Mtwara Corridor* limeimbwa siku nyingi lakini katika kitabu hiki nimeona sehemu ndogo sana wametaja suala la *Mtwara Corridor.* Sasa suala la *Mtwara Corridor* ni kubwa na linahitaji uangalifu na linahitaji kuendelezwa. Kwa sababu ni suala ambalo limewekwa kwa madhumuni kabisa ya kusaidia Mikoa hii ambayo ipo nyuma. Mikoa iliyokuwa nyuma katika Tanzania tulizungumza sana ilikuwa ni Mikoa ya Lindi, Mtwara, Mbeya, Kigoma, Pwani, Morogoro. *Mtwara Corridor* ilikuwa na madhumni takribani 100 ili kuweza kusaidia maendeleo ya Mikoa hii. Masuala ya umeme, mawasiliano, masuala ya ndege za anga, masuala ya barabara na masuala mengi, maji, madini, uchimbaji wa *gas*, barabara ya Kibiti-Lindi na kadhalika. Lakini sasa katika kitabu hiki wamezungumzia kidogo tu. Tunaomba sana mtusaidie kufufua suala zima la *Mtwara Corridor. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye suala la afya. Jana nilizungumzia kwamba afya katika Mkoa wa Lindi tunakosa mambo mengi, tunakosa wafanyakazi, tunakosa vitendea kazi, tunakosa majengo. Sasa tunaomba sana Mkoa wa Lindi tusaidiwe katika masuala mazima ya vifaa. Kwa mfano, katika Wilaya ya Ruangwa jana nilisema lakini nitarudia. Wilaya ya Ruangwa wenyewe walijitahidi kujenga majengo mbalimbali katika Wilaya ya Ruangwa Mjini pale Kituo cha Kigoma. Wakajenga *theatre room*, wakajenga chumba cha *x-ray*, wakajenga wodi ya watoto na *waiting maternity ward*. Lakini sasa tunakosa vifaa hatuna vifaa, hatuna *x–ray*, hatuna *ultra sound*, hatuna *operation set*, hatuna vitanda, hatuna dawa. Pale yupo Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa analijua hili na amelizungumza hili. Sasa tunaomba sana mtuone katika jicho la huruma ili muweze kutusaidia angalau viwili, vitatu ili niweze kupeleka katika Hospitali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Ruangwa inatumiwa na Wilaya sita. Upande wa Lindi Vijijini kuna Kijiji cha Namangale, upande wa Nachingwea kuna Kijiji cha Mtimbo, wanaita Mtimbo Nachingwea. Wilaya ya Kilwa Nanjilinji inakuja pale na upande mwingine kuna Nanganga, Mkoa wa Mtwara. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba Wilaya sita zinatumia Hospitali hii ya Ruangwa. Tulistajabu mwaka 2004, Wilaya ile katika Jangwa la Sahara ilikuwa ya kwanza kuwa na vifo vya watoto wengi. Hii ni kwa sababu dawa zinazopelekwa pale hazitoshi, zinatumiwa na Wilaya sita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana muiangalie Hospitali ya Ruangwa na muipe vifaa ili nayo iweze kutumika na majirani wa zile Wilaya sita ambazo nimezitaja. Hiyo ilikuwa ni afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika afya suala la ulaji chumvi, maana yake katika afya kuna vitendea kazi, kuna madawa, kuna kula vyakula bora. Kuna kitu kinaitwa chumvi unaweka kwenye mboga na vyakula mbalimbali. Chumvi tunayotumia Tanzania karibuni nyingi inachimbwa ukanda wa bahari. Sasa ile chumvi inayotolewa shambani kuuzwa huwa mara nyingi madini yanayowekwa mle ndani, siyo wengi wanaweka madini. Kwa kawaida unaambiwa ni lazima kwanza uweke madini ndipo uuze, lakini ni wachache sana wanaweka madini katika chumvi, wanaiuza vile vile bila kuweka madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiuza chumvi bila madini maana yake watu wanaumwa *goitre*, watoto wanalemaa miguu. Kwa hiyo, suala la madini kuwekwa katika chumvi ni muhimu sana. Tungeomba Serikali iwaangalie wenye mashamba ya chumvi ili waweke madini. Pili na wao wapate pembejeo, madini yanauzwa bei kubwa sana na hivyo kusababisha wengi kushindwa kupata madini. Naomba Serikali iwe na mpango maalum wa kuwawezesha wakulima wa chumvi ili nao wapate ruzuku ya madini, wawe na Bodi yao ili waweze kupata mahali pa kusemea chumvi hiyo, kwa sababu chumvi nyingi sana karibu asilimia 40 ya chumvi ya Tanzania inauzwa sehemu mbalimbali nje ya nchi. Kwa hiyo, tafadhali sana tunaomba chumvi nayo iwe na bodi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala lingine la utalii. Lindi tumebahatika kuwa na vivutio vingi vya utalii. Naomba sana ndugu zangu wananchi kokote mnakonisikia mje Lindi kutembelea, Lindi kuna mambo mengi sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, muda wako umekwisha.

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nitazungumza siku nyingine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa sawa utazungumza siku nyingine safi.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii adimu ili nami niweze kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri ambayo inakidhi matarajio ya maendeleo ya Watanzania walio wengi. Mheshimiwa Waziri Mkuu hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea kwanza, naomba niunge mkono hoja. Naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, chini ya Mheshimiwa Dokta

Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuweza kuukumbuka Mkoa wa Kigoma ambao ulikuwa umeachwa nyuma muda mrefu, lakini sasa tumeweza kukumbukwa na sasa tunaanza safari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu muda mrefu sana tulikuwa tumefungwa, tulikuwa kisiwani. Lakini sasa tumefunguka kwa sababu sasa barabara zimeanza kutengenezwa. Sasa hivi barabara zimetengenezwa, aliyekwenda Kigoma miaka 2003/2004 akienda leo atashangaa anaweza akafikiri kwamba si Kigoma labda pengine amefika Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zilizotengenezwa katika Mji ule zimeufanya Mji wa Kigoma, uweze kuwa na mandhari nzuri sana. Kwa hiyo, ninazo sababu za kusema ahsante kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM imetekeleza ahadi iliyoitoa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 – 2010, barabara ya Mwandiga Manyovu imekamilika, barabara ya Kigoma, Kidahwe, Uvinza, Malagarasi inaendelea kutengenezwa. Mwezi wa tano nilipokuwa nikifanya ziara Mkoani Kigoma katika Wilaya zote nne, nilipita kufanya mikutano, nikawa naongea na wananchi na kila nilipokuwa nikimaliza kuongea na wananchi nikimaliza niliomba waniulize maswali, maoni na maombi. Kila aliyekuwa anasimama alikuwa ananiuliza kuhusu barabara ya Kigoma, Kasulu, Kibondo, Nyakanazi. Lakini kwa kupitia bajeti hii naishukuru sana Serikali ya CCM imeweza kujibu maswali niliyokuwa naulizwa na wananchi wa Kigoma, Kasulu na Kibondo. Naishukuru sana Serikali yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zote zile zilikuwa zinatengenezwa lakini walikuwa hawajaridhika. Maana yake wao barabara ya Kigoma, Kasulu, Kibondo, Nyakanazi ndio barabara inayounganisha Wilaya zote za Mkoa na ndio barabara inayotumika kusambaza zana za kilimo kama pembejeo kwa ajili ya kupeleka katika Wilaya zao kwa ajili ya kwenda kupeleka mashambani. Kwa hiyo, wamefurahi sana kuona kwamba barabara hii imekumbukwa, imetengewa fedha. Naishukuru sana Serikali, najua nikirudi nyumbani nitarudi kifua mbele, nimepata majibu ya kwenda kuwaambia kwamba barabara ya Kigoma, Nyakanazi imetengewa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisemee umeme, katika Ilani ya mwaka 2005/2010, Ilani iliainisha mambo yatakayofanyika. Kati ya mambo ambayo yaliainishwa katika Ilani ile ni pamoja na Miji Mikuu ya Wilaya, kupelekewa umeme. Sasa Mji wa Kibondo, Mji wa Kasulu tayari jenereta zimeshafungwa. Naishukuru Serikali ya CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabisa, muda si mrefu kwa sababu ni juzi tu nimeongea na Mheshimiwa Waziri, amenihakikishia kwamba mwezi ujao mwishoni umeme utawaka. Nguzo tayari zimeshasimikwa, kilichobakia ni nyaya ambazo zinamalizika kutambazwa. Kwa hiyo, naamini kwa sababu Serikali ya CCM iliahidi na inatekeleza umeme utawaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie reli. Reli ni mhimili muhimu sana kwa Taifa letu la Tanzania lakini kwa Mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi na Mwanza, reli ikikwama wananchi wa Mikoa hii wanapata tabu sana. Wanashindwa jinsi ya kusafiri, uchumi unakwama hawezi kujisaidia kwa lolote kwa sababu ndio njia kubwa inayowasaidia kusafirisha mizigo, usafiri kwa bei nafuu. Bei ya basi kutoka Kigoma mpaka Dar es Salaam ni shilingi 55,000 lakini kwa njia ya reli ni shilingi 20,000. Kwa hiyo, Watanzania walio wengi reli ni msaada kwao. Pamoja na mafanikio tuliyoyapata naomba sasa kilio hiki cha reli, Serikali iweze kutusaidia. Nina imani itatusaidia kwa sababu mwanzo ni mzuri tayari, tumeshaona mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali ya CCM kwa kutupatia Wilaya tatu, tumepata Wilaya Kakonko, Buhigwe na tumepata Uvinza na juzi tu tumepata mamlaka ya Mji Mdogo wa Kasulu. Naishukuru Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapopanua wigo ndio hatua ya kuelekea kwenye maendeleo. Sasa Wilaya zote mpya nilizozitaja tayari zime-*qualify*, naomba nazo kupitia Mpango wa *REA* zipelekewe umeme mara moja. Lakini vile vile kuna vijiji ambavyo vinazunguka miji hiyo ya Kibondo na Kasulu, navyo naomba vipelekewe umeme kwa kupitia Mpango wa Umeme Vijijini. Kwa mfano, kuna Kijiji cha Kabanga ambacho kijiji hicho kuna hospitali, kuna Chuo cha Uliamu, kuna Chuo cha Uuguzi, kuna kituo kinachowatunza *albino*. Kwa hiyo, naomba umeme huo nao uweze kuwafikia watu wa vijiji hivyo ili nao waweze kunufaika na matunda ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vipo Vijiji vya Helujuu, Vijiji vya Nyumbigwa vyote hivyo navyo vinahitaji umeme kwa sababu tatizo la maji wakati mwingine bila kupata umeme hatuwezi kupata ufumbuzi. Lakini tutakapopata umeme wa kuweza kwenda kwenye vijiji vile tayari tutaweza kupata ufumbuzi kwa sababu tutapata mashine za kuweza kupandisha maji. Tunaomba Serikali itatue tatizo hilo haraka iwezekanavyo tutakapokuwa tumemaliza kufunga mashine Mjini Kasulu na Kibondo lakini kupitia *REA* nako vijijini uende. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri mmoja kupitia Wizara zako Mheshimiwa Waziri Mkuu, wanaweza wakapunguza hela kidogo kidogo kwenye Wizara, wakipunguza hela kidogo kidogo kwenye Wizara tunaweza tukapata *solar* tukazipeleka kwenye vijiji, tukapeleka kwenye shule zetu. Tunaomba hilo nalo wakati mwingine mliangalie kwa sababu hata kama tukisema kuna mpango wa *REA* bado kutakuwa na vijiji vingine ambavyo viko mbali ambavyo havitaweza kufikiwa. Lakini mkipunguza kidogo kidogo kwenye Wizara zenu mkaweza kununua umeme wa *solar* utaweza kusaidia shule zile ambazo ziko mbali, shule za Kitanga na shule ambazo ziko Kagerankanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye kilimo. Mkoa wa Kigoma ni kati ya Mikoa sita ambayo imeainishwa kwa ajili ya kuzalisha chakula. Naomba Mkoa huo uangaliwe kwa jicho la huruma sana. Tuko mbali lakini tuko karibu kama Serikali ikiamua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba kupitia Bunge lako Tukufu *population* ya watu imeongezeka, ardhi imekuwa ndogo, watu hawana sehemu ya kulima, watu walio wengi ukienda kwa mfano, Jimbo la Kasulu Mashariki, watu hawa karibia nusu nzima wamepakana na hifadhi. Kwa hiyo, hawana sehemu ya kulima. Naomba Serikali irekebishe sheria ili muweze kuongeza sehemu ili watu waweze kupata sehemu ya kulima, maana yake tutakaposema kilimo kwanza na huku hakuna maeneo ya kulima hatutaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mipaka iongezwe kwenye hifadhi ile ya Kagerankanda kwa sababu wananchi wanateseka sana, hawana sehemu ya kulima, ni juzi tu walikuwa wameambiwa kwamba mwisho wa kuvuna mazao yao iwe tarehe 21 Juni, 2011, lakini tukamlilia Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI akatusaidia, akapiga simu, wakaongeza mpaka mwezi wa nane, wananchi wawe wameondoa mazao yao kule mashambani ili waweze kuwa wameyafikisha majumbani kwao, waondoke kule, wasiondoke kule kwa fimbo, lakini naomba wapime ardhi, wananchi waongezewe wapate sehemu ya kulima ili waweze kukidhi mahitaji yao.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna zao hili la tumbaku. Wananchi wanalima zao la tumbaku, lakini sasa kila mwezi bei ya masoko inabadilika badilika, naomba basi, kama Serikali inaona bei ya tumbaku haiaminiki, itangazie wananchi waache kulima zao hilo ili wasipoteze muda wao, wasilime na huku wakakosa masoko. Naomba Serikali iweze kusema mapema ili wakulima waweze kuamua kama wanashiriki kilimo hicho au hawashiriki kilimo hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Kilimo kwa kuweza kuhamasisha ununuaji wa pamba. Ni juzi tu wamefanya uzinduzi katika Kijiji cha Kanyonza, wamekwenda kuzindua kampeni ya ununuaji wa pamba na tayari wapo watu ambao tayari wamesema kwamba watanunua pamba hiyo. Naomba Serikali iweke msukumo katika Wilaya zile zinazolima pamba, ziungane na hawa watu watakaonunua pamba ili Serikali iweze kuwapa mikopo wananchi waweze kulima na hatimaye waweze kuuza pamba. Lakini vile vile wale wawekezaji wanasema wakifikia milioni tano wataweza kujenga viwanda, naomba Serikali iharakishe kupeleka umeme ili wale wawekezaji watakapokuja kuwekeza viwanda au kuweka *Ginnery* wasikose umeme ili wananchi waweze kujiinua kiuchumi, lakini pia ajira ziweze kuongezeka, vijana waweze kupata kazi kupitia kilimo cha pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie afya. Katika Wilaya ya Kasulu walipopita wakaguzi juzi wamefunga *theatre*, lakini mpaka sasa hivi hospitali wamepata msaada kutoka *CBG* wameanza kujenga *theatre* hiyo. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu Serikali iweze kuongeza pesa ili jengo hilo liweze kukamilika mara moja, wananchi wasiendelee kupata shida sana kwa sababu mpaka sasa hivi *theatre* pale haifanyi kazi, wananchi wanachukuliwa kwenda kufanyiwa *operation* katika hospitali ya Kabanga. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu, pesa zipelekwe mara moja kule Kasulu kusudi *theatre* iweze kukamilika, wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina kilio kingine, Mkoa wa Kigoma tuko pembezoni, hatuna Hospitali ya Rufaa. Mheshimiwa Rais alipokuwa anapita wakati wa kampeini alisema kwamba Hospitali ya Mkoa wa Kigoma ile ya Maweni itapandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa, naomba kupitia Bunge lako Tukufu hospitali ile iweze kutengewa pesa ili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wako, sasa nitamwita Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Lucy Owenya.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kwa heshima kabisa na kwa unyenyekevu wa hali ya juu kwa hotuba zote mbili zilizotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza nimshukuru Mungu ametupa fursa na afya njema, tunajadili haya mambo tukiwa na afya njema, Bwana Yesu apewe sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vile vile kuishukuru familia yangu, wapiga kura walioniwezesha kurudi kwenye Bunge hili na kujiunga na watu mahiri. Naomba vile vile niwashukuru viongozi wa Mkoa wa Kigoma, Wilaya, Tarafa na Kata zetu kwa sababu wote tunafanya kama timu moja. Lakini pili, niupongeze uongozi mzima wa Bunge letu, kuanzia kwa Spika, Naibu wake na uongozi mzima, naridhika na utendaji wenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nishukuru waliotoa mada Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mheshimiwa Mkuchika Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Majaliwa, wote wamefanya kazi nzuri. Labda niende moja kwa moja kwenye hotuba ambayo imetolewa na Ofisi hiyo. Ukiangalia kwenye jedwali, tuna upungufu mkubwa sana wa madarasa nchi hii, tuna upungufu wa nyumba za walimu na ukiangalia kwenye takwimu, tuna upungufu wa nyumba za walimu karibu laki mbili (200,000) tuna upungufu wa madarasa 112,722, tuna upungufu wa madawati nchi hii milioni 1,327,000. Sasa nilikuwa najaribu kuangalia bajeti hii, nikawa naona kweli haiwezi kuyamaliza matatizo yote haya. Sasa nasema hivi au na-*suggest* kwamba, kwa kweli lazima hili sasa tulivalie njuga na Mikoa huenda tuanze harambee kwa sababu kwa bajeti hii iliyopo hatuwezi kumaliza na hivi vijana wetu wataendelea kukaa chini. Labda tuongeze tozo kwenye biashara ambazo tunazo kwenye Mikoa yetu, kwa bajeti hii sioni kama tunaweza kukidhi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, nizungumzie ajira. Nimeona tena kwenye ndani ya hotuba yake, katika walimu waliopangiwa kwenye vituo vyao vya kazi, watu elfu 9,055 lakini karibu watu 2,081 wa shahada na stashahada hawajaripoti. Sasa kwenye ripoti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mkuchika hawajatuwmbia hawa 2,081

wamekwenda wapi na huu upungufu uliopo watauziba vipi na kwa kuwa walikuwa wamepangiwa na mishahara yao iko wapi. Sasa ni vizuri Serikali itwambie, hawa watu 2,081 watakuwa wamekwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu maisha bora kwa kila Mtanzania. Asilimia 70 ya Watanzania wako kwenye kilimo, naiomba ofisi au Serikali yote kwa ujumla kwamba Kigoma ni eneo la wakulima na najaribu kujiuliza kwamba, ule msukumo pamoja na pembejeo na juhudi zote tulizozifanya, nafikiri hawa wanaokuwa wanafanya *practicle* labda kwenye Vyuo vya Kilimo, Sokoine na vyuo vingine vya kilimo, basi Kigoma tunawahitaji waje wafanye *practicle*, twende nao mashambani watuoneshe namna ya kulima vizuri. Sasa sijui hizo *practicle* huwa wanakwenda kuzifanyia maofisini au wanafanyia kwenye mashamba. Kwa hiyo, nawaomba kwani Kigoma tunawahitaji waje watufundishie vijana wetu, akinamama na vikundi vingine ili tuweze kuzalisha kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ahadi za Rais. Rais ni mtu mkubwa, Rais ndiyo Mkuu wa Nchi na ndani ya Bunge letu hili nimeona Wabunge wengi wakilalamika kwamba ahadi za Rais hazitimizwi na sasa sioni haja hata ya kuuliza au Wabunge kuuliza. Nataka kuishauri Serikali iorodhoshe ahadi zote za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizozitoa wakati wa kampeni au mahali popote pale, tuwe na kitabu ambacho kinaainisha alichokiahidi ili tujue hiyo ahadi itatekelezwa lini na kwa bajeti ipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna haja ya kuwa tunauliza maswali kwamba Rais aliahidi hivi hakijatekeleza, tugawiwe, tuwe na mtu Mkoa huu aliahidi hiki, mipango hivi, hatuwezi kuwa tunakuja kuuliza ahadi za Rais hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye amani ya nchi. Tafsiri nyingi zimetolewa, lakini nataka tu nione kuna watu wanajadili amani wanailinganisha na utulivu. Nafikiri Serikali au chombo chochote kwa sababu hata kwenye kampeni zetu huko, watu wengine wanapotosha, wanasema nchi hii haina amani kwa sababu watu hawana kipato, nchi hii haina amani kwa sababu watu hawana ajira, nchi hii haina amani kwa sababu Polisi wamefanya kazi yao vizuri. Sasa amani na hivyo vitu nafikiri haviendani. Kwa hiyo, naona kwamba, watu watafsiriwe amani maana yake ni nini ambayo imeasisiwa na Viongozi wetu kutoka Marehemu Baba wa Taifa, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Mwinyi na sasa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, wote wameenzi amani, sasa hawa wanaobeza amani tungependa tafsiri ifike kwao vizuri ili waweze kuielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kumbukumbu za viongozi. Kumbukumbu za viongozi kwenye kitabu cha Waziri Mkuu wametenga milioni mia moja kwa ajili ya kuandaa sehemu za mazishi za viongozi wakubwa. Silibishii hilo, nafikiri sasa iko haja ya vijana wetu au kuwa na kumbukumbu za viongozi wetu ambazo huenda nyingine zikawa zinabandikwa ndani ya maofisi ya Serikali, mashuleni, zile historia zao ziweze kutunzwa. Akina Marehemu Kawawa wana historia ndefu, lakini vijana wetu huko mbeleni hawatawezi kuzitambua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina Karume ni vizuri sasa hizi nazo tutenge bajeti kidogo ili tutunze historia za hawa, ziende mashuleni kama ni sekondari kwenye ofisi ya Mwalimu Mkuu ziwe zinatunzwa pale, ziwe *framed* kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijielekeze Mkoa wa Kigoma. Kwanza nikubaliane na dada yangu Mheshimiwa Josephine kwa yote aliyoyasema, naomba niungane naye mkono mia kwa mia kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaelekea miaka hamsini, Kigoma sio sehemu ya sisi kukaa tunalalamika kila siku. Kigoma tunataka kubadilisha mtazamo kwamba sio watu wa kulalamika kila siku, tunakwenda sasa kuandika historia ya miaka hamsini. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nafikiri Ofisi ya Waziri Mkuu kama Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Bunge, naomba historia ya Kigoma unapoanza kuiandika kwenye risala haya mambo usiyasahau. Mheshimiwa narudia tena, Mheshimiwa Waziri Mkuu haya mambo ya Kigoma utakapokuwa unaandika hotuba usiyasahau. Kwanza kushukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba mtandao wa barabara za lami ambazo sasa nyie kama Serikali mmeziahidi zitakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa vilevile naomba nitumie nafasi hii, tumepewa taarifa kwamba, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete atakuwa Kigoma kuzindua baadhi ya barabara na daraja la Malagarasi, naomba nitoe wito kwa Watanzania walioko Kigoma wajitokeze kwa wingi wamlaki kipenzi Jakaya Mrisho Kikwete ambaye anakuja kuzindua haya mambo makubwa kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete tutamuingiza kwenye historia yetu watu wa Kigoma, naomba nimtangazie kwamba, ataingia kwenye historia kama mtu aliyeamua kwa dhamira kabisa kuona kwamba Kigoma ilikuwa imefungwa, sasa anaifungua. Wizara ya Ujenzi, mliyoyaahidi msimwagushe Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Mizengo Pinda Waziri Mkuu anauheshimu Mkoa wa Kigoma na anapenda uendelee, naomba msimwagushe. Wizara ya Uchukuzi mambo ya ndege, Kigoma sasa hivi hatuna ndege inayokwenda na juhudi nazisikia mnazifanya, mambo ya reli, bandari, Wizara ya Uchukuzi naomba msituangushie historia yetu. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa niaba ya taasisi zake zote naomba msituangushie historia ya watu wa Kigoma ambayo Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete sasa anaamua kuileta. Asubuhi hii tumeambiwa tunaunganishiwa umeme wa *grid* kutoka Nyakanazi, Kibondo, Kasulu mpaka Kigoma kuelekea Mbeya, naomba msituangushie historia hiyo. Tunaposema miaka hamsini Kigoma tuna kurasa zetu kumi na tano, basi haya mambo yatamkwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametaja mwenyewe amejibu kwamba kupitia *REA* tutatoa umeme wa Kigoma mpaka Manyovu ili watu wale waweze kuwa na umeme, ndugu zangu kwa watu ambao hawajawahi kufika Kigoma kwenye Jimbo langu la Manyovu au Majimbo mengine tuna nyumba nzuri sana. Nyumba zetu kuanzia mwaka 1990 hakuna mwenye nyumba ya kubabaisha, zote zilijiandaa kupokea umeme, kama mtu anafikiri Kigoma kaibeza asije akafanya hivyo, afike aone watu

wamejenga nyumba kwa kujiandaa kwa ajili ya kupokea umeme kwenye nyumba zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa upande wa utawala, Mheshimiwa Josephine amesema vizuri, ameishukuru Serikali kwa kutupatia Wilaya na mimi kama Mheshimiwa Obama naishukuru Serikali imeweza kutupatia hizo Wilaya. Sasa tunaomba zianze kwa sababu nayo lazima muiweke kwenye historia yenu ya hotuba ya miaka hamsini ya Mkoa wa Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapokuwa tumepata umeme na maji kwenye vijiji vyetu ndipo tutakapoweza kuiweka vizuri na nina imani kwamba Wizara ya Maji nayo inajiandaa vizuri na sasa hivi katika vile vijiji kumi ambavyo mmekuwa mkisema kwamba ni vya *World Bank*, ile miradi kwa kweli inasuasua, nimekwenda pale Wilayani wananiambia fedha za maji zimefika, lakini mkandarasi bado wana vile Viingereza vyao vya upembuzi na uyakinifu ambavyo vinachukua muda mrefu, sasa sijui vile vitu havina wasomi wa kutosha ili waweze kufanya haraka. Upembuzi yakinifu umezidi kuchukua muda mrefu, tusingependa watu wa Kigoma kuyaona hayo, sasa tunataka kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wengine kuwaombea Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji, kweli wanafanya kazi nzuri, wapewe hela inayowastahiki na wao wajione kama wako duniani. Kigoma kwa wale ambao hawaijui, inalima kahawa sana, ukianzia Jimbo la Kigoma Kaskazini kwa Mheshimiwa Zitto, ukitoka kwa Zitto unaingia kwa Obama pale Manyovu, ule ukanda wote ni ukanda wa kahawa na sasa hivi bei ya kahawa kule ndugu zangu, ni elfu nne mpaka elfu sita, kwa hiyo watu wanapata mazao yao vizuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, mchangiaji wetu anayefuata sasa ni Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa na Mheshimiwa Mtemvu kama nilivyosema ajiandae.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na nashukuru Mungu inakuwa mara yangu ya kwanza kuchangia tangu niingie Bunge hili. Nataka kutoa shukurani nyingi kwa familia yangu na watu wote ambao waliniwezesha kwa kila hali mpaka nikafika hapa kuwa Mbunge. Nakishukuru Chama cha CCM kwa kupitisha jina langu. Namshukuru Waziri Mkuu kwa kutupa msaada wa maafa kwa wakati wake. Kusema kweli Jimbo la Kilombero lilipata matatizo makubwa sana, maafa makali ya mafuriko, lakini sikutegemea, namshukuru Mungu, Ofisi yake ya Waziri Mkuu wetu inafanya kazi vilivyo. Ilileta misaada kwa wakati na

imetosheleza na mpaka sasa hivi bado misaada iko mingi kwenye ma-*godown* bado tunagawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mkuu wa Mkoa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, nashukuru watu wote waliochangia kwa hali na mali. Nashukuru Kamati ya Maafa ya Wilaya ambao walitekeleza vizuri mambo yote ya kupeleka vyakula na vitu vingine. Nawashukuru wanajeshi ambao magari yao yalivumilia barabara mbovu ya kupeleka chakula sehemu za Mbingu na Mofu. Kwa imani yangu najua Watanzania wote ni waungwana na waaungwana wana maadili safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nakuja kushangaa naona kama tunatoka katika uungwana tunakwenda kwingine. Kwa sababu lugha tunayotumia hapa Bungeni inaleta mfano mbaya kwa vizazi vijavyo ambao sasa wanatuangalia. Naomba kitu hiki tukirekebishe sisi ni waungwana. Muungwana yoyote huwa anafuata maadili. Napenda kusema kwamba Tanzania siyo maskini, Tanzania ni tajiri sana. Hizi bajeti zetu tunazopanga kama kweli tuna moyo na sisi ni waungwana hasa, Tanzania isingekuwa na tatizo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa tunafuata kwa sababu hela nyingi kwa mfano, zinakwenda Wilayani kwenye Halmashauri na katika Halmashauri zetu, hela nyingi zinapotea, lakini hakuna hatua za maana zinazochukuliwa. Wale wangekuwa wanakamatwa na wanapata *hush punishment* halafu wananyang’anywa au wanachukua vitu vyao vyote ambavyo wameiba, vinauzwa, sasa hivi Halmashauri zetu na barabara zetu zingekuwa kama Ulaya. Lakini tunabadilisha maadili tunakwenda kushoto halafu tunalindana, mtu anaiba Mwanga anapata *transfer* anakwenda Njombe. Hakuna hatua zinazochukuliwa, hicho kitu kinatuangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilombero ni Jimbo oevu, ina maana kwamba ni Jimbo ambalo hata jiwe ukipanda linaota, watu wanasema. Lakini miundombinu yake mingi ni mibovu hasa barabara, kama barabara ya kutoka Ifakara kwenda Mlimba, Mlimba kwenda Taveta. Hizo barabara ni mbovu na kutoka Taveta kwenda Tanganyika Masagati. Lakini leo hii utashangaa kuona kwamba, Kilombero kuna Tarafa inaitwa Uchindile haina muunganisho kabisa wa barabara kutoka Ifakara, inabidi utoke Ifakara uende Mikumi, uende Iringa, upite Njombe ndiyo uje Uchindile. Pia hakuna barabara ya kutoka Mlimba kwenda Uchindile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Ifakara mpaka Mlimba kila mwaka inajengwa, Serikali inapoteza pesa nyingi sana kwa sababu barabara hii kila mwaka inapatwa na mafuriko halafu inabomoka tena na watu tena wanatoa misaada na wanaijenga tena. Kwa hiyo, tunafanya kazi hiyo hiyo kila mwaka. Naona kama tunapoteza pesa nyingi sana za Serikali. Kama kuna *contractor* mzuri anaweza kupatikana, tunaomba hata mtujengee kwa changarawe, lakini liwekwe tuta kubwa na sehemu za *drainage* ili maji yaweze kupita kusudi wakati wa mafuriko kusiathirike. Kwa

sababu barabara hii inaleta mazao mengi kutoka Mlimba, Mbingu na Masagati, yote yanaletwa Ifakara. Kwa hiyo, hii barabara ni ya maana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waangalie madaraja, kama unataka kwenda Tanganyika Masagati, mkifika abiria wote mnashuka, gari inapita peke yake, daraja linatingishika hivi na hapo chini kuna mamba siyo mchezo, ukitema mate yanadakwa. Sasa barabara kama hizo na kule kuna mbolea, kuna matunda, wawekezaji wanapenda kulima mipira Tanganyika Masagati, Tanganyika Masagati ndio kuna kilimo cha mpira, lakini watu hawawezi kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hakuna simu Masagati, inabidi mtu akiwa na shida awe na nguvu ya kupanda kwenye kilima, juu kileleni ndiyo anaweza aka-*communicate* na mtu yoyote. Kwa hiyo, tunaomba Serikali na Ofisi yake Mheshimiwa Waziri Mkuu vitu hivyo viangaliwe kwa makini. Waziri Mkuu nakumbuka aliwahi kuja siku zilizopita. Kuna barabara ya Chita-Melela ambapo wakati wa masika ni bahari huoni kitu. Halmashauri haina fedha za kuweza kujenga barabara hiyo. Tunaomba barabara hizi zichukuliwe na Mkoa kwa sababu Halmashauri haina hela. Barabara hizi ni barabara ya Chita-Melela-Mofu na Mawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Kilombero ni wakulima, wanalima sana mpunga, ndizi na matunda. Lakini wakulima hao wanatozwa sana na hivyo kusabisha bei kuwa juu. Kuna *gate* Idete, wakulima wa kutoka Mlimba na Mbingu yenyewe na sehemu zingine za juu wakipita pale gunia moja la mpunga wanatozwa Sh. 1,000/= kwenye *gate*. Sasa nashangaa Wilaya hii ya Kilombero ina ma-*gate* mawili, *gate* la Idete na *gate* la Kidatu. Sasa mtu analipa *gate* la Idete lakini pale ukivuka *gate* la Idete kuna wakulima wengine ambao wanachukua mipunga yao wanakuja Ifakara hawalipi hii Sh. 1,000/=. Kwa hiyo, unaona kabisa wananchi wanaotoka sehemu za Mbingu na kutoka Mlimba pale wanaumia zaidi.

**TAARIFA**

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Mheshimiwa anayezungumza taarifa kwamba mwaka 2002, Serikali ilitunga Sheria inaitwa Halmashauri za Wilaya Kufuta Vizuizi Vinavyotumika Kutoza Ushuru wa Mazao, Tangazo la Serikali Na. 130 la mwaka 2002 na Sheria hiyo ilitungwa na aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI wakati huo Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi. Kwa hiyo ma-*gate* anayosema yapo pale kinyume cha Sheria. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Nashukuru kama ipo, naomba hiyo Sheria itumike. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mchangiaji sijakuruhusu kama uipokee au vipi.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

**MWENYEKITI:** Sasa sijui wewe umeipokea hiyo taarifa na sijui kama ina ukweli wowote. Sasa kama umeipokea uikubali au kama haujaipokea ni juu yako wewe.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Kama ya ukweli nimeipokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo *gate* ni usumbufu mkubwa sana. Tumelipigania na limekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wa Kilombero, tunaomba litolewe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu, Uchindile kuna shule toka imeanzishwa hajafaulu hata mwanafunzi kutoka darasa la saba kwenda darasa la tisa. Tatizo ni walimu na vitabu, shule ile ni kama imesahaulika. Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu, ilishughulikie suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kiwanda cha Kilombero pale panafukuta na Wazungu wanasema *prevention is better than cure.* Tunaomba twende mapema tukasuluhishe pale, pana matatizo panafuka. Kampuni ya Kilombero ilibinafsishwa ikawa inaitwa Ilovo, wakati wa ubinafsishaji huo kuna shule waliojenga wananchi kwa jasho lao, walichanga wakajenga shule. Lakini wakati wa kubinafsisha hiyo shule ikawa imeingia katika mkumbo huo huo lakini ile kampuni iliyochukua walikuwa hawana shida na hii shule. Mshauri wao aliamua kwamba hii shule ikodishwe, ikakodishwa kwa KKKT, nafikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini KKKT anatoza ada kubwa sana, hiyo shule inaitwa Malecela. Sasa wananchi wa Kilombero wanasema shule walijenga kwa jasho lao, kwa nini ile shule wasirudishiwe wenyewe kusudi watoto wao wasome, watoto wa wakulima wapate elimu pale. Ikishindikana ile shule basi irudishwe kwa Halmashauri kuliko kuwapa Kilombero wao wanaikodisha na wanapata faida tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, *out growers* wa Kilombero ambao ni wakulima wa nje wanalima miwa kwenda kuuza katika Kiwanda kile. Mwenye Kiwanda anawakata 3% ya mapato yao, anasema ni mchango wa kupanua kiwanda chake. Kama hawataki hawezi kununua miwa yao. Sasa huo ni unyanyasaji. Kwa sababu angewaambia anawakata asilimia tatu na wao wanakuwa kama wabia ingekuwa afadhali. Lakini anawakata halafu hawapati chochote ila yeye kiwanda chake kiongezeke. Naomba Waziri anayehusika akiwa na nafasi tuwe na mimi, twende tukawaone wafanyakazi wa pale, kuna fukuto moja baya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nataka kuwasemea wana michezo. Mimi binafsi nilikuwa mchezaji wa zamani wa Simba na *Pan Africa*. Wachezaji mpira wa nchi hii ambao wamechezea Taifa hawathaminiwi. Wako wengi ambao hali zao ni mbaya na zamani sisi tulikuwa tunacheza mpira kwa kupenda mpira, kwa moyo, hatulipwi kitu, lakini leo wamesahaulika kabisa. Kwa hiyo, hali zao ni mbaya mno.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu. Lakini pili, niwashukuru wapiga kura wangu wote wa TMK kwa mapenzi makubwa ya kunirejesha kwa kipindi cha pili katika Bunge hili Tukufu. Si kawaida TMK kupata vipindi viwili, naamini Mungu akipenda na afya yangu ikiwa njema nitarejeshwa kipindi cha tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshukuru sana Mkuu wangu wa Wilaya, Dada yangu Chiku, kwa kazi nzuri na ushirikiano wa pamoja. Lakini nishukuru viongozi wangu wapendwa wa Chama cha Mapinduzi wakiongozwa na Mwenyekiti na Katibu kwa ushirikiano mzuri wa kufanya kazi pamoja. Lakini niwashukuru Kaimu Mkurugenzi Gasto kwa kazi nzuri kwa kipindi kifupi na naamini wazee mtamwangalia mumpe Wilaya ile ya Temeke ili aweze kutupeleka haraka haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru Madiwani kwa ushirikiano mzuri. Nimshukuru sana mke wangu na watoto wangu. Vile vile nimpongeze Waziri Mkuu na Waziri Mkuchika kwa hotuba nzuri za Bajeti. Niseme naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mambo ya msingi niliyotumwa na watu wa Jimbo la Temeke. Tunalo tatizo la msingi katika eneo la Kurasini, Mtaa wa Kurasini na Mtaa wa Kiungani. Eneo la Kurasini tuliamua, Serikali iliamua liwe ni eneo la utanuzi wa bandari. Wananchi wale kwa nia nzuri kabisa wakakubaliana na Serikali. Mpango ukapita, lakini leo wananchi wale wanapata matatizo makubwa sana, sana. Lakini cha kusikitisha zaidi eneo lile la Kurasini Mabwawani, Waziri Mkuu alitembelea pale tarehe 14 Machi, akasema wale wananchi waliopunjwa walipwe, lakini cha kusikitisha hadi leo wananchi wale hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haitoshi, Rais aliagiza tarehe 29 Oktoba, lakini wananchi wale hadi leo hawajalipwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu ajaribu kuangalia ni namna gani tutakwenda kama viongozi Wakuu wanaagiza, halafu Watendaji hawatekelezi. Katika hili wananchi wa Kurasini wameniagiza, Waziri Mama Tibaijuka ni mgeni, lakini ndiyo analo, ndiye mwenye Wizara, wameniagiza ikifika bajeti yake kama wale wananchi watakuwa hawajalipwa, nihakikishe katika kifungu 1001, naondoa mshahara wa Waziri, siungi mkono bajeti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili hili sisi ambao tulikuwepo katika kipindi cha kwanza liliazimia hapa kuhakikisha nyumba zile za *National Housing* za wale wa kipato cha chini watauziwa kama walivyouziwa Mawaziri na watu wengine zikiwemo nyumba za Chang'ombe, Tandika Maghorofani na Keko Maghorofani. Hadi leo hatujaona msimamo wa Serikali unasemaje. Sasa niseme pia hili siyo la Waziri Mkuu, siku tutakapofika kwenye bajeti ya Wizara ya Ardhi, nitamwomba Mheshimiwa Waziri atoe msimamo kuhusu nyumba zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na Wabunge wote. Wabunge wote nia yao ni nzuri, Waheshimiwa Madiwani wawezeshwe ili waweze kufanya kazi yao vizuri. Lakini mimi niongeze tu kwamba, ule ujira wa mwia tuuboreshe au tuwape mishahara lakini pia wapewe uwezo na wao wa kukopa magari na usafiri mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la msongamano Dar es Salaam. Hakuna asiyejua tatizo la msongamano Dar es Salaam, kipindi kilichopita tulikubaliana hapa na mipango mizuri ya *fly over,* tukawa na mpango mzuri wa *ring road,* ulianzishwa na Waziri ambaye sasa yuko Wizara ya Elimu na sisi tunashukuru mpango ule ulikwenda vizuri ila katikati ukaja mgogoro mkubwa wa masuala ya fidia. Maeneo ya Kigogo, mpango ule ulikwama kwa sababu ya masuala ya fidia.

Sasa mimi niombe sana, nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, chama chetu ni kimoja, Mawaziri hawa wote ni wamoja, pale ambapo anaingia Waziri mwingine akimpokea mwenziwe, basi aendeleze aliyoyakuta na Waheshimiwa Mawaziri ni lazima muelewe kwamba nyie mmetokana na sisi Wabunge, leo mpo kesho na sisi tutakuja! *(Makofi)*

Kwa hiyo, mnapokuwa kwenye nafasi hizo, ukikuta mpango wa wenzio mzuri wa mabango, sema na wenzio. Ukikuta mpango mzuri wa wenzio wa fidia, sema na wenzio, si vyema wewe ukawa hodari kuliko wenzio, tunaomba sana. Kuna watu wanaostahili *Kilwa Road,* tulikubaliana na Waziri Kawambwa na uongozi huo huo, wale watu walipwe, watu wa Kigogo walipwe ili zile *ring roads* ziende kwa kasi, barabara zipitike, lakini sasa hivi watu wamekwama kwa uamuzi wa mtu mmoja; tunaomba uamuzi uliopita uheshimike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme Dar es Salaam. Suala hili linasikitisha, leo mji wa Dar es Salaam watu wanakaa na shida ya umeme kwa siku tatu mpaka nne! Karibu Wabunge wote tuna makazi yetu Dar es Salaam, lakini tunapozungumzia suala la umeme Dar es Salaam, suala la msongamano wa watu hawalioni hili! Sasa sisi tunamwambia Waziri Ngeleja na Waziri Malima, wote hao ndugu zetu kwamba siku ya Wizara yao tunaomba waje na jawabu la umeme Dar es Salaam, la haraka sana; hatuwezi kukubali mpango wa miaka mitano, hamuwezi kutuambia huo umeme wa hakika mwaka 2015, tutaishi wapi? Lakini haitoshi, Zanzibar walikuwa na tatizo la umeme kwa miezi mitatu, leo wamefunga majenereta shida ya umeme Zanzibar unaambiwa kama mgawo ni saa

moja! Malima umesoma Uingereza, unajua majenereta yanakopatikana, kama hamjui niambieni niwachukue nikawaoneshe mtufungie majenereta ya dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi toka tuzaliwe na tupate fahamu zetu pale Dar es Salaam hatujawahi kukaa na kiza na wanasema kwamba haya matatizo kwa kuwa wakubwa kwao hakuna shida hizi kuna majenereta, ndio maana hamyajali! Kwa hiyo, siku ya Bajeti ya Nishati tunaomba tupate jawabu la haraka kuhusu suala la umeme; tumechoka na mipango ya Mheshimiwa Ngeleja ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiri, lipo suala la msingi la Mzee Maulid, alikuwa *TANSORT* pale Uingereza, yule mzee anateseka. Yule mzee alikuwa muaminifu, angekuwa mtu hovyo hovyo angeiba, leo asingelalamika. Anashindwa hata nauli ya kurudi nyumbani, amefanya kazi miaka 41, leo anafika Wizarani anazungushwa na kila mtu anamjua, mpaka Mheshimiwa Rais, anamjua, alivyokuwa Waziri wa Mambo ya Nje alipokuwa akienda anamuona yule mtu, leo anateseka kupita kiasi. Naomba Mheshimiwa Ngeleja yupo, Malima nakuona ndugu yangu, siku ya Bajeti yenu mtupe jawabu la Mzee Maulid, ambaye anaadhirika Uingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana suala la umeme lipate jawabu. Leo Dar es Salaam, tunachangia uchumi wa Taifa 85% hakuna umeme! Viwanda hapa tunaongea hapa uchumi wetu umekuwa kwa 7%, hivyo katika hali kama hii hatuna umeme, utakuwa au utashuka chini? Lazima tuwe na jawabu la haraka, tuwe na maamuzi! Kama haiwezekani hebu tupeni nafasi; tufanye maamuzi mambo yote yanawezekana hakuna kisichowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu mia kwa mia. Nasubiri Bajeti za Wizara ya Ardhi na ya Nishati na Madini. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Aidha, ninazo sababu za kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda na kunipa uhai na afya njema ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuchangia hoja ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda niipongeze hotuba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani, hotuba ambayo ilikuwa imefanyiwa utafiti wa hali ya juu. Ni matumaini yangu kwamba Serikali itaitumia na wala msiogope kwa sababu jana kuna mchangiaji ambaye alikuwa anaibeza hotuba ya Msemaji wa Upinzani, anasema kwamba mauaji yaliyofanywa na polisi sio polisi walifanya. Sisi tumefanya utafiti na tunajua ni mapolisi walifanya, kwa hiyo, asikae kujibu hoja asubiri kwanza, achangie hoja yake na mtoa hoja atajibu hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani hapa mlikuwa na siasa ya chama kimoja ndio maana mlikuwa hamuoni kwamba mnapewa changamoto. Ni lazima mzikubali changamoto, sasa hivi ni siasa ya vyama vingi. Hata kwenye litabu kitakatifu cha Wakorintho II, mlango wa tano, mstari wa 17 unasema, tazama ya kale yamepita sasa tunayaangalia mapya; kwa hiyo, mkubali kwamba siasa ya vyama vingi ni mambo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niombe ombi kwa Waziri Mkuu kuhusu Kitengo cha Maafa. Mkoa wa Kilimanjaro tuna njaa kubwa, kwa sasa hivi mvua hazikunyesha za kutosha, Same Mashariki, Same Magharibi, Mwanga, Hai, Moshi Mjini, Moshi Vijijini mpaka Rombo, wote wanakufa njaa. Cha kusikitisha kule Rombo wale wafanyabiashara wanaouza mahindi wanaishia Himo, hawaendi kwenye soko la Tarakea wala Holili! Sasa napenda kuuliza je, Rombo ni nje ya Tanzania? Tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, waruhusu wafungue ule mpaka pale Himo, waweze kupeleka mahindi kule Holili ili wananchi wa Rombo nao waweze kufaidika wasife njaa, kwa sababu Mbunge wao ameshajaribu kwa kiasi kikubwa kuwatetea wananchi wa Rombo, lakini kuna wanasiasa wanapita kule wanasema Mbunge ndio anayezuia. Naomba wale wa Rombo wanaonisikia sasa hivi wajue kwamba Mbunge wao Joseph Selasini, anafanya juhudi zote kuhakikisha kwamba mahindi yanafika Rombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo naomba nizungumzie kidogo kuhusu amani na utulivu. Ukiwa wa mwisho unasikiliza maneno mengi. Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakiyaandama sana maandamano ya CHADEMA. CHADEMA tumeandamana Mbeya, Iringa, Rukwa, kote huko tumepita hamna amani iliyovunjika, lakini naomba nizungumzie kidogo maandamano ya Arusha. Mimi nilikuwa ni mmojawapo katika yale maandamano ya Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo kilichofanyika Arusha ni cha kinyama. Wananchi hawakuleta vurugu yoyote, mimi nina imani kabisa kwamba polisi ndio wanaotakiwa kuchunga usalama wa raia na sio vinginevyo. Lakini Arusha, polisi ndio walianza kupiga raia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, mimi ninaamini wewe ni Mbunge wa muda mrefu kidogo. Jambo hili limeshakuwa likitokea hapa na limekuwa na majibu *constantly* kwamba suala la maandamano ya Arusha lipo Mahakamani. Kama ulitaka kujenga hoja, basi sio lazima utumie *premise* hiyo, unaweza ukajenga hoja kwa namna nyingine na mimi ninaamini una uwezo mkubwa wa kujieleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge, endelea.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuhusu maandamano ya Arusha, mimi sizungumzii mambo ya kesi iliyoko Mahakamani. Mimi nilikuwa kwenye maandamano yale, polisi walitueleza kwamba tusiandamane, mimi nilikuwa ndani ya gari…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kwa namna yoyote ukizungumzia tu utarataibu wa yale maandamano na matokeo yake na nini, tayari unazungumzia jambo ambalo lipo Mahakamani; huna *style* nyingine ya kubadilisha maelezo yako Mheshimiwa Mbunge?

Nakuomba tafadhali, hebu tuache hilo jambo lililo Mahakamani maana hata chombo hicho cha Mahakama kinalalamika sana kwamba Wabunge tunakiingilia katika shughuli zake. Kwa hiyo, mimi nisingependa iwe hivyo, ninaamini utaweza kunisikia. Endelea Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Naomba nizungumzie hali ya uchafu, ujenzi holela na msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, napenda niipongeze Manispaa ya Moshi na Jiji la Mwanza kwa kushika namba moja katika usafi na utunzaji wa mazingira chini ya uongozi wa CHADEMA. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchafu Dar es Salaam; Dar es Salaam ni kioo cha nchi yetu lakini ukiangalia kwenye ile barabara ya Morogoro uchafu umezagaa kila mahali. Takataka zinatupwa kwenye mitaro ya maji machafu, hata yale magari yanayozoa takataka yenyewe ni machafu, badala ya kuzoa takataka, yanasambaza takataka. Naamini kwamba magari yale yapo kwenye *tender,* basi wale wanaopewa zile *tender* wapewe vigezo vya yale magari. Wahakikishe kwamba yale magari yamefunikwa na wale wafanyakazi ambao wanafanya kwenye yale magari ya takataka wanapewa vitendea kazi kama *gloves* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifereji ya maji machafu ambayo iko wazi; mifereji ya maji machafu imekuwa ndio majalala ya takataka na kule mazalia ya mbu yanakuwa ni mengi. Mimi ningeshauri wayafunike mashimo yale ili kupunguza magonjwa ya kuambikiza kama *typhoid, cholera* na kadhalika ambayo ndio magonjwa sugu katika Jiji letu la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira kule Mikocheni kuna viwanda kama *BIDCO, MMI* kiwanda cha chuma na kiwanda cha dawa cha *Shelys* ambao wamekuwa wakimwaga maji ya sumu kuelekeza kwenye mfereji wa Nyirenda. Je, Serikali inalijua hili? Kwa sababu, maji yale ya sumu yanaathiri ubongo na watu wengi kule wamekuwa kama akili zao haziko vizuri, watu wanasema ni wavuta bangi! Sio wavuta bangi, nafikiri ni ile sumu inaathiri vichwa vyao. Ningependa Serikali iunde Tume wakaangalie ni kwa

nini wawekezaji hawa wamekuwa na kiburi kiasi hicho! Kwa sababu Madiwani wameshaenda pale, Wenyeviti wa Mitaa wameenda pale kuwaelekeza kwamba wasielekeze maji kwenye mfereji ule lakini hawasikii, wanasema wameiweka Serikali mkononi. Sijui kama ni kweli, tunaomba Tume iundwe waende wakahakikishe hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano wa magari katika jiji letu la Dar es Salaam. Tumeona wakati wa mvua msongamano wa magari unakuwa ni mkubwa zaidi! Unakuwa ni mkubwa zaidi kwa sababu zile barabara za pembezoni hazijatengenezwa, tunajua kuna mradi wa magari yaendayo kwa kasi lakini ule ni mradi wa muda mrefu. Lakini kwa muda mfupi, ningeshauri kwamba zile barabara zitengenezwe ili tupunguze msongamano kwa sababu watu wengi wanakuja kwenye hizi *main roads* na hizi barabara za pembezoni zinasaidia sana, ndio maana magari mengi yanaenda kule pembeni lakini kwa sababu ya mashimo madereva wengi wanaogopa kwenda kule pembezoni ili wasiharibu magari yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi holela katika Jiji letu la Dar es Salaam. Sasa hivi maghorofa yanajengwa mengi sana, mimi ningependa kujua je, Dar es Salaam tunayo *master plan?* Na kama ipo, inatumika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema watu wasijenge kwenye *open space*, lakini Serikali imekuwa ndio ya kwanza kuvunja Sheria hii, kitu cha kushangaza pale *Sokoine Drive* Serikali imewapa *Nyerere Foundation* kujenga ghorofa pale na pale ilikuwa ni sehemu ya *parking* ambayo maghorofa mengi yangeweza kupumulia pale! Ni kwa nini Serikali isiwape mahali kama Kigamboni ambako ndio tunasema tunajenga mji mpya, waende wakajenge ghorofa kule badala yake mnawapa katikati ya mji ambako tayari tuna shida ya *parking* katikati ya mji? Mimi ningeshauri muende mkajenge Kigamboni, muwape nafasi kule Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo hilo la ujenzi holela. Sasa hivi imekuwa ni mtindo baa nyingi zinajengwa kwenye makazi ya watu. Mfano, pale Sinza kuna baa nyingi sana zinacheza muziki mpaka asubuhi, watoto wanashindwa kusoma, wanashindwa kufanya *homework!* Kwa hiyo, tunaomba Serikali iingilie kati… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa, ya kwanza hiyo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante natumaini umelinda muda wangu saa ile uliponipa taratibu. Waingilie kati ili waweze kuwazuia hawa wanaojenga kwenye makazi ambayo inaharibu pia maadili ya watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka ningeomba niongelee kuhusu afya. Katika ripoti ya *CAG*, inaonesha TAMISEMI walinunua magari ya kubebea wagonjwa 43 ya shilingi 4,886,000.45/= lakini magari hayo hayajakabidhiwa. Ningependa wakati Waziri Mkuu anajumuisha watueleze je, magari haya yameshakabidhiwa? Kama bado, basi wafanye haraka kwa sababu magari ya kubebea wagonjwa ni tatizo katika Halmashauri zetu. Tumeona kila mtu analalamika, pia kule katika hospitali yetu ya Mkoa wa Kilimanjaro, pamekuwepo na ubadhirifu wa pesa. Hospitali ile wamejenga *theatre* kwa shilingi 400,000,000/= lakini haijatimiza vigezo, ina makabati chini, imejengewa *tiles*, imebidi waibomoe yote na hospitali ile ilikuwa inasimamiwa na *TBA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi wameibomoa yote na gharama za kuijenga hospitali ile zinatakiwa shilingi 700,000,000. Sasa mimi ningependa kujua wale waliosababisha hasara hii, watachukuliwa hatua gani? Au kama ikiwezekana basi Wizara ya Afya au Waziri, waende kule wakachunguze, waunde Tume na waangalie ubadhirifu huu! Ni fedha nyingi sana shilingi 400,000,000 ambazo zingeweza kuwasaidia akinamama ambao tumeona wanakufa kwa matatizo ya ujauzito na watoto. Tumeona katika ripoti kwamba Tanzania ni nchi ya tisa kwa akinamama na watoto kufariki. Japokuwa Serikali imekuwa ikitusaidia sana kuhusu hivi vifo vya akinamama na watoto lakini bado tunaongoza katika vifo hivyo; kwa hiyo, tunaomba Serikali iliangalie hili watusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijagongewa kengele ya pili, naomba niongelee kuhusu Wakuu wa Mikoa na ma-*DC*. Mkoa wa Kilimanjaro kumekuwa kukikaimu, Mkuu wa Mkoa alikuwa anatoka Tanga anakuja Kilimanjaro. Hata Dar es Salaam pamoja na kuwa ni Jiji kubwa lakini kwa muda wote limekaa bila Mkuu wa Mkoa kwa miezi zaidi ya sita sasa, wamekuwa wakikaimu! Mimi naishauri Serikali ikubaliane na sera yetu ya CHADEMA ya Majimbo, tupunguze gharama kwa ku-*allocate* Wakuu wa Mikoa waweze kusimamia Mikoa hiyo na suala la ma-*DC*. Kwa sababu, *DED* ndio wanaofanya kazi nyingi, mimi naona kada hii ingefutwa kabisa, ingeokoa hela nyingi sana za Serikali, ukizingatia tuna ma-*DC* 114, wote wana magari 114, wote wana nyumba 114, wote wanalindwa! Kwa kiasi kikubwa Serikali ingepunguza gharama na tungeokoa fedha nyingi sana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira. Tumeelezwa kwamba kuna wanafunzi zaidi ya 700,060 wanaomaliza vyuo na watakaoajiriwa ni 40,000 tu. Lakini pamekuwepo na *tendency* ya kuongeza mkataba kwa wastaafu na wastaafu ninaowazungumzia sizungumzii wale wa utaalamu ambao ni ma-*engineer*, madaktari au manesi na walimu; nawazungumzia hawa wa menejimenti, kwa mfano Mkurugenzi wa Halmashauri, anaongezewa mkataba wakati tayari ameshastaafu na anapata pensheni! Je, hii si kulipa mshahara mara ya pili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama anaongezewa mkataba ningependa kujua Waraka wa Utumishi wa Umma anaruhusiwa kurudi aendelee na kazi ile ile ambayo alikuwa anaifanya mwanzo na kama mstaafu huyu ameshastaafu na kuna vijana wanaosubiri kuajiriwa, vijana hao watapata wapi kazi kama mtaendelea kuongeza mikataba kwenye ajira ambazo zinaweza zikafanywa na vijana ambao wanamaliza Vyuo Vikuu? Naomba hilo pia liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea kidogo kuhusu utalii lakini nategemea labda wakati wa hotuba ya sekta husika nitapata nafasi. Suala zima la utalii katika Mlima Kilimanjaro pamoja na njia za kupanda mlimani kuna wageni ambao wanaenda kulala kule *crater* sasa *crater* hakuna vyoo, wale wapanda mlima wale ma-*guide* huwa wanapasua zile *glacier* wanayeyusha maji kwa ajili ya kupikia kwa maana hiyo ule mlima unazidi kuharibika mazingira hayatunzwi, kuna vinyesi, ni kumechafuka hapafai kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Maliasili na Utalii isitishe watu kwenda *camp* kule *crater*, kwa sababu hata wakienda *camp* kule *crater* hawalipi fedha ya ziada.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri, Taarifa.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Kanuni ya 64(a) nilikuwa naomba nimpe taarifa mzungumzaji aliyepita kwamba kuhusu suala la usafi na siyo Dar es Salaam tu, Tanzania nzima tulizindua tarehe 12 Februari na Makamu wa Rais kusafisisha majiji na tumeanza, Halmashauri zote tatu zimenunua magari mapya nimeyaona, si kweli kwamba hawana magari wamenunua. Kila Jumamosi ya kwanza ya kila mwezi tunasafisha na si suala la mmoja naomba Waheshimiwa Wabunge wote, tujikite kwenye suala hilo siyo suala la mtu mmoja na katika miji yote ya Tanzania ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sina hakika, lakini *anyway* tuendelee.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu, kwanza kabisa ninamshukuru Mungu kwa kuniwezesha kufika mahali hapa nikiwa mzima, ninaamini kabisa si kwa ujanja wangu wala si kwa akili yangu ila ni kwa neema yake tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri, hotuba ambayo inaendana kabisa na mpango wa maendeleo wa miaka mitano nampongeza sana Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kuzungumzia mambo manne kama siyo matano iwapo muda utaniruhusu. Nitaanza na eneo la wanawake, kwanza kabisa ninaipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kumthamini na kumtambua mwanamke kwa namna ya pekee kwa kuweka mpango wa kusambaza vyandarua vyenye dawa, mpango huu umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto wa chini ya umri wa miaka mitano, ninaipongeza sana sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tena niendelee kuipongeza Serikali yangu kwa mpango mzuri wa kujenga kiwanda cha kutengeneza dawa za malaria, kiwanda hicho kinajengwa Kibaha Mkoani Pwani, ninaamini kabisa kiwanda hicho kitasaidia tena kuchangia kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni *microphone* yangu au labda kuna mtu mwingine, naweza kuendelea nasikika. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Endelea.

**MWENYEKITI:** Endelea unasikika.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana baada ya pongezi hizo kwa Serikali ninataka nizungumzie kidogo kwenye eneo la ugawaji wa dawa hasa kule kwetu Geita. Kule Nyarugusu kituo cha afya cha Nyarugusu kina wakazi ambao wanakadiriwa kufika 46,000 lakini cha kushangaza ugawaji wa dawa, wanagaiwa dawa sawa kabisa na kituo cha afya cha Forwe ambacho kina wakazi wanaokadiriwa 3,000 tu, kwa hiyo, ningeiomba Serikali iangalie upya utaratibu huo, kituo kigaiwe dawa kulingana na *population* ya eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaiomba sana Serikali kupitia Halmashauri iangalie nyezo za usafiri, kwa kweli akinamama vijijini wanateseka sana wanapokuwa wanaenda kwenye vituo vya afya vya kujifungua, wasaidiwe basi hizi nyezo za usafiri. Bunge lililopita nilimuona Waziri Mkuu akinadi pikipiki ya miguu mitatu nikaona pikipiki hizi zingeweza kuwafikia akinamama kule Busolwa, Nyang’wale, Chato na Bukombe, zingeweza kuwasaidia sana kupunguza vifo wakiwa wanaelekea kwenye vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nitapenda kuchangia kidogo haraka haraka ni haya mabilioni ya JK, sidhani kama Serikali imeshakaa ikafanya tathmini kuhakikisha kama kweli haya mabilioni ya JK yaliwafikia walengwa, ninao uhakika kabisa kwamba haya mabilioni ya JK hayajawafikia walengwa kwa sababu masharti yake yalikuwa ni magumu, watu wengi walishindwa ku-*meet* vigezo vya kupata hayo mabilioni, matokeo yake wameyapata watu ambao walikuwa tayari wana mitaji mikubwa, wana biashara kubwa kwa hiyo, nia njema ya Rais wetu ninaamini kabisa haikufikiwa. Hivyo, naiomba Serikali ifanye tathmini upya iangalie ni wapi ilikosea ili haya mabilioni ya JK yaweze kuwafikia walengwa lengo tuweze kufika pale ambapo tulikuwa tumekusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia niipongeze Serikali kwa namna ya pekee sana, kwa kututhamini na kututambua wanawake, ikatuanzishia Benki ya Wanawake, ninaipongeza sana Serikali kwa uamuzi huo na kwa mpango huo. Lakini bado nina wasiwasi na bado nina tatizo kidogo na Benki yetu ya Wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake nimefuatilia nimeona masharti yake hayatofautiani sana na masharti ya Benki hizi zingine za kawaida. Sasa wanawake kweli watanufaika vipi na Benki yao? Niiombe Serikali tena kwa unyenyekevu mkubwa kabisa kama kweli hii benki imedhamiria kuwasaidia akinamama, basi kweli iwasaidie akinamama maana wote tunajivunia kwamba tuna benki yetu ya wanawake, tuna Benki ya Wanawake, lakini wanawake wachache sana wananufaika na hii benki, kwanza ukiangalia benki ipo Dar es Salaam ndiyo Makao Makuu, *fine* tunajua kwamba ndiyo kwanza imeanza lakini basi Serikali iongeze nguvu ili benki iwe na matawi katika mikoa na wilaya ili wanaotaka kukopa siyo lazima wafike Dar es Salaam. *(Makofi)*

La pili, masharti yalegezwe ili akinamama waliopo kule Kamuhanga, walioko kule Nzela basi waweze kukopa na wao wanufaike maana hii ni benki ya kwao ni Benki ya Wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuipongeza Serikali hususan nampongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa uamuzi wake wa kuanzishwa hii mikoa minne mipya ukiwemo mkoa wangu wa Geita, mkoa ambao umeniwezesha mimi leo kuingia katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali kwa uamuzi lakini ninaomba basi hii mikoa ianze. Ninaamini Serikali ina mipango mizuri kabisa na kweli mikoa itaanza kama ambavyo Waziri Mkuu alieleza kuna taratibu tu zinaendelea, ninaishukuru sana. Lakini nikiwa nazungumzia katika huu mkoa wa Geita, nikiangalia katika hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 32 inasema kwamba Serikali itaendelea kuwavutia wawekezaji katika viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya kilimo na kutoa mafunzo ya ujasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishikilia hapa hapa ninaomba kwa heshima kubwa na unyenyekevu mkubwa Geita iangaliwe kwa macho tofauti kidogo. Geita tunaomba wavutiwe hawa wawwekezaji waje Geita watujengee viwanda vya kusindika matunda. Mkoa wetu wa Geita nafikiri unafahamu kwamba tuna umaarufu sana wa kulima mananasi na maembe, lakini mwisho wa siku yale matunda yanatuozea hatunufaiki nayo chochote, tunaishukuru Serikali kwa wenzetu wa Singida walioweza kuwekewa kiwanda ambacho kinatengeneza alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo ukipita hii barabara kutoka Dar es Salaam kupitia Singida kwenda huko Geita kwetu tunaona vijana wengi, tunaona akinamama wengi wanauza mafuta ya alizeti, tena yameandaliwa vizuri kabisa kwa sababu wamewekewa kiwanda. Hivyo, tunaomba basi na sisi watu wa Geita tuwekewe hicho kiwanda, tusindike hayo matunda kama mananasi na maembe yasioze bure, itasaidia sana kuongeza ajira kwa vijana wasizurure hovyo katika hicho kiwanda, akinamama wengi watafanya kazi. Kwa hiyo, mtakuwa mmetusaidia sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa unyenyekevu mkubwa naomba usikie na Waziri wa Viwanda nadhani yuko hapa ninaomba katika majumuisho Mheshimiwa Waziri Mkuu atueleze kwamba wana mpango upi huo wa haraka haraka wa kutujengea viwanda vya kutosha katika mkoa wetu wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika maeneo ambayo yamezungumziwa yana njaa sikuiona Geita, lakini ninaomba niseme tena kwamba Geita njaa ipo, ipo sana ukienda kule Bukombe, kuna kituo cha watoto yatima cha *FTI* kila siku naongea na wale watu, watoto wanakunywa uji, wanashindia uji, hakuna kabisa chakula, isije watu wakadanganyika kwamba Geita njaa hakuna, Geita njaa ipo, tunaomba kama ambavyo mmejipanga kusaidia mikoa mingine basi hata na mkoa wa Geita ukumbukwe kwa chakula, njaa ipo kama ambavyo ipo katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda haraka haraka sipendi kupigiwa kengele, ningependa pia nizungumzie wale watu wanaoishi jirani na mgodi wetu wa Geita. Nimefanya utafiti wangu kidogo mahusiano yaliyopo kati ya mgodi wa Geita na wananchi wanaozunguka eneo lile siyo mbaya lakini kuna tatizo moja mimi nimeliona.

Mimi nimesikitika sana, *population* iliyopo mle ndani ni zaidi ya watu 3,000 kwa hiyo wanakula na wanakunywa mle, ninachoshangaa ni kwamba hata zile mboga za maji zinanunuliwa Kenya, wakati Wasukuma ni wachapakazi, Wasukuma wanaweza kulima mboga za kutosha wakawauzia wale watu mle ndani mgodini, *at least* ile hela ikabaki pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nimesikitika na nimeumia sana sisi Wasukuma tunafuga, tuna ng’ombe, tuna maziwa ya kutosha, maziwa mengine

tunashindwa hata kuyatumia, tunakunywa mpaka tunachoka mengine yanaharibika. Lakini cha ajabu ni kwamba hawa majirani zetu wananunua maziwa Kenya na *South Africa*, ningeomba basi Serikali kupitia Wizara husika ya Kilimo na Mifugo hebu ijaribu kuweka utaratibu basi, wahamasishwe kama ni kufundishwa kilimo cha kisasa au wenzetu wanataka kula mboga ambazo zipo *fresh*, basi Wizara ishirikiane na watu waliopo yale maeneo ya jirani iwaelimishe watu walime mboga za majani, wauziwe mle mgodini ili hawa watu wasiende kununua, naamini kabisa wakiona mboga zipo pale watanunua na hawataenda kununua Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata maziwa, Wasukuma wanaweza kuandaa maziwa vizuri kabisa wakisaidiwa na Wizara yao wataelekezwa wanataka *package* iwe, hao wenyewe wanunuzi watasema wanataka haya maziwa yawe ya kiwango gani watengenezewe na wauze mle ndani ili pesa hii isiende Kenya ibaki hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni ombi ambalo naliomba sana kwa Wizara husika, Waziri Mkuu utawaambia Mawaziri wako walishughulikie hilo na nitashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaridhika kama nitaondoka bila ku-*declare interest* kwamba mimi ni mwanamuziki, naitwa Vick Kamata, nimeimba wimbo wa Wanawake na Maendeleo na nyimbo nyingine nyingi tu mnazifahamu. Mfalme Suleiman mama Hewa kanikumbusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme neno moja kuhusu wasanii, ninaamini kabisa mchango wa wasanii katika nchi hii ni mkubwa na ndiyo maana hata Rais wetu alisema kwamba anawathamini wasanii kwa sababu anajua mchango wao. Tumeona nchi za wenzetu zilizoendelea Marekani kuna *Hollywood*, pato la Taifa la nchi ile linatoka *Hollywood* zaidi ya asilimia 20 wanachangia pato la nchi yao. Nenda India kuna *Bollywood*, nenda Nigeria unakuta kuna *Nollywood*, kwa nini Tanzania tusiwe na *Tollywood*, nadhani yote haya yanawezekana kama kweli tukiamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru pia Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda hivi juzi amewakaribisha vijana, amewakaribisha vijana wa *Bongo Movie* walivyokuja, hapa tukala naye chakula, tulikunywa naye, tukafurahi naye Waziri Mkuu wetu, tunampenda sana na tunamshukuru sana. Na zaidi ya yote aliwapa nafasi wale vijana wa *Bongo Movie* kueleza nini wanataka, wakamueleza kwamba wana mpango wa kuzunguka nchi hii kuhubiri amani kwa sababu wanaona kwamba kuna watu wanapotoshwa, kwa hiyo, Waziri Mkuu akasema kwamba lengo lenu ni jema na mimi kama Waziri Mkuu wenu nitawasaidia na kwa taarifa nilizonazo na nimetumwa na wasanii wa *Bongo Movie* nimwambie Waziri Mkuu kwamba wanashukuru sana ule mzigo wamepokea, wanampenda na wanamuombea sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, ninaomba nizungumzie jambo moja katika Bunge hili hili Rais wetu alilihutubia Taifa kupitia kwenye hili Bunge, alizungumzia anavyotuthamini sisi wasanii na akasema na kwa jinsi anavyotuthamini amesikia kilio chetu ametununulia chombo kinaitwa *Mastering Studio. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Mastering Studio* ambayo itatusaidia sisi wasanii kutoa kazi zenye kiwango kinachostahili cha Kimataifa. Lakini dhamira hii njema ya Rais wetu naona kama inataka kupotoshwa na watu wachache, kwa sababu inavyoonekana ni kama vile Rais wetu ametoa kitu kwa watu wachache, lakini mimi kama nilimuelewa vizuri Rais alivyokuwa anazungumza hapo mbele alisema *mastering studio* hii kaileta kwa wasanii wa Tanzania haijalishi walienda kupokea wasanii watano, walienda kuipokea wasanii kumi, walikuwa wametuwakilisha hata sisi ambao hatukuwepo*. (Makofi)*

Kwa hiyo, niiombe Serikali kupitia Wizara husika nadhani Mheshimiwa Nchimbi na Naibu wake wanasikia hebu waweke muongozo kwamba kuna utaratibu gani ambao umewekwa ili kila msanii aweze kunufaika na hiyo zawadi iliyotoka kwa Rais wake, ninaamini kabisa Rais huyu hapendelei, ametoa kwa wasanii wote, kwa hiyo, Waziri wa Utamaduni atuambie hiki chombo kipo kwa nani, kiko chini ya menejimenti ya nani na kama msanii anataka kutumia afuate utaratibu upi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima ninaomba Waziri alishughulikie hili kwa sababu limeshakuwa kilio kwa wasanii wengi, wasanii wengine wameshaanza kujenga chuki kwa Rais wao na sina hakika kama kweli jambo hili linatakiwa lifichwe lisiwekwe wazi. Tuambiwe kama hii zawadi ni kwa wasanii wote na mimi ndivyo ninavyoamini ni kwa wasanii wote, kama siyo kwa wasanii wote kuna mabadiliko fulani basi pia Waziri wa Wizara husika atuambie kwamba ni vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia*. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri, sasa nitamuita Mheshimiwa Agness Elias Hokororo na muda wetu kama utaturuhusu na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla naye atapata nafasi.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na nimeweza kusimama leo hapa kwa sababu ya uweza wake. *(Makofi)*

Pili, ninaomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Mtwara hasa wanawake wa UWT, kwa kuniwezesha kuwa katika jengo hili Tukufu kuweza kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusimamia vema na vizuri zaidi shughuli za Serikali, shughuli ambazo ni dhahiri za utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri wa TAMISEMI pamoja na Naibu Waziri na timu nzima kwa kazi nzuri na kwa kasi waliyoianza katika utendaji kazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie hotuba ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo; kwanza kabisa naomba nijielekeze katika sekta ya uchukuzi na hapa naomba niongelee eneo la bandari kama inavyoonekana kwenye kitabu hiki cha Waziri Mkuu ukurasa wa 34, na kwa ruhusa yako naomba nisome kwamba; "Katika mwaka 2010/2011 Serikali imeendelea kuboresha miundombinu katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kuhudumia meli na mizigo." Katika hili Serikali nitaomba itupe ufafanuzi mimi binafsi kama Mbunge wa Mtwara na kwa uelewa wangu hapa naona kuna maneno kidogo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari yetu ya Mtwara ilijengwa mwaka 1954 na tangu wakati ule mpaka sasa ninavyoongea saa hii bandari ile haijawahi kupanuliwa wala kufanyiwa marekebisho hata ya mita moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana marekebisho na matengenezo mengine yamefanyika ya miundombinu kwa bandari zingine lakini kwa Bandari ya Mtwara hili halijafanyika na hili linadhihirishwa na uwezo wa bandari yetu sasa. Bandari ya Mtwara ina uwezo wa kubeba mizigo tani 400,000 kwa mwaka lakini kutokana na ubovu wa miundombinu kwa maneno mengine miundombinu ya Bandari ya Mtwara ni ya kizamani kwa hiyo, inafanya kazi chini ya kiwango. Kwa mfano mwaka 2010 bandari yetu ya Mtwara iliweza kubeba mizigo tani 84,000 tu na mwaka huu mpaka kufikia mwezi huu wa sita sasa hivi ninavyoongea imeweza kubeba mizigo tani 220,000 tu. Kwa hiyo, hili linadhihirisha kwamba kutokana na miundombinu ya kizamani bandari hii haifanyi kazi kama inavyotakiwa, sasa hivi bandari ile inatumika na wawekezaji, sote tunafahamu kwamba kuna wawekezaji wanaoshughulika na gesi pamoja na mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa kuwa wote tunatambua ni sikivu, ifanye mambo mawili ambayo ni muhimu kwa maslahi ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara. Kwanza, Serikali iandae mkakati wa kujenga gati yenye uwezo mkubwa kwa Bandari ya Mtwara na pili Serikali ione namna ya kuifanya Bandari ya Mtwara kuwa ya kisasa kwa maana ya uwezo mkubwa. Ninapozungumzia uwezo mkubwa na bandari ya

kisasa naamanisha kwamba lazima tuhakikishe kwamba katika Bandari ya Mtwara ina mambo mawili; kwanza, lazima tuhakikishe kwamba katika Bandari ya Mtwara kutakuwa na gati *entrace* za kisasa lakini pia tuwe na *container terminal* ya kisasa. Tunaweza tukajiuliza ni kwa nini ziwepo kwa wakati huu na wakati bandari ile haifanyi kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa huo huo wa 34 inaonekana kwa mwaka 2011/2012 kwa Bajeti ya sasa hivi Serikali imeazimia kuboresha kama ilivyoandikwa hapa, itafanya upanuzi katika gati namba moja hadi saba za Bandari ya Dar es Salaam. Lakini kuna bandari ndogo ndogo za nchi kavu, lakini Bandari ya Mtwara haijatajwa kabisa. Wasiwasi wangu ni kwamba bado tutaendelea kuachwa nyuma watu wa Mkoa wa Mtwara na lingine ni kwamba tutakuwa hatujajielekeza katika mabadiliko tunayoyatarajia. *(Makofi)*

Katika mpango wa miaka mitano tumeona kwamba Mtwara kutakuwa na vitu vingi na wote tunajua kwamba Mtwara kuna gesi ya *Mnazi Bay* lakini pia kuna uchimbaji wa mafuta utaendelea. Sasa kama Mtwara itakuwa na viwanda vya saruji, chokaa, *plastic* na vinginevyo tunajiandaaje kukabiliana na changamoto hiyo? Wakati umefika sasa, mimi ninavyoelewa gati haiwezi kujengwa kwa siku moja na kuweka miundombinu ya kisasa, haiwezi kufanyika kwa miezi miwili. Serikali lazima ichukue hatua na sisi watu wa Mtwara tuweze kutoka katika umaskini wa miaka mingi kwani bandari tunayo.

Serikali ikionyesha nia ya dhahiri ya kulishughulikia hili ni wazi kwamba bandari ile itatumika kwa manufaa ya Tanzania nzima kwa sababu tukifanya haya mambo mawili niliyoyasema ina maana tutaweza kuwavutia wawekezaji lakini pia tutaweza kuwavutia hata wenye meli kwa sababu meli zinazofika pale sasa hivi ni zile zenye uwezo wenye kifaa ambacho kinaweza kubeba na kushusha mizigo. Kwa hiyo, tufanye haya mambo mawili na ndipo sasa tunaweza na sisi tukajitambua kwamba kweli itakapofika hiyo safari ya mapinduzi ya viwanda katika mkoa wa Mtwara na sisi tutaingia katika hiyo treni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende katika hoja nyingine. Naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika sekta ya elimu, naipongeza kwa sababu wote tumeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwa kiasi gani Tanzania tumefanikiwa kutekeleza baadhi ya malengo ya maendeleo ya milenia na hasa lile la kuwawezesha watoto ambao wana umri wa kwenda shule kwa mwaka 2010 tumefikisha 95.4%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kufanikiwa kujenga shule za sekondari karibu na wananchi kwenye Kata. Lakini pia katika vijiji vyote sasa hivi tunazo shule za msingi na kwenye vijiji vingine kama kule kwetu Lukuledi tuna shule zaidi ya moja. Naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu ninazo changamoto kadhaa; mimi nadhani tukitaka kujua kwamba namna bora ya elimu au elimu bora inapatikanaje, naamini ni kwa kuzingatia namna bora pia ya nyenzo au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la majengo, kama tunavyosema Serikali imefanikiwa kujenga lakini je, tunajiridhishaje kwamba elimu inayotolewa ni bora na inatolewa kwa kiwango kinachotakiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo idara ambazo naamini zikifanya kazi yake vizuri tutaweza kujiridhisha na tutaweza kufanikiwa, kwa mfano, Idara ya Ukaguzi, mpaka sasa hivi Idara hii mimi sioni kama inafanya kazi yake kama inavyotakiwa au haifanyi kazi yake kama inavyotakiwa, tukiwauliza wanasema ni kutokana na upungufu wa fedha yaani hawana fedha. Lakini Idara hii ingefanya kazi yake vizuri tungeweza tukaondoa baadhi ya lawama kwamba watoto wetu hawana akili au walimu hawafanyi kazi vizuri? Kwa sababu Idara hii inapokwenda kukagua kwenye shule ndiyo inaweza kubainisha je, walimu wanafundisha vipindi kama inavyotakiwa? Je, masomo yanaandaliwa vizuri? Je, uwiano au ukubwa wa darasa ndiyo unaotakiwa kwa maana ya *ratio?* Wabunge wamesema hapa madarasa yanafundishwa mwalimu mmoja kwa watoto 80, hivi vyote wakaguzi wangekuwa wanakwenda kukagua tungeweza tukavibaini mapema na vingeweza kupatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Lakini katika shule zetu za sekondari wakaguzi wamekuwa wakienda mara moja kwa miaka miwili, kwa idara hii kutofanya kazi yake vizuri kama ilivyokuwa huko nyuma inanitia mashaka kama tunaweza tukapata matokeo mazuri. Wakati mwigine kwenye vijiji vyetu unaweza ukakuta saa tano tu mwalimu amelewa; lakini wakaguzi wangekuwa wanakwenda kukagua hili lingeweza kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine katika sekta ya elimu ni mabadiliko ya mitaala ya mara kwa mara. Ni vizuri tukaangalia, ni kweli inawezekana mabadiliko haya yakawa na tija kama tunaamini kweli ni marekebisho ya msingi lakini je, walimu wanahusishwa, wanaandaliwa na wanapewa mafunzo? Wakati mwingine mabadiliko haya yanafanyika walimu wanakuwa bado hawajapata mafunzo na wala vitabu havijafika. Ni vizuri Serikali ikaona namna ya kushughulikia hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine katika elimu ni mwongozo uliotolewa na Baraza la Mitihani. Katika hili naomba niseme kwamba nilivunjika moyo sana tarehe 24 Juni, 2011 nilivyouliza swali hapa lakini likajibiwa kwa urahisi tu kwamba Mheshimiwa Mbunge hajasema ni eneo lipi mitihani inaulizwa kwa mtindo wa kuchagua A au B au C. Naomba niseme mwongozo upo kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge

tunavyouliza maswali hapa tunauliza ili tupate majibu ya zile kero ambazo zinatusumbua katika vichwa vyetu, hatuulizi kwa sababu tu ya kupoteza muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Mtwara nilivyouliza swali lile wangeweza kusema kwamba labda niliuliza swali la pupa kwa pupa, hapana! Nilikuwa na maana mwongozo uliotolewa na Baraza la Mitihani unaelekeza mitihani yote ya shule za msingi, darasa la saba kwa mwaka huu itajibiwa kwa mtindo wa A, B na C. Wasiwasi wangu ni je, hawa watoto tutakuwa tumewapima ujuzi? Tutakuwa tumewapima zile stadi ambazo tunazitarajia? Tunatarajia kweli watoto hawa waende sekondari wakiwa wamefaulu kwa uelewa tunaoutaka? Au inawezekana mwanafunzi akaamka, akasoma siku moja akafaulu mtihani wake mia kwa mia, lakini tutakuwa hatujamuandaa kwenda sekondari. Serikali lazima iangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo hilo la elimu, tunazo ofisi za *TSD* yaani *Teachers Service Department.* Hizi zilianzishwa ili kushughulikia masuala ya kupandishwa vyeo walimu, nidhamu kwa ujumla na kuthibitishwa kazini. Lakini hivi sasa vimegeuka kuwa vijiwe katika ofisi za Halmashauri kwa sababu hazina pesa, vikao vinavyopaswa kufanyika kushughulikia maeneo yote niliyoyasema hayafanyiki, ni vema Serikali iangalie, hatuna haja ya kuwa na idara ambazo hazifanyi kazi za msingi na kugeuza ofisi kuwa vijiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo hilo la elimu mbona zamani kulikuwa na mafunzo ya walimu wakiwa kazini? Idara na Wizara nyingine mafunzo yanatolewa, kwa nini walimu hawapati mafunzo wakiwa kazini? Mwalimu wa sasa hivi anaajiriwa mpaka anafikia umri wa kustaafu hajaenda hata kozi fupi ya mwezi mmoja. Lazima Serikali iangalie hilo. *(Makofi)*

Pia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tumeona kwamba tutakuwa na shule za sekondari za kidato cha tano na sita kwenye kila Tarafa. Katika Bajeti ya sasa nilitarajia tutakuwa tumeanza kujenga *hostel* za shule za kidato cha tano na sita lakini hakuna. Kwa hiyo, tujenge sekondari halafu tuanze kukimbizana na *hostel?* Nadhani ni suala ambalo tunatakiwa tulianze sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye eneo lingine la sekta ya kilimo. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, mtoto wa mkulima kwa wito au kauli mbinu ya Kilimo Kwanza. Sisi wananchi wa Mtwara tumeitikia kauli mbiu hii ya Kilimo Kwanza na kwa kuwa korosho zinalimwa kwa wingi watu wanaimarisha zaidi zao hili la korosho. Lakini tatizo langu hapa ni kwa mazao mchanganyiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa haina maana kama tunahamasisha wakulima hasa wadogo wanaolima kwa jembe la mkono halafu tusiwapatie masoko ya kuuza mazao yao. Wanawake wa Mtwara ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango mzuri, kwa namna yoyote lazima wewe ni mwalimu tu. Sasa nitamuita Mheshimiwa Profesa Peter Msolla na ndiye atakayekuwa mchangiaji wetu wa mwisho jioni hii. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imegusa maeneo mengi na ambayo kwa wale walioisikiliza toka mwanzo na hata walio nje ya Bunge hili imewapa matumaini makubwa. Kutokana na hilo nasema naunga mkono hoja hii kutoka mwanzo. *(Makofi)*

Kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuzungumza Bungeni ningependa nichukue fursa hii kuwashukuru sana wapigakura wa Jimbo la Kilolo kwa kunipa ushindi wa kishindo pamoja na chama changu cha Mapinduzi, na mimi napenda kuwaahidi kwamba sitawaangusha, tuendelee kushirikiana na tuyafanyie kazi pamoja ili kusudi Kilolo ya juzi isiwe ndiyo Kilolo ya kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza sana mazungumzo, hoja mbalimbali na michango ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao wametangulia. Kuna wachache ambao wamebeza maendeleo yaliyopatikana katika miaka 50 ya Uhuru wetu. Mimi nasema aliye na macho haambiwi tazama na aliye na masikio haambiwi sikia kwa sababu mambo yako wazi na wengi wametoa mifano mingi. Hata mzungumzaji aliyekaa sasa hivi amezungumzia katika maeneo ambapo kumekuwa na maendeleo licha ya upungufu uliopo lakini angalau tumethubutu, tumeanza na tunakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani kwa upande wa elimu, kila kijiji kina shule ya msingi, leo hii kila Kata ina shule ya sekondari pengine katika zile Kata ambazo zimeanzishwa juzi tu. Sasa wengine wamekuwa wakisema kuna matatizo katika elimu ni kweli, matatizo haya yamekuwepo. Tulipofika njia panda mwaka 2004/2005 vijana wengi waliomaliza darasa la saba walikuwa hawaendelei na kidato cha kwanza na sababu

siyo kwamba walikuwa wanafeli lakini walikuwa wanakosa nafasi katika shule za sekondari. Kwa hiyo, walizidi kurundikana nje na kama lingengoja mpaka tuwe na madarasa, walimu, maabara, maktaba na vitabu vya kutosha leo hii tungekuwa hatujafika hapa tulipofika. Kwa hiyo, mimi nathamini sana shule za sekondari zilizojengwa katika Kata zetu kwa mchango mkubwa wa wananchi na haya ni maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Vilevile hakuna haja ya kujiuliza mambo mengi, licha ya sekondari tumekwenda Vyuo Vikuu na mifano imetolewa na wengi wetu na si ajabu tuliopo humu ndani ni matokeo ya juhudi zilizofanywa na Serikali katika miaka 50 iliyopita. Kwa hiyo, tuna mifano mingi ukienda kwenye afya na maji kuna mifano mingi, ukienda miundombinu ndiyo usiseme! Leo tuna barabara ya lami, mtu unatoka Dar es Salaama mpaka Mwanza kwa muda mfupi, lini yalikuwepo hayo? Kwa hiyo, sitaki kuchukua muda mrefu kuelezea juu ya mafanikio yaliyokwishapatikana, lakini nilitaka kuwa shahidi kwamba kwa kweli kumekuwa na maendeleo makubwa. Hata mimi katika Wilaya yangu ambayo wakati ule haikuwepo na sasa Kilolo ipo kwa hiyo, kuna maendeleo makubwa. Kuna maeneo katika Wilaya yangu ambayo toka dunia ilipoumbwa hata basi walikuwa hawajawahi kuliona, lakini leo hii mabasi yanafika mpaka maeneo hayo. Kwa hiyo, hayo ni maendeleo makubwa na siyo jambo ambalo tunaweza tukalibibishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie juu ya utatu mtakatifu kwa maana ya mafiga matatu, wengi wamezungumza juu ya jambo hili. Ni jambo linazozungumzwa sana na wenzetu Madiwani na Wenyeviti wanasikiliza na wanaamini Serikali yao ambayo ni sikivu, itasikiliza suala hili na kilio hiki ili kusudi mazingira wanayofanyia kazi yazidi kuboreshwa. Kwa sasa wanaishi kwa posho, mimi nasema posho za vikao waendelee kupata lakini wapate mshahara mwisho wa mwezi. Kama kuna sheria ambazo zimekuwa zikizuia basi tuangalie upya hizo sheria ili wapate mshahara na mwisho wa siku waweze kupata chochote cha maana baada ya kuacha hizo kazi. *(Makofi)*

Vilevile waweze kupata vyombo vya usafiri ili watembee katika maeneo ambayo ni magumu kufuatilia miradi mbalimbali ambayo inatekelezwa na Halmashasuri zetu. Leo hii inakuwa vigumu kwa Diwani kutembea kwa miguu kilomita 30 kutoka eneo moja hadi lingine halafu akarudi tena kwa ajili ya kukagua miradi kwa hiyo, jambo hili naliunga mkono na wengi waliozungumza nawaunga mkono sana kwa ajili ya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu maji vijijini, hili bado ni tatizo na hasa mimi nijikite katika mradi wa vijiji kumi kwa kila Halmashauri. Mradi huu ulianza mwaka 2000 na umekuja kuanza kutekelezwa mwaka 2009, imepita miaka karibu nane au tisa. Gharama za wakati ule kwa visima kumi ilikuwa pengine inakidhi, lakini kwa leo hii kutokana na gharama kuongezeka visima hivyo kumi kwenye Halmashauri haviwezi kufikiwa. Kwa hiyo, utakuta fedha zimepelekwa wakati huu lakini tumeambiwa na Wizara husika kwamba chagueni wenyewe fedha mtakazopata zitatosha, vijiji vitatu au vinne. Sisi tunashukuru hata hilo dogo kwa sababu usiposhukuru hata kwa dogo hata ukipewa kubwa hutashukuru.

Sasa Serikali ioneshe nia ya makusudi kabisa kwa sababu wananchi tayari wameshachanga fedha na fedha hizo zimewekwa benki na wanajiuliza, kila siku kuhusu hili. Ni vema Serikali ikachukua hatua kusudi itafute fedha ili mradi huu uweze kukamilika. Najua kuna awamu ya pili ya mradi huu lakini kwa ule mradi wa kwanza bado kuna manung'uniko makubwa.

Kwa hiyo, Serikali kama ingechukua hatua za makusudi za kutafuta fedha ili kusudi waweze kumalizia huu mradi katika maeneo mbalimbali. Tatizo la maji haliko vijijini tu, katika jimbo langu nina mji mdogo ulionziswa mwaka 1968 unaitwa Ilula. Mwaka 1968 kulikuwa na watu 3,000 tu lakini leo hii kuna watu 40,000. Maji na miundombinu iliyopo haitoshi na watu wanatumia muda mrefu sana kwa ajili ya kutafuta maji. Ningeomba sana tatizo la maji kwa mji mdogo wa Ilula liweze kupatiwa ufumbuzi ili kusudi wananchi waweze kuishi katika maisha ambayo wanayatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu rasilimali watu. Mimi nilifurahi sana kuona kwamba katika ile *skills development levy* 4% inakwenda kwenye Bodi ya Mikopo. Lakini kutokana na mpango tulioanza wa MMEM, ikaja MMES ni kwamba tutarundika watu wengi sana wanaomaliza kidato cha nne, kwa sababu hata kidato cha tano bado kuna upungufu na wanaokwenda Vyuo Vikuu ni wachache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufundi ndiyo sehemu ambayo ingetusaidia kutuokoa pamoja na ujasiriamali. Kwa hiyo, ninaomba sana ujenzi wa vyuo vya ufundi upewe kipaumbele ili tupate vijana wengi zaidi ambao wana *competence* ambao wanaweza kujiajiri wenyewe na kuwaajiri watu wengine.

Kwenda Chuo Kikuu ni njia mojawapo, lakini kwa kweli wale unaowapeleka Vyuo Vikuu wale ni *think tanks.* Anaweza kuchora *engine* ya gari, lakini ukimpeleka kwenye *engine* yenyewe ya gari iliyosimama hapo hawezi kukusaidia jambo. Lakini hawa ambao wana *hands on skills* ndio ambao wanaweza kutusaidia zaidi, ni mfano wa jeshi. Hata jeshi halifundishi ma-*generals* tu, linafundisha na askari wa kawaida *infantry* kwa sababu hawa ndiyo wapiganaji wenyewe. Huwezi ku-*train* ma-*generals* watupu ukasema una Jeshi kwa sababu huwezi kufika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie tatizo la Kihesa Mgagao katika wilaya ya Kilolo. Kihesa Mgagao ilikuwa ni kambi ya wapigania Uhuru kutoka Kusini mwa Afrika. Ilichukua wapigania Uhuru kutoka *South Africa,* Namibia, Zimbabwe na Angola, waliishi pale chini ya mafunzo ya JWTZ. Walipoondoka baada ya kumaliza mafunzo na kupata Uhuru, eneo lile lilikabidhiwa Magereza ambapo wanafunga watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya iliomba mahali pale paendelezwe na kuweka historia kwa kujenga shule ya wasichana ya kidato cha kwanza

mpaka cha sita. Lakini pamoja na ombi hilo kutolewa bado mpaka sasa halijapatikana jibu kamili. Rais alipokuwa katika ziara yake tarehe 5 Agosti, 2008 wananchi waliwasilisha ombi hilo na Rais walitamka kwamba Magereza wahamie mahali pengine jambo ambalo halijatekelezwa mpaka leo. Ni matumaini yangu kwamba tutapata jawabu katika maelezo ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na nawatakia kila la kheri katika hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. Waheshimiwa Wabunge huyo ndiye alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho jioni hii, lakini kabla ya kuahirisha Bunge naomba nitoe tangazo. *(Makofi)*

Itakumbukwa kuwa tarehe 23 Juni, 2011 tulitengua Kanuni ya 38(3) inayohusu maswali kwa Waziri Mkuu ili kumuwezesha kujiandaa vizuri na hotuba ya Bajeti yake. Kutokana na kibali hicho cha Bunge na kwa kuwa tumeongeza muda wa mjadala, kesho siku ya Alhamisi hakutakuwa na maswali kwa Waziri Mkuu ili tumpe fursa zaidi ya kujiandaa. Baada ya tangazo hilo sasa naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,*

*Tarehe 30 Juni, 2011 saa tatu asubuhi)*